# Nipashe

Jumatatu Oktoba 10, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581094

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710 LIKE & FOLLOW US






JACKPOT BABA LAO!

TZS. 367,741,460

KWA TZS. 1000 TU!

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

SportPesa.co.tz

PIGA *150*87#




**ACT:** Muswada Bima Afya una shida, usitishwe

UKURASA 3

MAKALA MAALUM

# Asimulia alivyosota miaka 18 akisubiri siku ya kunyongwa

• **Apoteza** familia, wazazi na mali zote... *Endelea ukurasa 4*



Tete Kafunja, mwathirika wa adhabu ya kifo aliyenusurika kunyongwa (kushoto), akihojiwa na mwandishi wetu.
**PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## YALIYOMO


UKURASA WA 2

**RAIS SAMIA ASHTUKA MMOMONYOKO MAADILI**

RAIS Samia Suluhu Hassan amewataka viongozi wa dini kusimamia suala la...

UKURASA WA 8

**NMB YAONGEZA KIWANGO MKUPUO MMOJA WA MKOPO HADI BIL. 250/-**

UFANISI mkubwa wa kiutendaji ambao Benki ya NMB imeupata miaka ya hivi...

UKURASA WA 21

**MBARONI AKITUHUMIWA KUMNG'ATA SIKIO MKEWE**

JESHI la Polisi Mkoa wa Songwe linamshikilia Nadi Said (60) kwa tuhuma za...


## Kila watu 4, mmoja ana tatizo la akili

UKURASA 2



## Mbu wageuka sugu kwa dawa, wanauma mchana

UKURASA 5

**MICHEZO** NABI: SUBIRINI DAKIKA 90 SUDAN UK.32

**KABWELA** UK.7

# Rais Samia ashtuka mmomonyoko maadili

**Na Jenifer Gilla**

RAIS Samia Suluhu Hassan amewataka viongozi wa dini na waumini kusimamia suala la maadili mema katika jamii kwa kuwa sasa linaonekana kurudi nyuma katika jamii.

Aliagiza hayo jana aliposhiriki Baraza la Maulid lililoandaliwa na Baraza Kuu la Waislamu Tanzania (BAKWATA) Taifa kwenye Ukumbi wa Diamond Jubilee jijini Dar es Salaam.

"Maadili haya ni mtetereko uliotokea katika taifa letu, kama viongozi, wazazi tulitetereka mahali. Kwa hiyo, turudi tukatizame wapi tulitetereka. Tufundishane tuongoze watoto wetu wapate maadili," aliagiza.

Rais aliwataka viongozi hao kukemea vitendo viovu ikiwamo vya kuuana, kudhurumiana na kuoneana, ambayo vipo katika taifa, akisisitiza serikali itafanya kazi kadri inayoweza kuvitokomeza.

"Siku kama hizi wafuasi wa dini na madhehebu mbalimbali huweka kando tofauti au hitilafu zao, na wote kuafikiana kuwa na misingi mikuu itakayoweka utamaduni wa maisha ndani ya dunia yetu," alisema.

Rais Samia pia aliwataka viongozi hao kushirikiana na Wizara ya Afya kuelimisha umma kuhusu maradhi ya ebola ambayo sasa yameingia nchini.

Pia aliyataka madhehebu ya dini pamoja jamii kutumia teknolojia kuendelea kufundisha watoto dini ili kuhakikisha wale wasioweza kuhudhuria masomo hayo, wajifunze wakiwa nyumbani.

"Tujipange vyema kutumia sayansi na teknolojia ili tutoe mafundisho kwa watoto kwa wakati ule ambao watakuwa wametulia majumbaili. Kwa wale watakaowahi madrasa waende madrasa, wakati umebadilika na sisi tubadilike," Rais Samia alisisitiza.

Sheikh Mkuu na Mufti wa Tanzania, Dk. Abubakar Zubeir pia alisisitiza umuhimu wa taifa kuwa na maadili na tabia njema kwa kuwa ndiyo msingi wa maendeleo katika jamii.

"Kwa hiyo, taifa lolote, watu wa aina yoyote, popote walipo, kama hawana tabia njema, wala hawana maadili, basi lazima uhesabu pia hawana mafanikio," Mufti alifafanua hoja yake.

Katibu Mkuu wa BAKWATA, Alhaji Nuhu Mruma, alisema baraza linaipongeza serikali na vyombo vya ulinzi na usalama kwa kuendelea kuimarisha amani nchini.

Pia alisema baraza linalaani vitendo visivyo vya kibinadamu vinavyoendelea katika jamii na kuitaka jamii kufuata matendo yaliyo sahihi aliyokuwa akiyasimamia kiongozi wa umma wa Kiislamu, Mtume Mohammad ili kuishi maisha ya furaha.

"Hivi karibuni katika nchi yetu tumekuwa tukiona na kusoma katika vyombo vya habari matukio mbalimbali kama vile mauaji ya binadamu wenzetu kwa visingizio mbalimbali, wizi, uvunjaji wa nyumba hususan panya road (vijana wahalifu wa mitaani), hayo yote hayakubaliki katika jamii iliyostaarabika," alisema.

Alitaja maficho ya uovu huo ni watoto kutohudhuria masomo ya dini vizuri kutokana na ufinyu wa muda, kwa kuwa muda mwingi wanakuwa shuleni, hivyo kukosa elimu ya dini ambayo ina maadili mema.

Baraza hilo lilihudhuriwa na viongozi mbalimbali wakiwamo Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson na wakuu wa vyombo vya ulinzi na usalama.

**UJIO WA RUTO**

Katika hatua nyingine, Rais wa Jamhuri ya Kenya William Ruto, jana aliwasili nchini kwa ziara ya kikazi ya siku mbili na kupokewa na Waziri wa Mambo ya Nje ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Dk. Stergomena Tax.



Waumini wa dini ya Kiislam, wakiwa katika matembezi maalum ya kuazimisha Maulidi ya Uzawa wa Mtume Muhammad (S.A.W), yalioandaliwa na wamiliki wa Kiwanda cha kuzalisha nguo cha Nida Textile jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Askofu KKKT aiomba serikali kupunguza kodi vituo huduma

**Na Adela Madyane,** KIGOMA

MKUU wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Dk. Fredick Shoo, ameiomba serikali kuwapunguzia gharama za kodi kwenye vituo wanavyotoa huduma za kijamiii ikiwamo shule na hospitali ili kueneza injili na kuisaidia jamii.

Alitoa ombi hilo wakati wa sherehe za uzinduzi wa Dayosisi ya Ushirika wa Magharibi mkoani Kigoma baada ya kanisa hilo kudumu kuwa misheni kwa muda wa miaka 40 na kuifanya kuwa dayosisi ya 27 pamoja na kumsimika askofu mkuu wa dayosisi hiyo.

"Kodi ya ardhi ya kuweka miundombinu pamoja na uendeshaji wa vituo vyetu vya kutoa huduma ni kubwa, zinatuelemea, tunaomba serikali iweze kupitia upya ili kanisa lisione kama adhabu kuendelea kutoa huduma hizo," alisema.

Askofu Shoo alisema ukatili unaoendelea katika jamii unayofanywa na familia, taasisi za dini za kiserikali na zisizo za serikali pamoja na mtu binafsi ni matokeo ya malezi na makuzi ya watoto na kile wanachokiona wanapokuwa nyumbani, shuleni na hata kwenye televisheni, hivyo ni jukumu la jamii kuwakuza watoto katika maadili na hofu ya Mungu.

"Ninaiomba jamii kwa pamoja tushirikiane kufanya malezi chanya kwa watoto ili kuwa na taifa lenye maadili, tusimame kwa pamoja kulinda tunu iliyomo ndani ya watoto wetu, tusimamie haki na maono yao kama watu wa taifa moja, tusiwanyanyase wala kuwafanyia ukatili, kwani hata vitabu vya Mungu vimekataa kufanyika kwa matendo hayo," alisema.

Askofu Jackson Mushendwa aliyewekwa wakfu kuwa Askofu Mkuu wa Dayosisi ya Magharibi akisaidiwa na Melikizedeki Kusesa, aliwataka wana dayosisi kujituma na kufanya kazi ili kujisimamia wenyewe na kuepuka utegemezi kutoka dayosisi nyingine.

"Tijizatiti kufanya kazi ili kukidhi mahitaji yetu yote muhimu ya chakula, mavazi, elimu, afya na malazi bila kunung'unika, tumshudie Kristu kwa matendo yanayosadifu, tuepuke kufanya kazi goigoi na kula milumilu," alisema Mushendwa.

Askofu Mushendwa aliwaonya washirika kutopenda ushirikina kwa kuwa wapo baadhi ya watumishi wa Mungu wenye uwezo wa kumwombea mtu.

Waziri anayeshughulikia Ajira, Kazi, Wazee na Vijana katika Ofisi ya Waziri Mkuu, Prof. Joyce Ndalichako, alisema inawapaswa kutoa mapendekezo ya kodi zinazowaumiza ili zifanyiwe kazi kwa mwaka wa fedha 2023/24.

# Bingwa Muhimbili: Kila watu 4, mmoja ana tatizo afya ya akili

**Na Mwandishi Wetu**

LEO ni kilele cha Siku ya Afya ya Akili Duniani huku Tanzania inakadiriwa kuwa mtu mmoja kati ya wanne anaishi na matatizo ya akili.

Mtaalamu wa Afya ya Akili na Mhadhiri wa Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi cha Muhimbili, Dk. Isaac Lema, alibainisha hali hiyo wakati wa mkutano na wahariri wa vyombo kuhusu masuala ya afya ya akili mwishoni mwa wiki mkoani Dar es Salaam.

Alikumbusha kuwa matatizo ya akili siyo ugonjwa, bali ni hali kama kuwa na hofu, mfadhaiko, msongo wa mawazo, wasiwasi, hasira, mihemko na kila mtu ana shida hizo, akisisitiza siyo jambo la kuogopa, bali kutibu.

Aliwashauri Watanzania kupima afya ya akili zao na kusisitiza kuwa vipimo na utaalamu upo kwa watoa huduma wa afya na matatizo hayo yana ufumbuzi na yanatibika.

Alisema jambo linalosababisha matatizo hayo ni kuzidiwa msongo unaotokana na mambo kusongamana na akili kushindwa kuhimili au kuyadhibiti.

Dk. Lema alisema kupima na kufahamu afya ya akili ni muhimu wakati huu ili kuwa na ukamilifu wa michakato na ustawi wa akili, mwili na jamii.

Alikumbusha kuwa mara nyingi watu wakiumwa homa, mifupa, kisukari au kichwa wanaripoti hospitalini na kuanzia sasa wanapopata matatizo ya afya ya akili kama sonona, hofu, wasiwasi, woga, hasira na ukali, waende hospitalini.

Akizungumzia vipimo vya afya ya akili, alisema watu hawafahamu kuwa vinapatikana na kueleza kuwa ni pamoja na kutumia nyenzo mbalimbali kama maswali, mahojiano na mazungumzo na daktari ili kutambua hali ya akili ya mgonjwa.

Alishauri ukienda kumwona daktari, ni vyema kumwambia unataka kupima afya ya akili, ili kuchunguza viwango vya msongo na sonona vinayoongezeka kwa kasi ndani ya jamii.

"Tukifanya hivi tutapunguza shida ya matatizo ya akili. Tupime hata mara mbili au tatu kwa mwaka. Ugonjwa wa sonona uko katika kiwango cha juu na una dalili zake, ndiyo maana ukimweleza daktari anakuchunguza tufahamu nyenzo zipo.

"Mtaalamu atakushauri kuacha mambo kama unywaji pombe kupindukia, atakuelezea tiba iwapo ni matatizo ya kunyanyaswa, kudhalilishwa na kudharauliwa na ikibidi kwenda kwa wataalamu wabobezi kuchunguzwa zaidi.

"Anaweza kukushauri pia kupumzika, kulala, kufanya mazoezi, hivyo ni vyema kuanzia sasa kubadilika na kutafuta tiba ili isifikie watu kuwa na magonjwa ya akili," alisema.

Akizungumzia magonjwa ya akili, Dk. Samwel Lindikoki, mbobezi wa tiba ya magonjwa ya akili katika Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), alisema kuna aina zaidi ya 280 za maradhi ya akili na siyo kwamba kuwa na ugonjwa ni mtu kufikia hatua ya kuokota makopo.

"Matatizo yanaanza utotoni, kwa mfano wapo watoto watukutu, watundu wasiotulia. Kuna usonji, wakorofi, wanaokula magodoro wapelekeni hospitali watibiwe," alisema.

Alitaja hofu na tatizo la wanaume kuhofia kupungukiwa na nguvu za kiume na kuongeza kuwa yote hayo ni matatizo ya afya ya akili, hivyo waende kwa wataalamu.

**HABARI KITAIFA**

# Tiba shufaa kuimarishwa

**Na Jenifer Gilla**

MGANGA Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Dk. Said Mfaume, amesema wanatarajia kuboresha huduma ya tiba shufaa kwa kuendeleza rasilimali watu, ili kuwapunguzia maumivu watu wenye magonjwa ya muda mrefu.

Aliyasema hayo mwishoni mwa wiki wakati akifungua mdahalo wa kisayansi wa tiba shufaa uliofanyika katika Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi cha Muhimbili (MUHAS), ukiandaliwa na Chama cha Madaktari wa Tiba Shufaa wa Afya ya Jamii (EAPCON).

Dk. Mfaume aliwataka viongozi wa kisiasa na wadau wote Mkoa wa Dar es Salaam kushirikiana kuhamasisha umuhimu wa kutoa huduma hiyo, ili iwe sehemu ya majukumu ya kila siku ya jamii.

"Ninataka Dar es Salaam iwe mfano, inawezekana wenzetu wakawa wanasita lakini kama tukifanya vizuri, inaweza kuwa chachu ya maboresho ya sera," alisema Dk. Mfaume.

Pia alisisitiza umuhimu wa eneo hilo kufanyiwa uchunguzi na kutolewa machapisho ili kuwapo takwimu zinazoonyesha ukubwa wa tatizo pamoja na kuboreshwa mifumo ya utoaji wa taarifa. "Tunaposema watu wengi hawajafikiwa na huduma ya tiba shufaa, tujue ukubwa wa tatizo ukoje kwa Dar es Salaam. Jambo la kuwa na takwimu ni la muhimu sana. Na naamini wizara inaweza ikajifunza na kufanya kwa mikoa mingine," alisema.

Aliongeza kuwa ofisi yake iko tayari kushirikiana na wadau hao ikiwamo viongozi wa dini na vyama vya wazee, ili kuhakikisha jamii inakuwa na uelewa wa kutosha kuhusu utoaji wa huduma hiyo muhimu.

Mwenyekiti wa EAPCON, Dk. Frank Manase, alisema waliandaa mdahalo huo ili kuwakumbuka watu wanaotoa huduma hiyo na kujadili namna ya kuboresha, kuwasaidia watu wenye maumivu ya muda mrefu.

"Tiba shufaa ni tasnia ya utabibu ambayo kazi yake kubwa ni kuwaondolea maumivu wagonjwa. Maumivu haya ni kama ya kimwili, kijamii hata kiimani, mfano mtoto anapomhudumia baba yake wakati mila hairuhusu, huyu baba anapata maumivu," alifafanua Dk. Manase.

Mkurugenzi wa Programu ya Afya, Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Dk. Paul Mmbando, alisema watoa huduma wamekuwa wakiongeza maumivu kwa wagonjwa hao kutokana na namna wanavyowahudumia.

Alisema hali hiyo inasababisha wagonjwa kukata tamaa na mioyo yao kufa kwa sababu ya maumivu mara mbili wanayoyapitia.

Alisema kuna taasisi 100 pekee nchini zinazotoa tiba shufaa na kusababisha wagonjwa na wazee wengi wanayoihitaji huduma hiyo kutoipata na hivyo kufa wakiwa katika maumivu makubwa.

Kwa mujibu wa Shirika la Afya Ulimwenguni (WHO), watu milioni 58 wanahitaji huduma hiyo huku wanaoipata ni asilimia 14 pekee.

# Polisi walivyomnasa kidigitali mtuhumiwa wizi wa watoto

**Na Gideon Mwakanosya,** SONGEA

JESHI la Polisi mkoani Ruvuma kwa kushirikiana na askari wa kitengo cha uhalifu wa kimtandao wamemkamata mfanyabiashara Merry Duwe (40), mkazi wa Mwengemshindo, Manispaa ya Songea akiwa na watoto wawili wanaodaiwa kuibwa Oktoba 4, mwaka huu, Salasala jijini Dar es Salaam.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Ruvuma, Michael Chilya, alisema walimkamata Oktoba 8 eneo la Kijiji cha Litola wilayani Namtumbo ambako alikuwa na watoto hao wenye jinsi ya kike na kiume.

Alifafanua kuwa Oktoba 4, mwaka huu, eneo la Salasala jijjini Dar es Salaam, mtuhumiwa alikwenda nyumbani kwa Zenatha Majaliwa, mama wa watoto walioibwa na kumkuta mume wake ambaye alimwomba hifadhi ya kulala na kumruhusu.

Alisema siku iliyofuata, asubuhi baba wa watoto hao alikwenda kazini na kuwaacha na binti wa kazi, kitendo kilichompa nafasi mtuhumiwa kuwachukua watoto hao kwa kuwadanganya kuwa anakwenda kuwanunulia pipi na kutokomea nao kwa usafiri wa bajaji.

Alisema baadaye alishuka kituo kilichofuata na kupanda daladala hadi Ubungo ambako inadaiwa alipata usafiri wa lori uliowafikisha Morogoro.

Kamanda Chilya alisema mtuhumiwa baadaye alipata usafiri mwingine wa basi kutoka Morogoro hadi Iringa na kupanda gari lingine la abiria ambalo liliwafikisha Njombe Mjini na kupata usafiri mwingine hadi Songea.

Alifafanua kuwa baada ya Jeshi la Polisi kupata taarifa ya kuibwa kwa watoto hao, lilianza juhudi za kuwatafuta.

Alisema kuwa baadaye jitihada zilifanyika kwa ushirikiano kati ya askari polisi wa kitengo cha uhalifu wa kimtandao, Polisi Ruvuma pamoja wazazi wa watoto na kufanikisha kumkamata mtuhumiwa akiwa na watoto hao ambao walikutwa wakiwa katika hali nzuri, japo wanaendelea kufanyiwa uchunguzi zaidi wa afya zao.

Mama mzazi wa watoto hao, akizungumza na Nipashe jana, alisema mtuhumiwa kabla ya kuwaiba wanawe, alikuwa na uhusiano naye katika shughuli za biashara.

Alisema kuwa Oktoba 4, mwaka huu, asubuhi mtuhumiwa Merry aliwaiba watoto na kutokomea nao kusikojulikana na baadaye alipigiwa simu kuwa watoto wote wawili anao na hawezi kuwarudisha mpaka alipwe fedha zake, jambo ambalo lilimlazimu aendelee kumtafuta licha ya kuwa tayari alikuwa ameshatoa taarifa polisi kuhusu kuibwa kwa watoto wake.

Zenatha alilishukuru Jeshi la Polisi kwa jitihada walizozifanya za kufanikisha kuwapata watoto wake wakiwa salama kwa kuwa alishakata tamaa kuwapata.

# ACT: Muswada Bima ya Afya kwa Wote usitishwe

**Na Maulid Mmbaga**

CHAMA cha ACT-Wazalendo kimependekeza kusitishwa kwa Muswada wa Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote, kikitoa sababu kwamba una upungufu mwingi na utaongeza idadi ya wanachama kabla ya kutatua matatizo yaliyokwamisha mfuko husika.

Msemaji wa Sekta ya Hifadhi ya Jamii wa chama hicho, Mwanaisha Mndeme alitoa angalizo hilo jana mkoani Dar es Salaam alipokutana na waandishi wa habari, akisisitiza kuwa chama chao kimebaini muswada huo haulengi kutatua matatizo yaliyoko.

Muswada huo uliwalishwa bungeni Septemba 23, mwaka huu na unatarajiwa kusomwa kwa mara ya pili, kujadiliwa na hata kupitishwa katika mkutano unaofuata wa Bunge.

Alisema muswada huo umeeleza adhabu zitakazotolewa kwa watumiaji na watoa huduma watakaokiuka Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote, lakini haujaelezea udhibiti wa ubadhirifu wa fedha za mfuko wa bima kupitia mamlaka za serikali.

Mndeme alisema muswada huo umeipa serikali kupitia kwa waziri mwenye dhamana mamlaka yatakayoingilia majukumu ya mamlaka ya usimamizi wa bima, akieleza kwamba unachochea mwendelezo wa ubadhirifu wa fedha za mifuko ya hifadhi za jamii ulioanza miaka ya nyuma.

Aliongeza kuwa muswada huo umeweka vigezo vya kupata leseni, pasi ya kusafiria, kitambulisho cha taifa, laini za simu hadi uwe na kadi ya bima ya afya, huku akieleza kwamba utaratibu huo unawanyima wananchi uhuru na haki yao ya msingi ya kupata huduma hizo ambazo tayari wanazilipia kupitia kodi na tozo mbalimbali.

Alikumbusha kuwa katika maelezo ya Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, watu wasio na uwezo watatambuliwa kupitia taarifa za uanachama wa Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF), akidai kuwa utaratibu huo hautajumuisha watu wengi zaidi wenye kipato kidogo kwenye sekta isiyo rasmi wasio na vigezo vya kunufaika na TASAF.

Alisema muswada huo pia haujagusa kichocheo cha ongezeko la gharama za dawa, vifaa tiba na vipimo ambao unaamuliwa na soko la dawa.

Hivyo, alipendekeza kuwa kila mwananchi mwenye ajira rasmi na kukatwa michango ya hifadhi ya jamii, apate fao la matibabu, kwamba mifuko ya NSSF na PSSSF, ambayo mwajiriwa ana mchango wake, upeleke moja ya tano (1/5) ya mchango wa mwajiriwa katika skimu ya bima ya afya.

Pia alishauri kila mwananchi aliyejiajiri kwenye sekta ya kilimo, biashara au shughuli nyingine yoyote na ni mwanachama wa hiari katika mfuko wa hifadhi ya jamii anayechangia kiwango cha chini cha mchango wa mwezi Sh. 30,000, achangiwe na serikali theluthi ya mchango kila mwezi.

"Hii itakuwa kivutio kwa watu walio kwenye sekta isiyo rasmi kujiunga kwenye mfuko wa hifadhi ya jamii na kupata bima ya afya, NSSF iwasilishe kwa skimu ya bima ya afya 1/5 ya mchango huu kila mwezi kwa ajili ya fao la matibabu la mwanachama.

"Mapendekezo ya serikali katika muswada ni kuwa mwanachama atatakiwa kuchangia Sh. 340,000 kwa mwaka kwenye mfuko wa afya kwa ajili ya matibabu pekee na serikali haichangii chochote.

"Mtu yeyote ambaye ni mnufaika wa TASAF alipiwe mchango wake kwa hifadhi ya jamii na serikali moja kwa moja kwenye NSSF kwa asilimia 100," alishauri.

Pia alishauri kuwa mfuko wa hifadhi ya jamii uanzishe fao maalum la kuwawezesha kuzalisha kipato ili kufikia kundi la kuchangiwa theluthi tu.

Vilevile, alipendekeza kuwa Mamlaka ya Usimamizi wa Sekta ya Hifadhi ya Jamii (SSRA) isimamie na kudhibiti skimu ya bima ya afya badala ya Mamlaka ya Usimamizi wa Bima (TIRA) kama ilivyo sasa.

Alisema endapo hayo yatazingatiwa, chama hicho kina uhakika kila Mtanzania mwenye umri zaidi ya miaka 18 atakuwa na bima ya afya kama fao miongoni mwa mafao ya mfumo wa hifadhi ya jamii nchini.


**KUPOTEA KWA KADI YA GARI**

**SABA GENERAL ENTERPRISES LTD** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye usajili namba **T110 CYE , CHASSIS NAMBA 1FSGE2PK002458, ENGINE NAMBA: 162FMJE5079209.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

**POLISI TAARIFA: ARU/ARU/RB/399531/2022**

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 136 OF 2022**
**In the matter of the Estate of the late**
**GETRUDA EVANCE MBISHI of Madukani Area within Dodoma Region**
**AND**
**IN THE MATTER OF THE APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION**
**BY JAMES MICHAEL MACHALLO**

**GENERAL CITATION**
**(RULE 75 OF PROBATE RULES GN NO. 369 OF 1963)**

**ALL PERSONS** claiming to have any interest in the Estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the **17 Day of 10,2022.**

**Date at Dodoma this 08 Day of September, 2022.**

RESIDENT MAGISTRATE

RESIDENT MAGISTRATE
DODOMA DISTRICT

# Simulizi ya kusisimua aliyesota jela miaka 18 kwa mauaji ya kusingiziwa

## ●Apoteza familia, wazazi, mali zote zauzwa

Na Mwandishi Wetu



Tete Kafunja, mwathirika wa adhabu ya kifo aliyenusurika kunyongwa (kushoto), akiwa katika mahojiano na mwandishi wetu.

LEO ni Siku ya Kupinga Adhabu ya Kifo Duniani, ambayo kwa Tanzania hutolewa dhidi ya watu wanaokutwa na hatia na Mahakama Kuu ya Tanzania, huku baadhi wakijikuta kwenye adhabu hiyo kwa kutotenda kosa husika.

Tete Kafunja (66) ni mfungwa aliyehukumiwa kunyongwa na kunusurika baada ya kukaa gerezani kwa miaka 18 kwa uonevu.

Sasa anamwomba Rais Samia Suluhu Hassan katika utawala wake kutotia saini hati ya kifo ili kuwanusuru watu wengi wasio na hatia kunyongwa.

Alihukumiwa kunyongwa akiwa na umri wa miaka 34 na ni mtoto pekee kwenye familia yake. Alipoachiwa huru alikwenda kijijini kwao Ileje na kukuta wazazi wake wameshafariki dunia na mashamba yao yameuzwa kwa kuwa walijua amehukumiwa kunyongwa na asingerejea tena kijijini huko.

Mpaka leo hajafanikiwa kukutana na mkewe na watoto wake wawili, jambo analosema linamuumiza moyoni.

Kafunja anaiomba serikali kurekebisha sheria na kutoa hukumu ya kifungo cha maisha kwa wote watakaopatikana na kesi za mauaji ili kunusuru roho za watu wasio na hatia na kuwawezesha kukata rufani.

Katika mahojiano na Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Vyombo vya Habari kwa Maendeleo ya Jamii (TAMCODE), Rose Mwalongo, hivi karibuni kuelekea maadhimisho ya Siku ya Kupinga Adhabu ya Kifo Duniani inayoadhimishwa kila mwaka Oktoba 10, Kafunja anasimulia maisha yake kabla ya kukamatwa, alivyokamatwa, alivyohukumiwa na kusihi gerezani na namna alivyotoka kwa msamaha.

Akisimulia tukio hilo, Kafunja anasema alikuwa mfanyabiashara wa baa eneo la Manzese mkoani Dar es Salaam iliyoitwa Mary.

"Mnamo mwaka 1990 nilikuwa kwenye biashara yangu ndipo polisi walipokuja na kuniuliza kama nilifahamu mtu ambaye nilimjua kama Kidevu, wakanijuza kuwa anaomba kuwekewa dhamana na nilikubali. Cha ajabu nilipofika kituoni, nilishikwa na kuwekwa ndani na polisi waliniambia kuwa Kidevu amesema nilikuwa nimehusika kwenye mauaji ya Geofrey Shambarai na kwamba nilikimbia na silaha iliyotumika kwa mauaji," anasimulia Kafunja.

Alipoulizwa ni jinsi gani alijisikia jaji alipotamka adhabu ya kifo dhidi yake, Kafunja alisema, "Ilikuwa ni jinamizi. Niliishiwa nguvu na nikashindwa kutembea huku nguo zangu zikilowa kutokana na jasho. Lilikuwa jambo zito na gumu hasa nilipofikiria kuwa maisha yangu yalikuwa yanaenda kukatizwa kwa jambo ambalo sikuwahi kuhusika," anasimulia Kafunja.

Kwa mjibu wa Kafunja, Desemba 1990 wahusika wa mauaji ya Geofrey Shambarai walikamatwa na polisi ambao walikiri kuhusika, lakini wakakana kabisa kumfahamu Kafunja.

Akisimulia hali ilivyo kwenye gereza la wanaosubiria kunyongwa, Kafunja anasema kila mlango unapofunguliwa alihisi ulikuwa umefika muda wa kumchukua kwenda kunyongwa na kila anapokaa anawaza namna kifo chake kitakavyokuwa, hali ambayo anasema ni ngumu kisaikolojia.

Licha ya wahusika kukamatwa, Kafunja hakuachiwa huru na kumlazimu kuchukua uamuzi mgumu ili kushinikiza kuachiliwa kwa kuwa moyoni mwake alijua hajafanya kosa hilo.

"Niliamua kugoma kula kwani niliona ni bora kufa kwa njaa kulikoni kufa kwa ajili ya mauaji ambayo sikuyafanya. Kifupi nilikata tamaa ya kuishi na kuamua nife tu na njaa kuliko kunyongwa," anasimulia Kafunja.

Ilipofikia siku ya saba ya mfungo wake, hali ilikuwa mbaya sana, jambo liliwafanya maofisa magereza wa Gereza la Isanga mkoani Dodoma alikokuwa amewekwa, kuomba wafungwa wengine wambebe na kumpeleka hospitalini ambako aliongezwa maji mwilini.

Licha ya kuendelea na matibabu, msimamo wake ulikuwa pale pale kwa kuwa alitaka rufani yake isikilizwe ili apate haki katika mahakama ya juu zaidi.

"Siku chache baadaye, nililetewa nyaraka za rufani kisha nikasafirishwa kwenda Dar es Salaam, Mwaka 2008 rufani yetu ilianza kusikilizwa mwezi wa tisa. Nilipofika mahakamani nilishtuka sana baada ya kuambiwa kuwa wakili wangu alikuwa amefariki dunia na nikaanza kuhisi kukata tamaa zaidi, lakini nikajuzwa kuwa yupo mwakilishi mwingine ambaye aliniuliza kama ninasali na nikajibu ndiyo," anasimulia Kafunja.

Baada ya ushahidi kuwasilishwa, Majaji wa Mahakama ya Rufani walishangaa kuona Kafunja alikuwa pale huku watuhumiwa halisi wakiwa wanajulikana na walimeshakiri kuhusika na mauaji hayo.

Anasema hakuamini baada ya mahakama hiyo kumwachia huru. "Naikumbuka Oktoba 10 mwaka 2008, niliachiwa huru na kwenda gerezani kuwaaga wenzangu niliokaa nao kwa muda mrefu, nikawatia moyo wasikate tamaa kwa kuwa inawezekana."

### APOTEZA FAMILIA, MALI

Kafunja anasema miaka 18 aliyokaa gerezani amepoteza familia yake na hadi sasa hajafanikiwa kuonana na mkewe na watoto wake wawili, yote ikiwa ni makosa yaliyofanywa na binadamu kumharibia maisha yake.

"Mara ya mwisho kumwona mke wangu na watoto ilikuwa ni mwaka 1993. Nilipotoka gerezani nikaenda nyumbani kwetu Ileje, nikakuta wazazi wangu walishafariki wakati nipo gerezani. Mimi nilikuwa ndiye mtoto wa pekee, nilikuta ardhi ya familia imeuzwa kwa madai nilikuwa nimeshanyongwa," anasema Kafunja.

### MAISHA YA SASA

Mzee huyo anasema alipotoka gerezani alipata mke mwingine wakawa wanaishi pamoja wakabarikiwa mtoto mmoja, lakini baadaye mke aliondoka kwenda kuishi kwingine na sasa amebaki na mwanawe mwenye umri wa miaka sita.

Anasema anaishi kwa kufanya vibarua sehemu mbalimbali, lakini hapati kipato kinachotosheleza na kuwaomba wasamaria wema kumsaidia kupata mahali pa kuishi kwa kuwa alipo sasa amehifadhiwa kwa mtu.

"Nilikwenda lililokuwa eneo langu la biashara nikakuta pamebaki kuwa jengo chakavu na mmiliki alishafariki dunia, ninatamani kurudi kwenye biashara, lakini sina mtaji wala uwezo wowote. Nilivyoachiwa niliambulia kupewa nauli ya Sh. 1,000 tu kunifikisha nyumbani," anasema.

### JAJI MSTAAFU ANENA

Ushauri wa Kafunja unakuja ikiwa ni miezi michache tangu Jaji mstaafu wa Mahakama ya Rufani, Engera Kileo, aishauri serikali kufuta adhabu ya kifo kutokana na kutompa nafasi mkosaji kujirekebisha na kwamba mahakama zinaweza kufanya au hufanya makosa wakati mwingine.

Anasema ipo hatari ya kufanya makosa ya kibinadamu yanayoweza kusababisha wasio na hatia kunyongwa.

Jaji huyo anayejulikana kwa msimamo wake wa kupinga matumizi ya adhabu ya kifo, alisema ipo haja serikali kutoa kifungo cha maisha kama mbadala wa adhabu ya kifo, ili kukwepa kufanya makosa ya watu wasio na hatia kulipia makosa ambayo hawajafanya.

### MWANASHERIA ANENA

Wakili Fulgence Massawe anasema mfumo wa sheria kwenye makosa kama hayo haupo wazi kwa mtu kudai fidia na una utaratibu mgumu, unapodai lazima useme ni nani kakushtaki.

"Marekani wana mfumo wa kulipa fidia, wanalipa hadi dola milioni moja kwa mtu aliyehukumiwa kimakosa wanalipa kidogo kidogo, wanajua madhara ya adhabu hiyo ni kubwa, lakini mfumo wetu hauna namna ya kutoa fidia kwa huyu mtu ameteseka muda mrefu," alisema.

Massawe anasema siyo kwenye makosa hayo tu bali yenye adhabu kubwa kesi zinachukua muda mrefu hata miaka mitano, saba na halafu inaonekana mtu hana hatia anaachiwa, na hakuna mfumo rasmi wa kudai haki ya kupotezewa muda.

Tanzania bado ina sheria ya unyongaji na mtu wa mwisho kunyongwa nchini ilikuwa mwaka 1994. Takwimu kutoka Kamisheni ya Haki za Binadamu Tanzania inaonesha kuwa kati ya watu 2,478 waliohukumiwa kunyongwa hadi kufa kufikia mwaka 2010, ni watu 232 waliotekelezewa hukumu hiyo sawa na asilimia 9.39.

**Ukihitaji kumsaidia Tete Kafunja tafadhali wasiliana naye kwa namba hizi 0713-332-794 au 0783-177-480.**

# ‘Mbu wamejenga usugu kemikali za kuwadhibiti’

Na Grace Gurisha

KIWANDA cha Uzalishaji wa Viuadudu Tanzania (TBPL) kimesema mbu wamejenga usugu dhidi ya kemikali, jambo linalofanya wazoee na hivyo kemikali hizo kutowaua.

Kimesema pia mbu wamebadilisha tabia ya kung’ata, badala ya usiku, anang’ata jioni na asubuhi na muda unaotumika mtu kuwa kwenye chandarua ni mdogo kutokana na tabia zao kubadilika.

Meneja Uzalishaji wa kiwanda hicho, Gasper Philip, alisema hayo katika maonesho ya tatu Viwanda, Biashara na Uwekezaji yanayofanyika Kibaha, mkoani Pwani.

Alisema dawa inaweza kunyunyizwa na mbu wachache wakafa wengine wakaanguka, baadaye wakapata fahamu na kuamka, kwenye mfumo wao wa vinasaba umeshajenga usugu ambao kemikali haziwezi kuwaathiri tena.

Alisema kutokana na tabia hizo zao kubadilika aliyekuwa mwenezaji mkubwa wa malaria (Anophelese) sasa ameibuka mwingine Anofelesi aladiesisi, ambaye haishi ndani ya nyumba mara nyingi.

“Kwa hiyo teknolojia ya viuadudu inatusaidia kupambana na chanzo cha mbu ambacho ni viluilui kwa sababu haviwezi kubadilisha tabia, ni kama samaki maisha yake yote ni kwenye maji hadi abadilike awe mbu baadaye awe mbu kamili,” alisema Philip.

Alisema njia pekee ya kumwangamiza ni kuua mayai na viluilui vyote na kuwa na uhakika wa kumaliza uzao wa mbu.

“Huyu mbu anayeruka kwa siku 21 hadi 30 atakufa au tutaweza kupambana naye kwa njia nyingine ambazo zinatumika kama unyunyuziaji wa dawa ukoko pamoja na vyandarua, lakini tunakuwa tumeshauangamiza uzao wa mbu,” alisema.

Alisema lengo kubwa la viuadudu ni katika mapambano dhidi ya malaria na magonjwa mengine yanayosambazwa na mbu kwa sababu haviui viluivuli vya malaria pekee pia vya mbu wanaosambaza magonjwa mengine.

“Magonjwa kama dengue, matende na mabusha, zika, chipungunya na mengine yanayosambazwa na mbu, hivyo tunakuwa tumepambana na mbu kwa kuangamiza magonjwa ambayo yalikuwa yanatusumbua katika jamii kwa kipindi cha muda mrefu,” alisema.

Alisema viuadudu ni teknolojia salama, imeanza miaka mingi, ilikuwa inatumika kemikali kuangamiza mazalia ya mbu pamoja na mbu, lakini baadaye iligundulika zinaleta madhara kwa viumbe vingine pamoja binadamu na mazingira.

Pia alisema kiwanda hicho kilianzishwa na serikali mahusus kwa ajili ya kuondoa ugonjwa wa malaria, kinazalisha bidhaa za kibailojia zisizotumia kemikali bali viumbe hai wanaoitwa bakteria ambao ni rafiki na wamethibitishwa kisayansi.

# Kampeni kuzuia ebola nyumba kwa nyumba

Na Mary Geofrey, KAGERA

KAMPENI ya kudhibiti tishio la mlipuko wa ugonjwa wa ebola nchini katika Mkoa wa Kagera imeanza kufanyika nyumba kwa nyumba, mtaa kwa mtaa na nyumba za kulala wageni ili kufikisha elimu kwa wananchi.

Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya Kinga Kitengo cha Elimu ya Afya kwa Umma, Dk. Amma Kasangala, jana alianza kampeni hiyo akiwa ameambatana na maofisa wa afya na viongozi wa mtaa kutoa elimu hiyo wilayani Misenyi mkoani humo.

Akiwa katika soko la Bunazi lililoko Wilaya ya Misenyi, Dk. Amma alisema kampeni hiyo ina ushawishi mkubwa kwa sababu wanawafikia walioko kwenye shughuli zao na nyumbani.

“Hakuna kulala, serikali haitalala hadi hapo nchi jirani itakapotuhakikishia imeudhibiti ugonjwa huu.

“Tutaendelea na kasi hii, tutashambulia kila mahali, nyumba za wageni chumba kwa chumba, wageni wanaingia na kutoka wapate elimu ya kujikinga na ebola na tutashambulia mitaani, nyumba hadi nyumba na mtu hadi mtu,” alisisitiza.

Dk. Amma alisema tayari wametoa maagizo kwenye nyumba zote za wageni kuzingatia afua za afya kwa kuweka sabuni, maji tiririka na kuwapima joto wageni wote wanaoingia.

“Tumewaelimisha na kama kuna mgeni anahisiwa, basi wapige simu namba 199 ambayo ni bure na kutoa taarifa na wataalamu wetu watachukua hatua kwa haraka,” alisema Dk. Amma.

Alisema kampeni hiyo inaendelea pia kwa kutumia magari ya matangazo kuzunguka katika halmashauri zote za mkoa huo, mipakani na maeneo ambako wananchi hawawezi kupata taarifa kwa urahisi.

Dk. Amma aligawa vipeperushi vyenye ujumbe mbalimbali za dalili za ugonjwa wa ebola na namna ya kujikinga.

Akiwa katika kampeni hiyo, aligawa vizibao vyenye ujumbe wa kujikinga na ebola kwa madereva wa bodaboda katika soko la Bunazi, wilayani Misenyi.

Aligawa pia vipeperushi na flashi zenye ujumbe maalum wa kujikinga na ugonjwa huo kwa wafanyabiashara na wananchi waliofika kununua mahitaji katika soko hilo.

Dk. Amma alisema serikali imeendea kuweka nguvu kubwa mkoani humo kutokana na mkoa huo kuingiliana kwa karibu na nchi ya Uganda.


MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA

Imethibitishwa na ISO 9001: 2015

TAARIFA KWA UMMA

ONYO KWA WATUMIAJI WA NAMBA ZA USAJILI WA MAGARI ZISIZOTAMBULIWA NA TRA

Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) imebaini uwepo wa magari barabarani yaliyobandikwa na kutumia namba ambazo hazijatolewa na TRA ama Taasisi nyingine za Serikali ambazo zimepewa jukumu hilo kisheria. Aidha, kumekuwepo na matumizi ya Vibao *(Number Plates)* vya namba vyenye rangi zisizotambulika kisheria vinavyowekwa mbele na nyuma ya vyombo vya moto.

Hivyo, wamiliki wa vyombo vya moto na umma kwa ujumla wanatangaziwa kwamba, utengenezaji na matumizi ya vibati hivyo ni kosa kisheria kama inavyoelezwa kwenye **Kifungu cha 8** cha **Sheria ya Usalama Barabarani** *(The Road Traffic Act, 1973)*. Hatua kali za kisheria zitachukuliwa kwa yeyote **anayekiuka sheria hii** ikiwa ni pamoja na **kutaifisha chombo cha moto husika**.

Kwa maelezo zaidi, tembelea ofisi za TRA zilizopo karibu au piga simu bure kwa Kituo chetu cha Huduma kwa Mlipakodi kupitia simu nambari **0800-780078** au **0800-750075** au **0800-110016** au WhatsApp **0744-233 333** barua pepe huduma@tra.go.tz.




*“Pamoja Tunajenga Taifa Letu”*

Imetolewa na;
**IDARA YA HUDUMA NA ELIMU KWA MLIPAKODI**

217080802

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Wawakilishi michuano CAF inawezekana 90 za mwisho

**WAWAKILISHI** wa Tanzania kwenye michuano ya kimataifa, Yanga, Azam na Kipanga FC, Jumamosi iliyopita walipata matokeo yasiyofurahisha katika mechi zao za kwanza za Raundi ya Kwanza ya Ligi ya Mabingwa na Kombe la Shirikisho Afrika wakiwa katika viwanja tofauti ndani na nje ya nchi.

Yanga inayoiwakilisha nchi kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika, iliikaribisha Al Hilal ya Sudan katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam na mechi kumalizika kwa sare ya bao 1-1, hivyo inahitaji ushindi ama sare yoyote ya kuanzia mabao mawili ili kutinga hatua ya makundi.

Kwa upande wa Azam FC, ikiwa ugenini nchini Libya, ilikumbana na kipigo kikubwa cha mabao 3-0 dhidi ya Al Akhdar kwenye mechi ya kwanza ya Kombe la Shirikisho Afrika, hivyo kuwa na mlima mrefu wa 'kupindua meza' katika mchezo wa marudiano mwishoni mwa wiki hii utakaopigwa Uwanja wa Azam Complex uliopo Chamazi, Dar es Salaam. Ushindi wa mabao 4-0 na kuendelea, ndio utakaoiwezesha Azam kusonga mbele kwenye michuano hiyo, wakati Kipanga FC ya Zanzibar iliyoikaribisha Club Africain ya Tunisia katika Uwanja wa Amaan visiwani humo, yenyewe ikilazimishwa sare tasa, hivyo ushindi wowote ama sare yoyote ya mabao itaiwezesha kusonga mbele kwenye hatua inayofuata ya kinyang'anyiro hicho.

Wawakilishi wengine kwenye michuano hiyo ya kimataifa kwa ngazi ya klabu ni Simba, ambayo jana jioni ilikuwa ugenini nchini Angola ikipepetana dhidi ya Primeiro de Agosto kwenye mechi ya Raundi ya Kwanza ya Ligi ya Mabingwa Afrika kabla ya kurudiana Jumapili wiki hii katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Hivyo, ingawa matokeo kwa Yanga, Azam na Kipanga hayakuwa rafiki sana, bado tunaamini hakuna kinachoshindikana katika mchezo wa soka na lolote linaweza kutokea kwa wawakilishi wetu hao kupata matokeo chanya zaidi na kusonga mbele.

Tunatambua mashabiki wengi hususan ni wa timu hizo na Watanzania kwa ujumla, wamekata tamaa wakiamini ni vigumu hususan kwa Yanga na Kipanga kwenda ugenini na kupata matokeo, lakini kwa Azam kuweza kupindua meza kwa kushinda zaidi ya mabao matatu katika mechi ya marudiano hapa nchini.

Lakini sisi tunaamini, kinachotakiwa ni maandalizi makubwa ndani ya wiki hii, kwa makocha kutazama wapi walifanya makosa dakika 90 za kwanza na kuyatafutia ufumbuzi lakini wakitumia muda vizuri kwa kuwajenga wachezaji kisaikolojia kwa kuwaaminisha inawezekana kupata matokeo ugenini na hata kwa Azam kushinda nyumbani kwa idadi kubwa ya mabao.

Kikubwa kinachotakiwa ni kuwaonya wachezaji kutobeba kile kinachojadiliwa na mashabiki kwenye mitandao ya kijamii na vyombo vingine vya habari, ambavyo vinawakatisha tamaa wakiamini kwamba tayari timu zao zimeshatolewa.

Nipashe tunatambua mpira wa miguu una matokeo matatu ambayo yanaweza kupatikana popote iwe uwanja wa nyumbani ama ugenini ambayo ni kushinda, kushindwa na sare, lakini ni mchezo wa makosa na anayekosea huadhibiwa.


Kwa mantiki hiyo, kama Al Hilal iliweza kupata sare Uwanja wa Benjamin Mkapa, hata Yanga ikijipanga na kuweka kando kelele na vifijo vya mashabiki wa wapinzani wao ugenini, inawezekana kabisa kupata matokeo na kutinga hatua ya makundi.

Lakini, kwa Azam FC, hilo linawezekana kwani itakuwa nyumbani dhidi ya Al Akhdar na yenyewe ikifaidika na mashabiki wake na uzoefu wao mkubwa katika uwanja wake wa Azam Complex ukiwabeba, hali kadhalika kwa Kipanga ambayo ililazimishwa sare tasa dhidi ya Club Africain, kwani itakuwa na faida zaidi endapo ikijitahidi kupata bao la ugenini kwa kuwa sare yoyote itaifanya kusonga mbele na kusubiri kupangiwa timu moja kutoka zitakazotolewa kwenye raundi ya Kwanza ya Ligi ya Mabingwa Afrika ili kucheza mechi ya mtoano kuwania kufuzu hatua ya makundi ya Kombe la Shirikisho.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:

**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Adam Fungamwango

## Muungwana Lazima Nilonge

# Yanga, Azam siyo mwisho hadi ifike mwisho

**ILIKUWA** mwaka 1979, Simba ikiwa inaiwakilisha nchi kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika, wakati huo ikiitwa Klabu Bingwa Afrika.

Ilipangwa kucheza dhidi ya Mufulira Wanderers ya Zambia, ambayo ilikuwa kwenye kiwango cha hali ya juu wakati huo kimpira kuanzia timu yenyewe pamoja na kikosi chao cha timu ya taifa.

Ikiwa na wachezaji wengi wanaochezea timu ya taifa, timu hiyo ilifika nchini Tanzania kucheza na Simba Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam (sasa Uhuru).

Kwenye mechi hiyo Simba ilipokea kipigo cha mabao 4-0 na ilitakiwa kwenda nchini Zambia kwa ajili ya mechi ya marudiano wiki mbili zijazo. Ikumbukwe kuwa wakati huo michuano ya kimataifa ilichezwa kila baada ya wiki mbili, mechi ya nyumbani na ugenini kutokana na miundombinu na usafiri wakati ule.

Kila mmoja alikata tamaa. Siyo viongozi, wanachama na mashabiki wa Simba, lakini hata watangazaji wa Redio Tanzania Dar es Salaam (RTD) ambao walitakiwa kwenda kutangaza mechi hiyo moja kwa moja, hawakujisumbua.

Ni kama kila kitu kilisambaratika. Hata wachezaji walikata tamaa, baadhi yao wakaondoka kwenda nchini Oman kucheza soka la kulipwa.

Siku zilipokaribia, viongozi wachache wa klabu walikusanya wachezaji wakawaweka kambini kwa ajili ya mechi ya marudiano. Hakuna aliyeingia tena gharama ya usafiri wa ndege. Badala yake serikali iligharamia kwa kutoa behewa moja la treni ya TAZARA kwenda nchini Zambia.

Timu ilisafiri kinyonge na wala hakuna aliyeitilia maanani. Mechi ya marudiano ilichezwa mgeni rasmi alikuwa ni Rais wa Kwanza wa nchini hiyo, Kenneth Kaunda.

Kwa namba ambayo haikutarajiwa Simba iliibuka na ushindi mnono wa mabao 5-0, yaliyofungwa na wachezaji wawili tu, Thuwein Ally akifunga 'hat-trick' na George Kulagwa akipachika mawili.

Kaunda hakuamini na ilibidi aulize kama wachezaji wale wa Simba ndiyo wale wale waliocheza Tanzania au kuna mamluki. Akawaambia ndiyo hao hao. Akaondoka uwanjani wakati bado Simba ikiongoza mabao 4-0.

Ushindi huo uliifanya Simba kusonga mbele ya michuano hiyo kwa namna iliyoshangaza Afrika nzima kiasi kwamba hadi leo hii mechi hiyo ipo kwenye moja kati ya matukio ya ajabu na ya kukumbukwa kwenye soka la Afrika na Shirikisho la Soka Afrika (CAF), huposti tukio hilo kila mwaka ikifika tarehe hiyo.

Nchini Tanzania kwa sababu hakukuwa na teknolojia kama sasa hakuna aliyefahamu hilo mpaka matokeo ya mechi hiyo yalipotangazwa saa mbili usiku kwenye taarifa ya habari na kuifanya nchi nzima kuzizima.

Nimeamua kuanza na tukio hili lililotokea miaka 43 iliyopita kuzikumbusha klabu za Tanzania kuwa kwenye soka lolote linaweza kutokea sehemu yoyote.

Juzi Yanga imetoka sare ya bao 1-1 dhidi ya Al Hilal ya Sudan kwenye mechi ya Ligi ya Mabingwa Afrika, huku Azam ikifungwa mabao 3-0 kwenye mechi ya Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya Al Akhdar.

Nilivyofuatilia sehemu mbalimbali za vijiwe vya soka na kwenye mitandao ya kijamii ni kama mashabiki wameshaanza kukata tamaa.

Wanaona ni kama Yanga ambayo inakwenda kucheza ugenini, Khartoum sehemu ambayo ni ngumu sana kutokana na mazingira pamoja na aina ya ushangiliaji wa mashabiki wao.

Wingi wa mabao ambayo Azam imeruhusu inawapa shaka mashabiki kuamini kuwa timu hiyo inaweza kupindua mechi kwa ushindi wa mabao 4-0 kwenye Uwanja wa Azam Complex.

Kwenye soka lolote linawezekana kama ambavyo mfano huo nilioutoa na unavyojieleza. Kama Simba ilikwenda kushinda ugenini mabao 5-0, kwa nini Azam ishindwe kupata mabao 4-0 nyumbani?

Kwa nini Yanga ishindwe kupata ushindi ugenini dhidi ya Al Hilal? Kila kitu kinawezekana kama mikakati itawekwa na timu zikajipanga. Pamoja kuwa na mashabiki wenye vurugu, lakini kama timu ikiwa bora, Wasudan wanafungika kwao.

Simba iliifunga Al Merreikh nyumbani kwao bao 1-0 mwaka 1994 kwenye Klabu Bingwa Afrika na kusonga mbele, na mwaka huo huo, iliifunga timu hiyo hiyo mabao 2-1 kwenye Kombe la Kagame wakati huo likiitwa Kombe la Afrika Mashariki na Kati lililochezwa nchini humo, ingawa mashabiki wao walivamia uwanja na kuwapiga hadi kuwajeruhi wachezaji wa Simba kiasi cha baadhi kulazwa hospitalini.

Hiyo ni kuonyesha timu ya Tanzania ina uwezo wa kuifunga timu ya Sudan nyumbani kwao kwa sababu imeshatokea huko nyuma na Yanga isihofu kwa hilo.

Kinachotakiwa sasa ni mabenchi ya ufundi kuzitengeneza timu hizo kimbinu na wachezaji kuwa na utayari kwa kwenda kupambana na kukabiliana na mazingira magumu ya kucheza ugenini.

Mashabiki wa soka watulie, kila kitu kinawezekana, haiwezekani ikawa mwisho kabla hujafika mwisho.

HABARI KITAIFA

## RITA yatoa vyeti kuzaliwa maonyesho ya uwekezaji

**Na Mwandishi Wetu**

WAKALA wa Usajili, Ufilisi na Udhamini (RITA) umesajili na kutoa vyeti vya kuzaliwa kwa wananchi wote waliozaliwa ndani ya mipaka ya Tanzania Bara katika maonyesho ya uwekezaji wa viwanda Mkoa wa Pwani.

Wananchi hao wameishukuru serikali kupitia RITA kwa kuwasogezea huduma za usajili na vyeti vya kuzaliwa.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti kwenye maonyesho hayo yanayoendelea kwa siku tano wilayani Kibaha, wananchi hao akiwamo Salum Moto, walisema wametumia muda mfupi kusajiliwa na kupatiwa vyeti vya watoto wao.

Moto alisema aliposikia huduma hiyo inatolewa katika maonyesho hayo, aliwasiliana na baadhi ya ndugu zake ili wafike na walifanikiwa kwa haraka na muda mfupi.

Ofisa Usajili Wilaya ya Kibaha, George Chuwa, alisema mwitikio umekuwa mkubwa kutokana na wananchi wengi kujitokeza kupatiwa huduma.

"Ninashukuru mpaka sasa watu zaidi ya 257 wamesajiliwa na kupatiwa vyeti vya kuzaliwa kupitia maonyesho haya.

"Mbali na kutoa huduma ya usajili na kutoa vyeti vya kuzaliwa, tumeendelea kutoa elimu kuhusu huduma zetu kama usajili wa ndoa na talaka, umuhimu wa kuandika na kuhifadhi wosia na usajili wa bodi ya wadhamini," alisema.

Aliongeza kuwa kuandika wosia kutasaidia kupunguza migogoro ndani ya familia endapo wazazi, walezi watafariki dunia.

**Ofisa Usajili Wilaya ya Kibaha, George Chuwa, alisema mwitikio umekuwa mkubwa kutokana na wananchi wengi kujitokeza kupatiwa huduma.**



Mkurugenzi wa Masoko ya Kifedha Benki ya Absa Tanzania, Esther Maruma (wa pili kushoto), akizungumza na baadhi ya wateja wa tawi la benki hiyo mkoani Morogoro kuhusu huduma na bidhaa zitolewazo na Absa, ikiwa ni maadhimisho ya Wiki ya Huduma kwa Wateja, Morogoro, mwishoni mwa wiki. Kushoto ni Meneja wa benki hiyo, Godfrey Chilewa. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Chuo kikuu chataka wajasiriamali wanufaike NSSF na bima ya afya

**Na Mwandishi Wetu**

WATAFITI kutoka Chuo Kikuu cha Mzumbe wamewataka wajasiriamali wadogo kuhakikisha wananufaika na huduma zitolewazo na mifuko ya hifadhi ya jamii, bima za afya na taasisi za fedha kwa kuwa kuna utaratibu mzuri uliowekwa kwa ajili yao.

Walitoa rai hiyo mwishoni mwa wiki mkoani Dar es Salaam wakati wa warsha ya kurejesha matokeo ya utafiti kwa wadau, wakiongozwa na Dk. Godbertha Kinyondo.

Warsha hiyo iliwakutanisha wajasiriamali wadogo zaidi ya 70 kutoka kata za Magomeni, Mburahati, Ndugombi Magomeni, Tandale na Manzese.

Akizungumza wakati wa warsha hiyo, Dk. Kinyondo alisema walifanya utafiti kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Nairobi na Chuo Kikuu cha Roskilde cha Denmark, wakilenga wafanyakazi katika sekta za ujenzi, usafirishaji na wajasiriamali wadogo katika miji ya Dar es Salaam, Dodoma, Nairobi na Kisumu.

Dk. Kinyondo alisema utafiti huo ulifanyika kuanzia mwaka 2017 hadi 2021 katika nchi za Tanzania na Kenya kwa ufadhili wa Shirika la Kimataifa la Maendeleo la Denmark (DANIDA).

Dk. Kinyondo alisema pamoja na ukweli kwamba kuna matatizo kadhaa kwa upande wa sekta isiyo rasmi, hivi karibuni mifuko mingi ya hifadhi ya jamii imekuwa na ubunifu na mipango mizuri ya kuhakikisha hata wasio katika sekta rasmi wanafaidika na huduma zao.

Alisema katika utafiti huo, waliwahoji wafanyakazi wa mabasi ya usafirishaji 250 na madereva pikipiki 158 kwa Tanzania.

Alisema pia waliwahoji wajenzi 212 wakihusisha miji ya Dar es Salaam na Dodoma na kwa upande wa Kenya utafiti ulihusisha wafanyakazi 200 katika sekta ya usafirishaji.

Dk. Kinyondo alisema matokeo ya utafiti huo yalionyesha wengi wa wafanyakazi hao hawajajisajili katika mifuko ya hifadhi ya jamii licha ya kuwa wanatambua kuwapo kwa mifuko hiyo.

Alisema ili kuhamasisha makundi hayo kujiunga na mifuko hiyo, timu hiyo ya utafiti imebuni nguo maalum zinazoakisi mwanga zikionyesha orodha ya mifuko ya hifadhi ya jamii, bima na taasisi zinazotoa huduma za fedha na mafunzo pamoja na mawasiliano ya simu. "Vikoti hivyo vinatarajiwa kusambazwa kwa wadau katika sekta isiyo rasmi zaidi ya 1,000 hasa katika majiji ya Dar es Salaam na Dodoma," alisema.

Dk. Kinyondo alisema tayari wameshakutana na madereva pikipiki na wafanyakazi wa daladala na sasa wana mkakati wa kukutana na wajenzi.

"Siyo suala la kuja na machapisho ya utafiti tu, tungependa kuona matokeo halisi ya utafiti huu kwa faida ya wengi," alisema.

Dk. Aloyce Gervas kutoka Chuo Kikuu cha Mzumbe alisema utafiti huo pia ulilenga kuangalia iwapo wafanyakazi wa sekta hizo wamejiunga na mifuko ya hifadhi ya jamii.

Alisema pia ulihusisha wadau kama polisi, mifuko ya hifadhi ya jamii na vyuo vya ufundi stadi, lengo kuu likiwa ni kuangalia kwa pamoja namna bora ya kuimarisha huduma za jamii kwa sekta isiyo rasmi.

Mmoja wa wajasiriamali katika Soko la Mburahati, Asha Hassan alisema: "Nilikuwa gizani, sasa nina mwanga. Tunaomba watafiti waendelee kutoa mwanga kwa wajasiriamali wengi zaidi. Nitafundisha wenzangu."

Naibu Katibu Mkuu wa Chama cha Wafanyakazi Wasafirishaji kwa Njia ya Barabara Tanzania (TAROTU), Amani Mwinyimvua aliwataka wanachama wa chama hicho kuhakikisha wanashiriki katika warsha za mafunzo mara kwa mara.

## KABWELA



# NMB yaongeza kiwango mkupuo mmoja wa mkopo hadi Bil. 250/-

**Na Mwandishi Wetu**

UFANISI mkubwa wa kiutendaji ambao Benki ya NMB imeupata miaka ya hivi karibuni, umeiwezesha taasisi hiyo kinara wa huduma za kifedha nchini kuimarika kiufadhili.

Viongozi wake waandamizi wamebainisha kuwa miongoni mwa matokeo ya kufanikiwa huko kifedha ni kuiwezesha benki hiyo kuongeza kiasi cha mkupuo mmoja wa mkopo kwenye miaka ya hivi karibuni.

Akizungumza jijini Dar es Salaam wakati wa hafla ya Mtandao wa Wateja Wakubwa na Wanaochipukia (BEN) wa NMB mwishoni mwa wiki, Mkaguzi Mkuu wa Ndani wa benki hiyo, Benedicto Baragomwa, alisema kiwango kikubwa cha mkupuo mmoja wa mkopo sasa kimefikia Sh. bilioni 250.

Kiasi hicho ni kikomo cha kikanuni ambacho benki hiyo inaweza kumkopesha mteja mmoja kwa mkupuo.

Wateja wa NMB na viongozi wa Jiji na Mkoa wa Dar es Salaam walioudhuria mkutano huo, walionyesha kuvutiwa na hilo, wakiipongeza NMB kwa hatua hiyo kubwa kiufadhili na kusema ni matokea ya uwezo wake kiubunifu na uwekezaji wa kizalendo inaoufanya nchini.

"Sisi ndiyo mkopeshaji mkubwa mwenye viwango vya faida ambavyo havina mpinzani sokoni na aina tofauti tofauti za huduma za mikopo kama ile ya dharura inayopatikana papo kwa papo kidijitali kwa kutumia simu za mkononi," Baragomwa aliwaambia washiriki 100 wa mkutano wa BEN wa Mkoa wa Dar es Salaam.

Akizungumza katika hafla ya aina hiyo iliyofanyika jijini Mbeya, Mkuu wa Idara ya Mikopo wa NMB, Demetus Kamguna alisema kwa sasa benki hiyo inajivunia kuwa na mizania mipana yenye rasilimali zenye thamani ya takribani Sh. trilioni tisa pamoja na amana zipatazo Sh. trilioni 6.6.

Alisema kukua kwa mali zake zote kumesaidia kupanua kiasi cha mtaji wake hadi zaidi ya Sh. trilioni moja na kupelekea kuzidisha ukomo wa mkupuo mmoja kwa kila mkopaji mwenye sifa.

"NMB pia tunatoa mikopo kadri ya uwezo wa mfanyabiashara, tukiwa na uwezo wa kutoa hadi Sh. bilioni 250 kwa mkopaji mmoja," kiongozi huyo mwandamizi alisema kwenye mchapalo huo wa kujadili masuala muhimu na wateja wake wakubwa wa mkoani Mbeya uliofunguliwa rasmi ya Mkuu wa Mkoa ya Mbeya, Juma Homera.

Akielezea kiwango kipya cha mkupuo wa juu wa mkopo kwa kila mteja, Mkuu wa Idara ya Biashara wa NMB, Alex Mgeni alimwambia mwandishi wa habari kuwa maendeleo ya ukopeshaji yaliyopatikana, ni matokea chanya ya faida kubwa ambazo NMB imekuwa ikipata miaka ya karibuni.

Pamoja na mambo mengine mengi, Mgeni alisema faida za NMB zimekuwa zikitumika kuimarisha utendaji na uendeshaji wa benki hiyo, pia kuzatiti mtaji wake.

Mgeni alisema matokeo ya uwekezaji huo ni pamoja na kuongeza kiwango cha NMB kuwakopesha wateja wake.

"Kimsingi, mtaji wetu sasa ni Sh. trilioni 1.2 ambazo zinapelekea mkupuo mmoja wa mikopo yetu kufikia hadi Sh. bilioni 300 kwa kuzingatia kanuni ya Benki Kuu (BoT) ya benki kukopesha asilimia 25 ya mtaji wake," Mgeni alisema.

Katika hotuba yake ya ufunguzi, Mkuu wa Mkoa wa Mbeya aliitaka Benki ya NMB kuendelea kuwaunga mmono wakulima kwa kuwa ni sekta inayokua kwa kasi sana kwa sasa, huku akisisitiza kuendelea kuweka nguvu kubwa katika ufadhili wa kilimo cha maparachichi, mchele na pareto.

Katika hafla ya jijini Dar es Salaam, Mkuu wa Wilaya ya Ilala, Ludigija, aliimwagia sifa NMB kwa kuja na wazo la BEN, akisema si tu ni muhimu kwa ajili ya kupata mrejesho kutoka kwa wateja, bali pia kusaidia kuchangia mawazo ya sera za kitaifa.

Meya wa Ilala, Omary Kumbilamoto alisema NMB sasa ni mshirika wa kimkakati wa maendeleo ya kibiashara wa kitaifa ambaye anaisaidia serikali kuboresha upatikanaji wa huduma za kijamii.

NMB ilianzisha mtandao wa BEN mwaka 2014 ikilenga kuitumia mikutano yake kama jukwaa la kukutana na wateja wake wenye mzunguko wa fedha kuanzia Sh. bilioni tano kwa mwaka kwa ajili ya kubadilishana wazo na uzoefu wa kibiashara.

Mpango huo ulilenga mikoa mikubwa na inayoongoza kiuzalishaji na mpaka sasa mtandao huu uko katika mikoa saba ambako ina washirika zaidi ya 1,000. Mikoa hiyo ni Dar es Salaam, Dodoma, Morogoro, Kilimanjaro, Mwanza, Arusha na Mbeya.



Mtafiti Dk. Godbertha Kinyondo wa Chuo Kikuu cha Mzumbe akisisitiza jambo katika warsha ya kutoa mrejesho wa matokeo ya utafiti kwa wadau mwishoni mwa wiki jijini Dar es Salaam. Watafiti hao walikutana na wajasiriamali wadogo zaidi ya 70 kutoka kata mbalimbali ili kutoa mrejesho wa utafiti wa miaka mitano kuhusu sekta isiyo rasmi na hifadhi za jamii. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## NBAA kutoa bure elimu kuandaa hesabu za fedha

**Na Joseph Mwendapole**

BODI ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu (NBAA), imeandaa maonesho ya huduma za kihasibu ikiwa sehemu ya shamra shamra za maadhimisho ya miaka 50 tangu kuanzishwa kwake.

Maonesho hayo ya siku tatu yatakayofanyika mwezi Novemba 10 hadi 12 kwenye viwanja vya Mnazi Mmoja jijini Dar es Salaam, yatahudhuriwa na mashirika na taasisi mbalimbali za uhasibu na ukaguzi.

Mkurugenzi Mtendaji wa NBAA, CPA, Pius Maneno, alisema hayo wakati akizungumzia maonesho hayo yaliyobeba kaulimbiu ya 'Utaalamu, Maslahi ya Umma na Uendelevu'.

Alisema bodi hiyo imeazimia kufanya shughuli mbalimbali za kusaidia jamii yakiwamo maonesho hayo ya kihasibu kwa watakaofika kupewa elimu hiyo.

Alisema shughuli hizo za maadhimisho zilianza Agosti mwaka huu na zinatarajiwa kuhitikishwa Novemba 30, Bunju nje kidogo ya Jiji la Dar es Salaam.

Alisema lengo la maonesho hayo ni kuwaelimisha wafanyabiashara na wananchi jinsi ya kuandaa taarifa za hesabu za fedha, kodi na kuwasaidia kwenye nyanja mbalimbali zinazohusu uhasibu na ukaguzi.

"Kwenye kniliki hiyo NBAA itaungana na wadau wake mbalimbali kama vile makampuni ya uhasibu na ukaguzi, Mamlaka ya Mapato TRA, Mamlaka ya Bima na mengine katika kutoa huduma hiyo," alisema.

Alisema katika miaka yake 50, NBAA imefanya mambo mengi makubwa ikiwamo kusajili wahasibu na wakaguzi na mpaka sasa waliofaulu mitihani ya bodi hiyo wanafikia 26,000 na kati ya hao, 12, 000 walifaulu katika ngazi ya CPA na 14,400 katika ngazi ya watunza vitabu vya hesabu.

# Barrick Bulyanhulu yatoa mashine kukabili bakteria

**Na Mwandoshi Wetu,**
KAHAMA

MGODI ya Barrick Bulyanhulu umetoa msaada wa mashine mbili za kuzuia kusambaa bakteria hatarishi kwenye maabara (Biohazard Safety Cabinet) kwa Hospitali ya Manispaa ya Kahama na Kituo cha Afya Bugarama, Halmashauri ya Msalala mkoani Shinyanga.

Vifaa hivyo viona thamani ya Sh. milioni 30 ikiwa ni sehemu ya mchango wa kampuni hiyo kuunga mkono jitihada za serikali katika kuboresha huduma za afya nchini.

Katika hafla ya kukabidhi msaada huo mwishoni mwa wiki kwenye Hospitali ya Manispaa ya Kahama, Kaimu Meneja Mkuu wa Mgodi Bulyanhulu, Josephat John, alikabidhi msaada huo kwa Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Festo Kiswaga, vifaa hivyo vya kusaidia katika maabara.

Akizungumza jana katika hafla hiyo, John alisema "Tunajivunia kutoa vifaa hivi maalum ili kuimarisha miundombinu ya matibabu katika jamii zinazozunguka migodi ya kampuni na huu ni mwendelezo wa jitihada za kampuni kuunga mkono jitihada za serikali za kuboresha huduma katika sekta ya afya nchini."

Akipokea mashine hizo, Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Kiswaga, aliishukuru kampuni hiyo kwa kutoa ushirikiano kwa serikali na kuunga mkono jitihada za kuboresha afya kwa jamii.

"Barrick hamjawa nyuma, mmekuwa mstari wa mbele kila wakati, serikali inapokuwa na jambo, mmekuwa mkifungua mikono yenu. Asanteni sana kwa kuiunga mkono serikali kwa jambo hili jema la kuleta vifaa hivi vya kisasa ambavyo vitasaidia kuboresha huduma za maabara katika hospitali zetu," alipongeza Kiswaga.

Alitoa wito kwa wananchi kutunza afya zao huku akiutaka uongozi wa Hospitali ya Manispaa ya Kahama na Kituo cha Afya Bugarama kuhakikisha wanasimamia vyema matumizi na utunzaji wa vifaa hivyo.

Diwani wa Bugarama, Prisca Msoma aliyemwakilisha Mwenyekiti wa Halmashauri ya Msalala, alipongeza kampuni ya Barrick kwa jitihada ambazo imekuwa ikifanya kuunga mkono jitihada za serikali za kukabiliana na kero mbalimbali kwenye jamii ikiwamo kuboresha sekta ya afya.

## Bilioni 1.8/- kujenga madarasa elimu bure

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

HALMASHAURI ya Manispaa ya Morogoro imepokea Sh. bilioni 1.8 za ujenzi wa vyumba vya madarasa ya kidato cha kwanza mwaka 2023 na matumizi ya elimu bila malipo.

Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini wa Manispaa ya Morogoro, Lilian Henerico, alisema fedha za ruzuku Sh. 1,870,115,241 zimepokewa Septemba mwaka huu, kutoka serikali kuu kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vya madarasa.

Alisema fedha hizo zinahusisha elimu bila malipo kwa shule za msingi na sekondari na matumizi ya kawaida.

Henerico alisema Sh. bilioni 1.6 zitatumika kwa ajili ya ujenzi wa madarasa ya kidato cha kwanza 2023, Sh. milioni 209.3 za elimu bila malipo kwa shule za msingi na sekondari na Sh. milioni 40.7 matumizi ya kawaida.

Wakati huo huo, Baraza la Madiwani wa Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro katika kikao maalumu, limeridhia hesabu za mapato na matumizi kupelekwa kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), baada ya kuridhishwa na taarifa za mapato na matumizi kwenye miradi ya maendeleo katika kipindi cha mwaka 2021/2022.

Akizungumza katika kikao hicho cha kupitia hesabu za mwisho, Meya wa Manispaa ya Morogoro, Paschal Kihanga, aliwapongeza viongozi wa manispaa hiyo kwa kazi nzuri.

Madiwani hao walipongeza kazi nzuri inayofanyika ikiwamo kudhibiti matumizi yasiyo ya lazima na fedha nyingi kuelekezwa kwenye maendeleo ikiwamo ujenzi wa shule, zahanati na miradi mingine ya maendeleo.

Hata hivyo, baadhi ya madiwani walisema udhibiti wa fedha uliofanywa na watendaji wa halmashauri umesababisha sehemu ya fedha kurudishwa Serikali Kuu badala ya kuelekezwa kwenye miradi mingine ya maendeleo.

Akijibu hoja hiyo, Mkurugenzi wa halmashauri, Ally Machela, alisema kuna kipindi wanapokea fedha kutoka serikali kuu katika kipindi kifupi kabla ya kufunga hesabu na kushindwa kutumika na kukamilika kwa mradi kutokana na hali hiyo kanuni zinaelekeza fedha hizo zirudishwe.

Machela alisema fedha zilizotarajiwa kurudishwa serikali kuu zilitengwa kwa ajili ya kuboresha mazingira bora ya kufanyia biashara wamachinga Sh. milioni 490, lakini fedha hizo zitaendelea kubaki kwenye halmashauri baada ya kupewa kibali cha kuendelea na programu hiyo.

Baraza hilo maalum lilihudhuriwa na viongozi mbalimbali akiwamo Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi (CCM) Wilaya ya Morogoro Mjini, Fikiri Juma, ambaye aliwapongeza madiwani kwa kuchangia hoja kwa busara bila ya jazba huku akiridhishwa na utekelezaji wa ilani ya CCM katika kuleta maendeleo ya wananchi kunakofanywa na watendaji wa halmashauri hiyo.




Mkuu wa Wilaya ya Ilala, Ng'wilabuzu Ludigija (wa pili kushoto), akisalimiana na Mkaguzi Mkuu wa Ndani wa Benki ya NMB, Benedicto Baragomwa (wa pili kulia), katika hafla ya kukutana na wateja wakubwa wa Benki ya NMB hoteli ya Johari Rotana jijini Dar es Salaam. Kushoto ni Mstahiki Meya wa Jiji la Ilala, Omar Kumbilamoto na kulia ni Meneja wa NMB Kanda ya Dar es Salaam, Donatus Richard. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# CCM yajivunia mafanikio ya Samia siku 558 madarakani

**Na Beatrice Shayo,** PWANI

KATIBU wa Itikadi na Uenezi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Shaka Hamdu Shaka, amesema siku 558 tangu Rais Samia Suluhu Hassan kuingia madarakani zimekuwa za mafanikio, akiruhusu falsafa za uchumi kuongoza uchumi badala ya nguvu za utawala.

Shaka aliyasema hayo jana wakati akitembelea maonyesho ya tatu ya uwekezaji na biashara yanayofanyika Kibaha, Pwani.

"Leo (jana) ni takribani siku 558 tangu Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan aapishwe kuwa Rais wa nchi yetu, baada ya kiapo alitoa mwelekeo wa serikali atakayoiunda na kuiongoza kuwa nia yake itakuwa kuifungua nchi kiuchumi.

"Sote ni mashuhuda tumeanza kushuhudia akiruhusu misingi ya falsafa za uchumi kuongoza uchumi badala ya nguvu za kiutawala. Tumeshuhudia Rais Samia akitumia taaluma yake ya uchumi na uzoefu wake wa kiuongozi na masuala ya kidiplomasia, akibadili kabisa mazingira na kasi ya utekelezaji wa mipango ya maendeleo," alisema.

Shaka alisema kupitia diplomasia ya uchumi amefanikiwa kutafuta na kuvutia wawekezaji, kuimarisha mazingira ya biashara na kuongeza shughuli za uzalishaji zitakazoongeza ajira na mapato ya serikali.

Alisema Rais pia amebadili mazingira ya biashara na uwekezaji kwa kuondoa urasimu, ukusanyaji kodi wa mabavu, kufanya maboresho ya sheria na mifumo mbalimbali kwa lengo la kuondoa kero kwa wafanyabiashara na wawekezaji, ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa ilani ya ibara za 22, 46 na 49.

Alisema wawekezaji popote walipo wanaweza kukamilisha taratibu zote za kusajili miradi na upatikanaji wa vibali vyote kupitia kituo kimoja kwa njia ya mtandao, yaani dirisha la uwekezaji kielektroniki.

"Mageuzi mengine ni kuiongoza Tanzania kuridhia mkataba wa kujiunga na eneo huru la biashara Afrika (AFCFTA), hatua itakayoiwezesha Tanzania kutumia nafasi yake ya kijiografia kunufaika na soko kubwa barani Afrika lenye takribani watu Sh. bilioni 1.3 na pato ghafi kwa kuuza bidhaa na huduma," alisema.

Shaka alisema Rais Samia ameonyesha mwelekeo wa kuifungua nchi kiuchumi kupitia uwekezaji wa kongani za kiuchumi (Economic parks) zikihusisha kongani za viwanda, teknolojia, uongezaji thamani na kilimo.

Alisema takwimu zinaonyesha katika muda mfupi wa uongozi wa Rais Samia amevutia uwekezaji wenye thamani ya dola za Marekani bilioni 16 sawa na Sh. trilioni 37.

"Huu ni ushahidi kuwa Rais Samia amedhamiria kuifanya Tanzania nguzo ya uchumi Afrika. Mafanikio makubwa yameonekana katika viwanda na biashara ushahidi ukiwa kuongezeka kwa mapato ya kodi, idadi ya viwanda vipya vinavyojengwa na biashara mpya zinazofunguliwa au kurejeshwa nchini kwa sababu ya mazingira ya sasa yanawapa imani na kujiamini wawekezaji na wafanyabiashara," alisema.

Aliongeza kuwa kati ya mafanikio makubwa, ni ujenzi wa kongani ya viwanda 100 katika Wilaya ya Kigamboni katika eneo lenye ukubwa wa mita za mraba milioni 2.2 na uwekezaji wenye thamani ya dola za Marekani bilioni tatu unaofanywa na Kampuni ya Elsewedy Electric ya Misri.

Shaka alisema viwanda hivyo kila kimoja kitaajiri watu 500 na nchi ina viwanda hivyo takribani 41.

Alisema ujenzi wa kongani ya Kwala Kibaha mkoani Pwani yenye viwanda 200 unaotekelezwa na mwekezaji GSI kupitia Kampuni ya Sino Tan Kibaha Industrial Park Limited (STKIPL) katika eneo lenye ukubwa wa ekari 2,500 na uwekezaji wa dola za Marekani sawa na Sh. bilioni sita.

Shaka alisema kongani hii ikikamilika itatoa ajira za moja kwa moja zipatazo 100,000 na ajira zisizo za moja kwa moja 300,000.

Alisema viwanda vitakavyojengwa ni vya kisasa na vikubwa na shabaha ya wawekezaji wote hao ni kuzalisha bidhaa zao wakiwa Tanzania, ili kutumia nafasi yake ya kijiografia kupata unafuu na urahisi wa kuyafikia masoko na kuingia soko la Afrika.

Shaka alisema chama kimeshauri viongozi wa serikali kuhakikisha ardhi inatengwa na kupimwa katika maeneo yote yaliyotengwa kwa ajili ya uwekezaji kwa kuyatanza na kupeleka huduma za msingi kama barabara, maji na umeme.

Mkuu wa Mkoa wa Mtwara, Kanali Ahmed Abbas, alisema maonyesho hayo yamempa funzo kubwa na atakaporejea mkoani kwake, atafanya jambo.

# JK aipongeza EPZA kuvutia wawekezaji uzalishaji bidhaa

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS mstaafu, Jakaya Kikwete ameipongeza Mamkaka ya Ukanda wa Uzalishaji wa Mauzo Nje ya Nchi (EPZA) kwa juhudi ya kuvutia wawekezaji kuzalisha bidhaa zenye ubora kwa ajili ya soko la ndani na la nje.

Kikwete aliyasema hayo mwishoni mwa wiki alipotembelea banda la EPZA wakati wa maonesho ya tatu ya uwekezaji na viwanda yanayofanyika Mkoa wa Pwani.

"Naipongeza EPZA kwa kuendelea kuvutia wawekezaji kwenye viwanda ambavyo vinatengeneza bidhaa zenye ubora na ambazo zinashindana katika soko la ndani na la nje," alisema.

Kadhalika alisema, juhudi hizo zinazofanywa na Taasisi ya EPZA zina manufaa makubwa katika nchi hasa kuzalisha ajira nyingi za viwandani na kuchangia ongezeko la fedha za kigeni katika nchi.

Aliwataka wananchi wa mkoa huo kutumia fursa kubwa zinazoletwa na ujenzi wa viwanda vingi katika mkoa ili kuboresha kipato na maisha yao na pia kuchangia katika uchumi wa nchi.

"Ujenzi wa viwanda vingi zaidi katika mkoa huu utawanufaisha wananchi kwa kuwapatia ajira za moja kwa moja na zisizo za moja kwa moja hivyo kuweza kupata kipato zaidi na kuboresha maisha yao," alisisitiza.

Kikwete alimwomba Mkuu wa Mkoa wa Pwani, Abubakar Kunenge, kusimamia vyema upimaji na uendelezaji wa eneo la mradi wa viwanda la Kwala ili kuepusha migogoro na kutimiza lengo la mradi husika.

Ofisa Mhamasishaji Mkuu wa EPZA, Nakadongo Fares, alimshukuru Kikwete kwa kutambua juhudi za kuvutia wawekezaji kwenye viwanda kuzalisha bidhaa zenye ubora kwa ajili ya masoko ya ndani na ya nje.

"Kwa niaba ya EPZA tunamshukuru sana Rais mstaafu Kikwete kwa kutuhimiza kuendelea kukuza na kuvutia uwekezaji katika viwanda ili kuchangia katika kukuza uchumi wa nchi," alisema.

Alisema EPZA inavutia wawekezaji katika viwanda nchini na inatoa leseni kuzalisha bidhaa na asilimia 80 huuzwa nje ya nchi.

Alisema kupitia EPZA, mwekezaji anapata ardhi ambayo imeendelezwa na huduma muhimu kama maji, umeme, na mawasiliano. Pia EPZA inatoa msamaha wa kodi kwa muda wa miaka 10 kwa kuwa uwekezaji katika viwanda huchukua muda mrefu kuanza kupata faida.

Fares alisema Watanzania wanahimizwa kutumia fursa hiyo kuwekeza katika maeneo ya EPZ na SEZ ili kunufaika na motisha mbalimbali zinazotolewa na mamlaka ili kuzalisha bidhaa bora kwa ajili ya soko la ndani na la nje.

Alisema uwekezaji katika viwanda ni wa muhimu kwa uchumi wa nchi na huzalisha pia ajira za kutosha kwa ajili ya wananchi ili kuboresha maisha yao.




Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Festo Kiswaga (kulia), akikata utepe katika hafla ya mgodi wa Barrick Bulyanhulu kukabidhi mashine 2 za biohazard safety cabinet kwenye Hospitali ya Manispaa ya Kahama mkoani Shinyanga na Kituo cha Afya cha Bugarama mwishoni mwa wiki. Kushoto ni Kaimu Meneja Mkuu wa Barrick Bulyanhulu, Josephat John na wengine ni maofisa wa serikali wilayani humo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wakulima kunufaika na mpango mikopo kidigitali

**Na Romana Mallya**

SHIRIKISHO la Vyama vya Ushirika Tanzania (TFC) kwa kushirikiana na kampuni ya usimamizi wa fedha kwa njia ya kidijitali ya Wakandi Tanzania, wamezindua Mpango wa Maendeleo ya Sekta ya Kilimo (ASDP II) ili kusaidia wakulima kuweka akiba na mikopo kidigitali.

Akizindua mpango huo juzi jijini Dar es Salaam, Mrajis Msaidizi wa Vyama vya Ushirika wa Mkoa wa Dar es Salaam, Abdillah Mutabazi alisema mfumo huo ni muhimu kwa wakulima kwa kuwa unawajengea uwezo wa kuwa na Vyama vya Akiba na Mikopo (SACCOS) mahali ambako kuna Vyama vya Ushirika wa Masoko ya Kilimo (AMCOS).

Pia alisema kuwapo kwa SACCOS mahali ambako kuna AMCOS ni kuwawezesha wakulima kupata mikopo yenye gharama nafuu. "Kwa muda mrefu wakulima walikuwa na desturi wakiuza mazao msimu unaofuata wanapata shida ya kutafuta pembejeo.

"Ujio wa mfumo huu wa kidigitali wa CAMS kwa kuanzisha vyama vya akiba na mikopo mahali kwenye AMCOS utasaidia kujiwekea akiba na msimu wa kuhudumia mashamba, wataweza kukopa," alisema.

Katibu Mtendaji wa TFC, Alex Ndikile alisema kuwa kwa kushirikiana na Shirika la Wakandi, wamezindua mfumo huo utakaotumiwa na SACCOS.

"Wakandi ni mmoja wa wabia wetu ambao wamesajiliwa kutoa huduma ya mfumo katika SACCOS ambao utasimamia SACCOS kufanya shughuli zao kidigitali, vyama vya ushirika navyo vina wajibu wa kutumia Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) kama suluhisho la shughuli zao hasa wanapokutana na changamoto," alisema.

Alisema mifumo ndiyo itakayosaidia kuendana na upatikanaji wa fursa za masoko na kuwaunganisha na mikutano mbalimbali na bidhaa zinazozalishwa Tanzania zinawafikia walaji kwa muda mwafaka.

Alisema mpango wa ASDP II utafanyika mikoa yote katika awamu ya kwanza ambapo takribani vyama vya ushirika 2,100 vinatarajiwa kufikiwa na awamu ya pili itafuatia baada ya tathmini na matokeo ya awamu ya kwanza.

"TFC inakusudia kuvifikia vyama vyote vya ushirika 5,200 mwishoni mwa mpango huu ambapo sasa tunashirikiana na Wakandi, ambao hutoa ufumbuzi wa usimamizi wa SACCOS kwa mfumo wao wa kidigitali wa CAMS utakaonufaisha mpango huu," alisema.

Mwenyekiti wa Wakandi Tanzania, Richard Sinamtwa, alisema wanajishughulisha na eneo la TEHAMA kwa kuanza na SACCOS, lengo likiwa kuzifanya ziwe na ufanisi na zitimize malengo yake kigitali na kuondokana na jina 'sekta isiyo rasmi'.

"Mfumo huu umetengenezwa Tanzania na utatumika pia na nchi ya Kenya na Uganda, umelenga eneo lisilo rasmi Bara la Afrika. Wadau wetu kutoka Norway wamekubali Tanzania iwe chachu ya kuanzisha mfumo huu ili usaidie bara zima la Afrika," alisema.

Mkurugenzi wa Wakandi Group kutoka Norway, Espen Kvelland, akizizungumzia Tanzania, Kenya na Uganda ambazo zinatumia mfumo huo mpya, alisema anaamini nchi hizo zina ushindani wa kirafiki na zitautumia kuwanufaisha wakulima wao.

# Mabinti washtaki wazazi kwa Samia

**Na Sabato Kasika**

MABINTI waliokatisha shule kutokana na ujauzito wilayani Serengeti mkoani Mara, wamemwomba Rais Samia Suluhu Hassan kuwachukulia hatua wazazi na walezi wanaoozesha watoto wao walio chini ya umri wa miaka 18.

Mabinti hao wamemwomba Rais kufuta Sheria ya Ndoa ya Mwaka 1971, inayoruhusu mtoto wa chini ya umri huo kuolewa, kwa madai inasababisha kuolewa wakiwa wadogo badala ya kusoma na kushindwa kutimiza ndoto zao katika elimu.

Maombi hayo yamo kwenye barua yao waliyoiandika baada ya kupata mafunzo ya kuwezesha kujikimu kimaisha yaliyotolewa na mkufunzi kutoka Kituo cha Sauti ya Jamii Kipunguni Dar es Salaam, Seleman Bishagazi.

Mafunzo hayo yalifanyika mjini Mugumu na kuandaliwa na Shirika lisilo la kiserikali la Girls Education Support Initiatives (GESI) na kushirikisha mabinti 50 kutoka kata 15, ambao baadaye waliandika barua hiyo.

"Yahusu kuchukua hatua kali kwa wazazi wanaoozesha watoto wadogo. Ndugu mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan. Tunatumaini u-mzima wa afya, nasi pia ni wazima wa afya," inasomeka sehemu ya barua hiyo.

"Dhumuni la kuandika barua hii ni kukuomba wazazi wanawaoozesha watoto wadogo wa chini ya miaka 18, wachukuliwe hatua kali za kisheria, kwani kuna madhara mengi ya ndoa za utotoni."

Katika barua hiyo wanataja madhara wanayokutana nayo watoto kuwa ni vifo na kumwomba Rais awasaidie kumaliza janga hilo, kwa kuwa limeshamiri nchini, hasa Mkoa wa Mara.

"Mwisho, sisi mabinti wa Mkoa wa Mara tunakuomba sheria inayoruhusu watoto kuolewa ifutwe. Tunaomba kuwasilisha." Inamalizia barua ambaye Nipashe ina nakala yake.

Akizungumzia barua hiyo, mkufunzi wa mafunzo hayo Bishagazi alisema hizo ni dalili kwamba mabinti sasa wameanza kujitambua na kujua haki zao na kufafanua kuwa hivyo ndivyo wanapaswa kupaza sauti zao.

"Sisi tunaopambana na ukatili wa kijinsia tumekuwa tukihimiza watu kujitambua na kupaza sauti wanapoona wanaonewa, hao mabinti wameshaelimishwa na sasa wanaonyesha ni jinsi gani wanatambua haki zao," alisema Bishagazi.

Alisema hata kama barua yao haitamfikia Rais, lakini wamethubutu kupaza sauti zao wakionyesha jinsi wanavyotambua na kukerwa na vitendo hivyo vinavyochangia kukwamisha maendeleo yao.

"Ninadhani barua yao iwe chachu ya kuhamasisha mabinti wengine nchi ambao wako kwenye hatari kama hiyo, ili wawe tayari kutoa taarifa kwa vyombo vya dola wanapokumbana na vitendo hivyo.



## Waliohama Hifadhi Ngorongoro wasimulia maisha waliyopitia

**Na Hamida Kamchalla,** HANDENI

BAADHI ya wanawake jamii ya kifugaji ya Kimasai, waliohama kwa hiari kutoka eneo la Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro (NCAA), kwenda Kijiji cha Msomera, Wilaya ya Handeni, mkoani Tanga, wameeleza namna walivyokuwa wakitegemea kuuza kuni kuendesha maisha yao.

Akieleza kuhusu ugumu wa maisha walipokuwa Ngorongoro, kiongozi wa wanawake wa Kimasai, Martha Maseya, alisema waliishi maisha ya kuokota na kuuza kuni ili kujikimu kimaisha.

"Tunamshukuru Rais wetu Samia, kwa kutuondoa kule kwenye maisha ya kuhangaika. Tulikuwa tunaokota kuni ili kuendesha maisha ya familia, sasa hapa tunaona tumefika sehemu yenye neema.

"Tunaona tumepata mabadiliko ya maisha kupitia mama (Rais Samia). Tumeona wenyewe na tunaamini, yale maneno maneno waliyokuwa wakisema viongozi wa mila na wanaharakati, wao ndiyo walitudanganya."

Mkuu wa Wilaya ya Handeni, Siriel Mchembe, akizungumzia maendeleo ya eneo hilo wakati wa kukabidhi hati kwa wananchi hao, alisema hadi sasa wamezipokea kaya 61 zenye wanawake 310.

"Ndugu zangu, mpaka siku ya leo, tumepokea jumla ya kaya 349 zenye watu 1,775 ikiwa ni pamoja na mifugo yao 9,390. Maana yake ni kwamba, hapo awali tulijenga kaya 103, baadaye tukajenga kaya 400, kwa hiyo bado tuna zaidi ya kaya 100 ambazo hazijaingia watu," alisema Mchembe.

"Serikali yenu itawaletea miundombinu ya umwagiliaji, kwa hiyo mtakapopewa hizo heka tano mjiandae kupata elimu ya kilimo bora cha kisasa ili hizo heka zituletee manufaa kwa kutuingizia kipato," alisema Mchembe.

Pia aliwahakikishia wananchi hao kuwapatia eneo la malisho ambayo pia watafuga kisasa na kuwa na mifugo ambayo itawaletea tija katika masomo kuliko kufunga ng'ombe wengi ambao huenda wakakisa afya kwakuwa imepangwa Msomera kiwe kijiji cha mfano cha wafugaji.

Alisema: "Vilevile mtapewa eneo la malisho kwa ajili ya mifugo yenu, ila kipekee ni kwamba sera ya Rais Samia Suluhu Hassan inataka muwe na pesa, kuliko kuwa na ng'ombe wengi wasio na tija, ni bora ubaki na ng'ombe watano, maana ukiwa na nao watano hawa wa kawaida hutakosa Sh. milioni tatu kila mmoja."

# Atiwa hatiani kwa kukutwa na dawa za kulevya

**Na Jaliwason Jasson,** MANYARA

MAHAKAMA ya Wilaya ya Babati mkoani Manyara imemtia hatiani mkazi wa Nangara, Fahad Abdi (21) kwa kosa la kukutwa na gramu 10.50 za dawa za kulevya aina ya bangi, kutakiwa kulipa faini ya Sh. 300,000 ili kuepuka kifungo.

Hata hivyo kijana huyo alishindwa kulipa faini hiyo na mahakama iliamuru apangiwe kazi za kijamii katika taasisi za umma kwa muda wa mwaka mzima.

Hukumu hiyo ilitolewa mwishoni mwa wiki na Hakimu Mkazi Mfawidhi wa Mahakama hiyo, Victor Kimario, baada ya mshtakiwa kukiri kosa.

"Kwa kuwa mshtakiwa amekiri kosa lake, mahakama hii imemtia hatiani kwa kosa hilo, baada ya kukiuka Kifungu cha 17(1) (b) cha Sheria ya Udhibiti wa Dawa za Kulevya, Sura ya 15 iliyofanyiwa marejeo mwaka 2019.

Kwa mujibu wa hati ya mashtaka, mshtakiwa huyo alikamatwa Septemba 8, mwaka huu, majira ya saa 5:00 asubuhi katika Kituo Kikuu cha Mabasi cha Makatanini cha Wilaya ya Babati.

Ilielezwa kuwa mshtakiwa huyo alikamatwa na askari polisi baada ya kupata taarifa kuwa kuna pikipiki imepeleka eneo hilo dawa za kulevya aina ya bangi kwenye duka la Omari.

Awali ilidaiwa mahakamani hapo na Mwendesha Mashtaka wa Serikali, Grace Mgaya, kuwa mshtakiwa alikamatwa na misokoto minne ikiwa ndani ya suruali.

Mgaya, aliiomba mahakama hiyo kumpa adhabu kali ili iwe fundisho kwa jamii.

Hakimu Kimario alimuuliza mshtakiwa ilikuwaje mpaka akakutwa na bangi, ndipo Abdi alisema alipigiwa simu na mteja wake akimtaka apeleke mzigo Stendi Kuu ya Mabasi Makatanini.

Alipotakiwa kujitetea mtuhumiwa huyo alisema ana familia, anaiomba mahakama impunguzie adhabu na hatarudia kosa hilo.



Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Mbegu za Kilimo (ASA), Dk. Sophia Kashenge, akitambulisha Kampuni ya Pro Agro Grobla kwa Mkuu wa Mkoa wa Arusha, John Mongela, mwishoni mwa wiki. Kampuni hiyo inajenga miundombinu ya umwagiliaji katika mashamba ya Arusha Ngaramtoni pamoja na Tengeru. **PICHA: WOINDE SHIZZA**

## Mradi kunufaisha wawindaji, waokota matunda, warina asali

**Na Allan Isack,** ARUSHA

JAMII za kifugaji pamoja na kabila jamii ya waokota matunda, warina asali na wawindaji wa Kihadzabe kutoka wilaya 10 za mikoa ya Arusha, Manyara na Singida, wako mbioni kunufaika na mradi mpya wa uhifadhi kwa ajili ya kuboresha maisha yao.

Mradi huo unalenga kuwajengea uwezo wananchi hao kusimamia rasilimali ardhi na nyinginezo zilizoko kwenye maeneo yao.

Mkurugenzi wa Shirika la Ujamaa Communit Resource Team (UCRT), Paine Mako, alisema mradi huo una thamani ya Dola za Marekani 840,000 na utatekelezwa kwenye vijiji 120.

Alisema mradi umefadhiliwa na Shirika la Kimataifa la Uhifadhi wa Mazingira (IUCN) na utatekelezwa kwenye wilaya za Monduli, Longido, Ngorongoro, Karatu, Simanjiro na Kiteto,Mbulu, Hanang', Babati na Mkalama.

"Mradi huu umelenga kuweka mipango bora ya matumizi ya ardhi, kuviwezesha vikundi vya vijana na wanawake, pamoja na kuijengea jamii uwezo wa kusimamia rasilimali zinazopatikana kwenye maeneo yao,"alisema.


Alisema UCRT kwa kushirikiana na serikali katika mikoa mitatu ya Arusha, Manyara na Singida, kwenye wilaya 10 zenye vijiji hivyo wamefanikiwa kutekeleza miradi ya kuiwezesha jamii kulinda haki ya ardhi zao, kuanzisha mipango ya kusimamia rasilimali asili kwa matumizi bora na endelevu.

Ofisa Miradi kutoka IUCN, Doyi Mazenzele, alisema shirikisho hilo linafanya kazi ya uhifadhi wa mazingira na limeanzishwa mwaka 1948 na lilianza kufanya kazi hapa nchini mwaka 1970.

"Shirika letu lina miradi mbalimbali pia ni wakala wa mfuko wa mazingira duniani, wakala wa mfuko wa mabadiliko ya tabianchi kwa kuzisaidia serikali na taasisi mbalimbali kuandika miradi kwa maendeleo endelevu,"alisema.

Alisema UCRT walipewa kipaumbele kwa ajili ya kuuandaa kwa upande wa Tanzania, umefadhiliwa kwenye mzunguko wa saba na utatekelezwa kwenye nchi 11.

"Mradi huu ufanyika kwenye nchi 11 na kwa Afrika ziko nchi tatu zilizopewa ambazo ni Tanzania, Kenya na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo," aliongeza.





## UVCCM yaijibu BAVICHA kauli iliyotolewa na Dk. Tulia

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

MWENYEKITI wa Jumuiya ya Vijana ya Chama Cha Mapinduzi (UVCM) Moshi Vijijini, mkoani Kilimanjaro, Yuvenal Shirima, amesema jumuiya hiyo haitaruhusu matamko yenye 'utata' yanayolenga kuwagawa Watanzania.

Alitoa kauli hiyo baada ya hivi karibuni Mwenyekiti wa Baraza la Vijana la CHADEMA Taifa, John Pambalu, kuzungumza na vyombo vya habari.

Shirima alisema yuko tayari kukabiliana naye, hatakubali kumuona mtu yeyote ambaye anajaribu kuongea mabaya dhidi ya serikali, hasa kumsema Rais Samia Suluhu Hassan.

Akizungumza jana na waandishi wa habari kuhusu kauli ya Spika wa Bunge, Dk. Tulia Akson iliyozua mjadala kutokana na kutumia neno 'nyooka naye' Shirima, alisema kinachoendelea katika nchi yetu kwa sasa dhidi ya kile alichokisema Dk. Tulia, ni utashi mdogo wa wanasiasa kutafsiri mambo.

Shirima alisema: "Nitahakikisha na dili nae, na nitahakikisha nafanya kazi kadiri niwezavyo kuhakikisha namfikisha ili aweze kujua umuhimu wa CCM na aweze kuiacha serikali iweze kufanya kazi.

Oktoba 5, mwaka huu, Mwenyekiti wa BAVICHA Taifa, John Pambalu alinukuliwa akimtaka Spika wa Bunge, Dk. Tulia Akson, kujiuzulu kufuatia kauli aliyoitoa hivi karibuni, wakati akizungumza na vijana wa hamasa CCM Wilaya ya Mbeya Mjini.

Oktoba 3, mwaka huu katika mitandao ya kijamii ilionekana video yenye sekunde 58, ikimwonyesha Dk. Tulia, akiwaonya vijana hao kutoungana na mtu yoyote anaemsema vibaya Rais Samia ambaye ni Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM).

Katika video hiyo Dk. Tulia ailisikika akisema: "Rais Samia ni Rais wa nchi na Mwenyekiti wa chama chetu, asitokee mtu yoyote ndani au nje ya chama akamkosoa, shughulikeni nae na nyookeni naye".

# Kiongozi wa dini ataja chanzo matukio ukatili

**Na Mwandishi Wetu,** HAI

MWANAZUONI wa Kanisa Katoliki, Jimbo la Moshi, Padri Jebra Kimario, amesema kiini cha ongezeko la matukio ya ukatili dhidi ya watoto kwa sasa, unachochewa na wazazi wengi kutoona thamani ya watoto wao kwa sababu ya kuabudu zaidi maisha ya kiuchumi.

Akihubiri jana katika ibada ya kuwaaga wanafunzi wa kidato cha nne wa Shule ya Wasichana ya St. Eugene Marie iliyoko Chekereni, Kata ya Mnadani, Wilaya ya Hai, mkoani Kilimanjaro, Kimario, alisema wazazi wengi wanafanya hivyo, kwa kuona uchumi wao unatikisika.

"Wazazi wengi wa sasa ni wazaaji na wengi hawamjali yule waliyemzaa. Hawamuoni kama ana thamani. Na hii inachagizwa na binadamu anayejali zaidi maisha ya kiuchumi, maisha ya kidunia ya kupata na kuendekeza anasa dhidi ya maisha ya utakatifu, ambayo ni ya furaha na ya heri kwa mwanadamu.

"Ukatili huu wa sasa unatokana na kuzaa watoto bila kupanga. Mtu anaposema anapenda na anatamani kuzaa, anakwenda kukaa na mtu kinyumba halafu wanaita ni ndoa. Hiyo siyo ndoa, kwa sababu mtoto anayezaliwa kwenye ndoa angethaminiwa na asingeteswa, kuchomwa mikono au mwili na mtu anayesema ni mzazi.

"Ndiyo maana unakuta, mtoto anayezaliwa nje ya ndoa, anaonekana kama ni bahati mbaya na hao ndiyo waathirika wakubwa wa vitendo vya ukatili, wale wanaolelewa na bibi na babu, baada ya wazazi wao kuachana na kukimbilia kutafuta maisha nje ya familia, huko mijini na mikoani."

Padri Kimario, alifafanua zaidi kuwa wazazi hao, wanamchukulia mtoto wa aina hiyo kama ni 'liability.' Yaani mzazi ambaye hajamzaa huyo mtoto, anaona kama huyo mtoto anakuja kula uchumi wa familia.

Mkuu wa Shule ya St.Eugene Marie, Mtawa Bernadetha Mushi, alisema shule hiyo imekuwa ikifanya vizuri katika mitihani ya kitaifa kwa watahiniwa wa kidato cha nne, mwaka 2020, daraja la kwanza walikuwa 89, daraja la pili, wanafunzi wanne na shule ilishika nafasi ya pili kimkoa, kati ya shule 275 na kitaifa ilishika nafasi ya 26.

Alisema mwaka 2021, daraja la kwanza walikuwa 82, na daraja la pili walikuwa wanafunzi saba. Shule ilishika nafasi ya tatu katika shule 271 kimkoa na kitaifa ilikuwa nafasi ya 26, kati ya shule 441.

Alisema nia yao ni kuwa miongoni mwa shule 10 bora kitaifa mwaka ujao, kwa watahiniwa wanaofanya mitihani yao Novemba mwaka huu.




Mkurugenzi wa Kitengo cha Ukuzaji Tija Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi, Vijana, Ajira na Watu Wenye Ulemavu, Yohana Madadi (kushoto), Mwenyekiti wa Taasisi ya Kalamandalam Tanzania, Thulaseedas Gopalan (kulia), wakikabidhi msaada wa baiskeli 24 za watu wenye ulemavu zenye thamani ya Sh. 850,000 kila moja. Wa pili kushoto ni Mkurugenzi Mtendaji wa Tumaini la Maisha, Dk. Trish Scanlan, hafla iliyofanyika jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# AUWSA yapongezwa kupeleka maji Uwanja wa Ndege

**Na Daniel Sabuni,** HAI

SERIKALI imesema imefurahishwa na uamuzi wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira jijini Arusha (AUWSA), kuridhia kuchepusha mradi wake mkubwa wa maji uliofadhiliwa na Benki ya Dunia (WB), kuingia katika himaya ya Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro (KIA)

Jana, Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Nurdin Babu, alisema maji hayo kuingizwa ndani ya viunga vya KIA, yatasaidia kuongeza kasi ya jitihada za serikali za kupambana na magonjwa ya mlipuko, ikiwamo ebola na UVIKO-19, ambayo yanaitikisa dunia kwa sasa.

Babu aliyazungumza hayo jana akiwa Wilaya ya Hai, alipokwenda kuzindua mradi mpya wa maji wa AUWSA, wenye uwezo wa kuzalisha zaidi ya lita 500,000 za maji.

Alisema upatikanaji wa maji safi ya kutosha na salama, yatasaidia kushinda vita dhidi ya magonjwa ya ebola na UVIKO-19, kwa wasafiri kunawa kabla na baada ya safari.

"Uwanja huu wa kimataifa unatumiwa na wageni wengi kutoka mataifa tofauti, UVIKO kwa kiasi kikubwa tumeushinda, sasa ebola iko jirani kabisa hapa Uganda. Tupambane nao kwa kutumia maji na maelekezo mengine ya wataalamu wa afya.

"Lakini, nikupongeze Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Uendeshaji na Usimamizi wa Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro, Christina Mwakatobe, kwa ndoto yako uliyoita ya mahitaji ya maji, hivyo kuomba mradi wa maji na hatimaye serikali kuamua uje hapa KIA." Alisema.

Mkurugenzi Mtendaji wa KADCO, Christina Mwakatobe, alishukuru serikali kwa kujali afya za wageni na kukubali kugharamia na kutekelezwa kwa mradi huo.

"Tuna mahitaji ya lita za ujazo 500,000, maji haya yakipatikana na kupata kiasi hicho na ziada tutagawa kwa kijiji cha chochote cha jirani ili kiondokane na adha ya kukosa maji,"alisema.

Ofisa Mwandamizi AUWSA, Felis Fidelis alisema: "Maeneo haya miamba yake ina madini mengi ya floride ambayo ni hatari kwa watumiaji, tumedhamiria kuchimba umbali huo kwa uhakika wa kupata maji ambayo hayana floride ya kudhuru watumiaji."

Mshauri wa kampuni iliyopewa zabuni ya kuchimba maji kupitia mradi huo ya Shanxi Engineering Constraction ya China, Khamis Sangoda, alisema miradi kama huo inagharimu zaidi ya Sh. mil. 300 mpaka kukamilika.

Alisema kwenye umbali wa mita 300 wakati wa kuchimba wanakumbana na miamba mingi na migumu na ndiyo sababu ya kuchimba kwa muda mrefu usiku na mchana.

Nipashe

# Spotika



WACHEZAJI WATANO WALIOFUNGA HAT-TRICK NYINGI KWA MSIMU EPL UK.16



## ISIKUPITE

KWENYE Ligi Kuu England, hakuna mchezaji yeyote aliyewahi kufunga hat-trick katika mechi tatu mfululizo za nyumbani hadi mshambuliaji wa Manchester City, Erling Haaland alipofanya hivyo dhidi ya Manchester United wiki moja iliyopita. Lakini hiyo ni 'dabi' ya kwanza ya Manchester kwa mchezaji wa City kufunga hat-trick tangu Francis Lee alipofanya hivyo Desemba 1970.

# MTU KATI...

Mshambuliaji wa Yanga, Fiston Mayele, akiwa amewekwa 'mtu kati' na mabeki wa Al Hilal ya Sudan kwenye mechi ya  raundi ya kwanza ya Ligi ya Mabingwa Afrika iliyopigwa katika Uwanja wa Benjamin Mkapa juzi na kumalizika kwa sare ya bao 1-1. **PICHA: MTANDAO**



KLOPP

# MAKOCHA WANNE WALIOKALIA KUTI KAVU

**LONDON,** England

KATIKA kiwango cha juu cha soka, makocha ni mojawapo ya seti za watu wanaochunguzwa sana. Kila matokeo yanachangiwa moja kwa moja na uwezo au kutoweza kwa kocha wa timu na ni kazi yenye shinikizo kubwa.

**Klabu za juu za Ulaya zina wafuasi wengi na mara nyingi makocha wanakuwa hatarini katika kila msimu. Haijapita miezi miwili tangu msimu wa 2022-23 uanze barani Ulaya, lakini tayari tumeona makocha wachache wakifukuzwa kazi.**

Thomas Tuchel ndiye mwenye hadhi ya juu zaidi kati ya makocha ambao tayari wamefukuzwa katika hatua za mwanzo za msimu mpya. Ni asili tu ya kazi siku hizi. Makocha mara nyingi huwa ndio mbuzi wa kafara katika ulimwengu wa soka wakati hali ya timu inakuwa kwenye wakati ngumu. Wakati mwingine ni kosa lao, wakati mwingine la kwao.

Hapa tunawaangalia makocha wanne wa hadhi ya juu ambao kwa sasa wako kwenye shinikizo kubwa la kupoteza kazi zao, twende sasa...

**#4. BRENDAN RODGERS (LEICESTER CITY)**

Leicester City ilimaliza katika nafasi ya tano kwenye Ligi Kuu England msimu wa 2019-20 na msimu wa 2020-21 walimaliza nafasi ya nane. Ingekuwa sawa kusema kwamba 'Mbweha' hao walikuwa wanaanza kujiimarisha kama timu ya kutisha kwenye Ligi ya England.

Hata hivyo, baada ya majira ya joto ambapo walikaa mbali na kuimarisha kikosi chao kutokana na matatizo ya kifedha, Leicester wanayumba msimu huu. Wako mkiani mwa msimamo na hawajashinda baada ya mechi nane za Ligi Kuu. Ni wazi kwamba kocha wa Leicester City, Brendan Rodgers kwa sasa yuko chini ya shinikizo kubwa.

Wamiliki wanaonyesha ukarimu kwa sasa kwani wamechangia katika kuanguka kwa timu hiyo kutokana na kushindwa kuwekeza kwenye soko la uhamisho. Lakini kuna hisia kwamba Rodgers yuko katika wakati mgumu, kwani anaweza kutimuliwa wakati wowote kama matokeo yataendelea kuwa mabaya kwao.

**#3. SIMONE INZAGHI (INTER MILAN)**

Inter Milan ya Simone Inzaghi inashika nafasi ya tisa kwenye jedwali la Serie A baada ya mechi nane. Kipigo chao cha hivi majuzi zaidi cha mabao 2-1 kutoka kwa AS Roma (Oktoba Mosi) huenda kitaonekana kuwa kikwazo kikubwa. Inzaghi aliwaongoza 'Nerazzurri' hao kumaliza katika nafasi ya pili kwenye ligi msimu uliopita.

Lakini timu hiyo ni wazi haifanyi vizuri kwa uwezo wao msimu huu. Akizungumza baada ya Inter Milan kuchapwa mabao 2-1 na AS Roma, mwandishi wa habari wa kutegemewa, Gianluca Di Marzio alisema kwamba Inzaghi anaweza kuishia matatizoni hivi karibuni.

Kazi yake kwa sasa haiko hatarini, lakini mambo yakiendelea hivi, "ataishia kwenye njia panda". Di Marzio alisema (kupitia Sempre-Inter):

"Hakika anatazamwa kwa karibu kwa sasa, lakini kwa sasa siwezi kusema kwamba kuna uamuzi wa mwisho.

"Hadi sasa uhusiano umekuwa wa karibu sana na Inzaghi. Hali ya klabu kwa sasa si ya kijinga hata kidogo. Ni wazi, ikiwa ataendelea kupoteza, ataishia kwenye njia panda."

**#2. MASSIMILIANO ALLEGRI (JUVENTUS)**

Katika misimu miwili iliyopita, Juventus imekuwa mbali na timu iliyotawala Serie A katika muongo mmoja uliopita. Kumtimua Andrea Pirlo na kumleta Massimiliano Allegri kulitarajiwa kusaidia kurejesha klabu hiyo katika siku zake tukufu kwa mara nyingine tena. Lakini kwa urahisi kabisa haijafanya kazi kwa njia hiyo.

Juventus wamevumilia mwanzo mbaya wa msimu mpya. 'Bianconeri' hao wamefanikiwa kushinda mechi tatu pekee kati ya nane za ligi hadi sasa. Wametoka sare nne na kupoteza moja na wanashika nafasi ya saba kwenye jedwali la Serie A.

Soka limekuwa duni na kikosi kinaonekana dhaifu. Allegri yuko chini ya shinikizo kubwa la kuboresha matokeo hivi sasa.

**#1. JURGEN KLOPP (LIVERPOOL)**

Kwamba Jurgen Klopp anaweza kuwa chini ya shinikizo huko Liverpool mapema msimu huu ilikuwa jambo lisilowezekana kabisa kwa muhula uliopita. Kocha huyo wa Ujerumani aliiongoza Liverpool kutwaa Kombe la FA na Kombe la Carabao. Pia walifika fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya na walikuwa kwenye mbio za ubingwa wa Ligi Kuu hadi mwisho.

Lakini baada ya kuanza vibaya kwa msimu wa 2022-23, Klopp yuko chini ya shinikizo. Kazi yake bado iko njiani kutoka kwenye usawa lakini kocha huyo wa Liverpool anahitaji kubadilisha mambo.

'Wekundu' hao kwa sasa wako katika nafasi ya tisa kwenye msimamo wa Ligi Kuu baada ya mechi saba. Wameshinda mechi mbili pekee za ligi hadi sasa msimu huu. Liverpool wanapaswa kufanya vizuri zaidi na aina ya wafanyakazi walio nao katika safu zao.

# IBRAHIM CLASS:

# ANAYEMTAMANI YEYOTE ULINGONI



Ibrahim Class (kushoto), akizipiga ulingoni na Mmexico, Alan Pina. **PICHA: MTANDAO**

**Na Saada Akida**

NI dhahiri vipaji vikiibuliwa tangu utotoni na kuendelezwa vema kwa vijana, wanakuja kuwa wazuri ukubwani katika tasnia husika na hatimaye kulitangaza vizuri taifa nchi za nje.

**Hali hiyo inadhihirika kwa bondia Ibrahim Class 'King Class Mawe' ambaye anafanya vizuri katika medani za ngumi na kulitangaza vema taifa.**

Hakuna asiyetambua kazi na ukubwa wa Ibrahim Class katika mchezo wa ngumi za kulipwa hapa nchini kutokana na kuwa na kiwango kisichotetereka na uwezo mkubwa miaka yote katika tasnia hiyo ya pili kwa kupendwa nchini baada ya soka.

Kwa mujibu wa BoxRec ama boxrec.com, mtandao unaotumika kuhifadhi kumbukumbu za mabondia, Class ana rekodi ya mapambano 33 akiwa ameshinda 27 kati ya hayo 12 kwa KO, amepoteza sita kati ya hayo matatu ni kwa KO na ndiye bondia namba mbili kwa ubora Tanzania.

Kwa kutambua ubora, uwezo na kipaji chake katika masumbwi, Nipashe limefanya mahojiano maalum na bondia huyo wiki iliyopita akitoka kumtembezea kichapo kwa KO bondia kutoka Mexico, Allan Pina pambano hilo likifanyika katika ukumbi wa Mliamani City, Dar es Salaam.

**MTAZAMO WAKE NGUMI ZA KULIPWA**

King Class anasema kwa sasa ngumi ziko juu, huku serikali, wadhamini na mapromota wakijitahidi kuzifanya ngumi kuwa mchezo pendwa na kurudi katika heshima yake.

"Kwa sasa tunaona mabondia wanajulikana sana kwa sababu ya sapoti inayotolewa, ninaimani kwa miaka ya hivi karibuni ngumi utakuwa mchezo wa kwanza kupendwa na kuishusha soka," anasema King Class.

**BONDIA ANAYEMTAMANI**

Anasema baada ya kufanikiwa kumpiga Pina, kwa sasa yuko tayari kupambana na bondia yeyote mwenye rekodi kubwa iwe ndani au nje ya nchini.

"Sichagui bondia, natamani kucheza na bondia mwenye rekodi kubwa kwa sababu malengo yangu makubwa ni kuona siku moja nailetea Tanzania mkanda wa WBC, WBO na WBA," anasema King Class.

**KWA NINI NGUMI**

King Class anasema alishawishika kuingia katika mchezo huo kutokana na mapenzi aliyokuwa nayo tangu utotoni ambapo alikuwa na ndoto za kuwa mwanamasumbwi mkubwa maishani mwake.

Anasema kuwa ndoto yake ilianza kutimia baada ya kaka yake anayeitwa Chaku Master kuwa mwanamasumbwi aliyekuwa akifanya vizuri miaka kadhaa iliyopita.

"Chaku nilikuwa nikiishi naye, hivyo wakati anakwenda kufanya mazoezi nilimwomba tuongozane hali iliyonifanya kuanza kucheza licha ya kwamba ilikuwa ndoto yangu ya siku nyingi."

Anasema kocha wake wa kwanza kuanza kumfundisha kucheza ngumi alikuwa ni mzee Babu Tule ambaye alimpa misingi ambayo imemfanya hadi kuwa bondia mzuri mwenye nidhamu na anayeheshimu sheria za mchezo huo.

Class anasema mwaka mmoja baadaye alihamia kwa kocha mkongwe Habibu Kinyogoli hapo alikutana na makocha wengi akiwamo kocha wa kimataifa wa mchezo huo nchini, Rajabu Mhamila 'Super D.

**KUSHINDA KWA KO**

Anasema baada ya kuwa chini ya kocha wa siku nyingi katika mchezo huo, Kinyogoli, kiwango chake kinakuwa kikiongezeka kila siku na kuwa tishio katika ngumi za 'amacha'.

Class anasema tangu wakati huo amepambana mapambano mengi ambao alifanya vizuri na kushinda kwa KO ni kitu anachojivunia kwa sasa.

"Huwa najisikia faraja ninampompiga mtu kwa KO kwani inazidi kunijengea heshima katika ngazi ya 'amacha' ambayo ndiyo niliyopo kwa sasa ambayo nahisi sina mpinzani," anasema Class.

**SIRI YA MAFANIKIO**

Anasema siri kubwa ya kufanikiwa kufanya vizuri kwenye mapambano yake ni kuzingatia mazoezi, miiko, sheria na kanuni za mchezo huo ambazo kila siku huwa anaelekezwa na kocha Kinyogoli.

Class anasema kila bondia anaweza kufanya vizuri ikiwa atajitahidi kusimama imara kuzingatia yanayokatazwa katika mchezo huo.

"Huwa nazingatia maadili ya kazi yangu ya ngumi, kusikiliza mwalimu na kujifunza kwa sababu kila siku nipo darasani na kupokea kila anayekuja kunipa ushauri na mbinu, siangalii umri wa mtu kwa anayekuja kunishauri," anasema.

**PAMBANO ASILOLISAHAU**

Anasema amecheza mapambano mengi (33), yote yamekuwa na historia, lakini mchezo wa hivi karibuni dhidi ya Allan Pina ni pambano ambalo hatalisahau kwa sababu lilikuwa gumu kwake kucheza.

"Nilikuwa naumwa, nilishikwa na homa kali, wakati promota amekuja kunitaka kusaini mkataba nilikuwa hoi, waliniomba sana nipigane, niliwakatalia kuhofia afya yangu, nakumbuka (Levix), alimpiga simu Mohammed (Mo Dewji) kumweleza hali halisi ya afya yangu.

"Bahati nzuri alituma watu kunifuata na kunipeleka hospitali na kuhakikisha napatiwa matibabu, hiyo ilikuwa wiki mbili kabla ya pambano baada ya matibabu na nilipopona nilifanya mazoezi siku tatu tu hatimaye kufanikiwa kumpiga mpinzani wangu kwa KO," anasena King Class.

Anasema hakutarajia kama angefanikiwa kumpiga kwa KO mpinzani wake kwa sababu ya ubora na maandalizi yake hayakuwa ya muda mrefu.

**UFUNDI UMEME**

King Class anasema licha ya kujihusisha na masumbwi, pia ni fundi wa spika za radio na vyombo vya vyote vya muziki vinavyotumia umeme.

"Kipindi ambacho ninakuwa nyumbani sina pambano lolote, huwa ninafanya kazi za umeme kwa kutengeneza spika za radio na zinazotumika katika kumbi mbalimbali hata kwenye bendi," anasema bondia huyo.

Anasema katika kuhakikisha anaendelea na fani yake hiyo, ana mpango wa kufungua ofisi kubwa kwa ajili ya kuwafundisha vijana ambao hawana ajira ili kujikwamua katika maisha tegemezi na kujitegemea baada ya kupata ujuzi huo.

**SAPOTI YA FAMILIA**


"Namshukuru Mungu familia yangu ipo bega kwa bega katika kuhakikisha wanakuwa nyuma yangu katika huu mchezo," anasema King Class.

Anasema mchezo wa ngumi ameanza kuupata kutoka kwa kaka yake, Remi Joseph, ambaye alikuwa akicheza Kick-boxing na kareti.

"Kipindi hicho nilikuwa mdogo, walikuwa wakinifukuza ila wanapomaliza mazoezi yao nafunga chupa zangu za maji na kujifunza mwenye hadi walipogundua na kunitafutia kocha," anasema King Class.

**NJE YA UWANJA**

KATIKA soko la usajili (transfer market), mchezaji wa Barcelona, Pedri na Jude Bellingham wa Borussia Dortmund ndio viungo wenye thamani kubwa zaidi (kila mmoja euro milioni 90), wakifuatiwa na Federico Valverde wa Real Madrid (euro milioni 80), Gavi wa Barca pamoja na Nicolo Barella wa Inter (kila mmoja euro milioni 70).



# WACHEZAJI WATANO WALIOFUNGA HAT-TRICK NYINGI KWA MSIMU EPL



HAALAND

**LONDON,** England

LIGI Kuu England (EPL), inachukuliwa kuwa ngumu zaidi kucheza kwa sababu ya kiwango cha timu na wachezaji kwenye mashindano hayo.

**Kufunga mabao mara kwa mara na kwa uthabiti katika misimu michache ya Ligi Kuu England, kunachukuliwa kuwa jambo ambalo washambuliaji bora pekee duniani wanaweza kufanya.**

Kwa sababu hiyo, washambuliaji wanaochezea klabu za Ligi Kuu mara nyingi huwa miongoni mwa wachezaji bora zaidi duniani.

Kabla ya enzi za Lionel Messi na Cristiano Ronaldo, wachezaji waliona kufunga hat-trick kama kazi muhimu ya kukumbukwa. Wawili hao mashuhuri wamefanya kufunga mabao matatu yaonekana kama kazi rahisi kutokana na uthabiti wao dimbani.

Nje ya Messi na Ronaldo, wachezaji wengi bado wanatatizika kufunga hat-trick nyingi katika msimu mmoja wa ligi. Hata hivyo, katika kipindi cha miaka 30 iliyopita, wachezaji wengi wamefikia mafanikio hayo katika ligi tano bora za Ulaya, ikiwa ni pamoja na Ligi Kuu England.

Makala haya inawaangalia wachezaji watano waliofunga hat-trick nyingi zaidi katika msimu mmoja wa Ligi Kuu England, EPL.

**#5. THIERRY HENRY - HAT-TRICK 2**

Gwiji wa Arsenal, Thierry Henry anachukuliwa na watu wengi kama mmoja wa washambuliaji bora kabisa kuwahi kushiriki kwenye Ligi Kuu England. Mfaransa huyo aliyestaafu, alifunga hat-trick mbili katika msimu mmoja wa ligi mara tatu mfululizo.

Henry aliandikisha hat-trick nyingi za ligi kwa mara ya kwanza msimu wa 2003-04 wakati Arsenal ikishinda taji bila kupoteza mchezo hata mmoja (ushindi 26 na sare 12). Hat-trick zake alifunga katika ushindi wa 4-2 dhidi ya Liverpool na ushindi wa 5-0 dhidi ya Leeds United. Mfaransa huyo alifunga mara nne katika mechi dhidi ya Leeds United.

Alirudia kazi hiyo katika misimu ya 2004-05 na 2005-06 kwa 'Washikabunduki' hao.

Kwa ujumla, Henry alifunga mabao 175 ya Ligi Kuu katika mechi 258 alizoichezea Arsenal. Mfaransa huyo alishinda taji la ligi mara mbili, msimu wa 2001-02 na 2003-04.

**#4. SERGIO AGUERO - HAT-TRICK 3**

Sergio Aguero alifurahia kazi yenye mafanikio makubwa pale Manchester City. Baada ya kuwasili kutoka Atletico Madrid mwaka 2011, alijiimarisha kama mmoja wa washambuliaji bora katika soka duniani. Muargentina huyo alifunga hat-trick tatu katika misimu miwili tofauti kwenye Ligi Kuu England.

Aguero alipata hat-trick kwa mara ya kwanza katika msimu mmoja wakati wa msimu wa 2017-18. Hat-trick yake ya kwanza ilikuja katika ushindi wa mabao 6-0 dhidi ya Watford na alirudia ushindi wa 3-1 dhidi ya Newcastle United. Aguero kisha alifunga mara nne wakati timu yake ilipoilaza Leicester City 5-1 wiki moja baadaye.

Alifunga hat-trick tatu katika msimu uliofuata pia, na kuiongoza Manchester City kutwaa ubingwa wa ligi mwishoni mwa kampeni zote mbili.

Kwa ujumla, Aguero alifunga mabao 184 katika mechi 275 za ligi akiwa na City, na kumfanya kuwa mchezaji aliyefunga mabao mengi zaidi ya Ligi Kuu England kwa klabu moja. Pia alifunga bao lililoipa timu hiyo kombe lao la kwanza la ligi mnamo mwaka 2012 na kushinda taji hilo mara tano.

**#3, ERLING HAALAND - HAT-TRICK 3**

Wakati Manchester City ilipomsajili Erling Haaland msimu wa majira ya joto wa 2022, mashabiki wengi wa soka walitabiri wakati mzuri katika klabu kwa kijana huyo.

Nyota huyo wa Norway hajashindwa kuishi kulingana na hali hiyo, na amefunga hat-trick tatu katika mechi nane pekee za Ligi Kuu England akiwa na klabu hiyo.

Haaland alifunga hat-trick yake ya kwanza kwa City katika ushindi wao wa mabao 4-2 dhidi ya Crystal Palace. Mechi yake ya pili ya mabao matatu ilikuja katika ushindi wa timu yake wa 6-0 dhidi ya Nottingham Forest.

Alifunga tena mabao matatu wakati City ikiinyanyasa Manchester United 6-3. Haaland pia alitoa pasi mbili za mabao kwa Phil Foden, ambaye alifunga hat-trick, kwenye mechi dhidi ya 'Mashetani Wekundu' hao.

Haaland sasa amefunga mabao 15 ya ligi kwa Manchester City baada ya mechi tisa pekee. Anashikilia rekodi ya kuwa mchezaji mwenye kasi zaidi kufunga hat-trick tatu katika historia ya mashindano hayo. Raia huyo wa Norway pia ndiye mchezaji wa kwanza kufunga hat-trick tatu mfululizo za Ligi Kuu akiwa nyumbani.

Haaland yuko mbioni kuvunja rekodi ya ufungaji mabao ya mashindano hayo kwa msimu iliyokuwa ikishikiliwa na Mohamed Salah, ambaye aliifungia Liverpool mara 32 katika msimu wa 2017-18.

**#2. HARRY KANE - HAT-TRICK 4**

Harry Kane ni mmoja wa wafungaji bora zaidi katika historia ya Ligi Kuu England kutokana na uchezaji wake katika safu ya ushambuliaji akiwa na Tottenham Hotspur. Kane alifunga hat-trick nne kwa klabu yake msimu wa ligi wa 2016-17.

Mabao matatu yake yote manne kwa Spurs wakati wa msimu huo yalikuja baada ya nusu ya msimu. Mbili zake za kwanza zilikuja katika ushindi wa 4-0 dhidi ya West Bromwich Albion na Stoke City.

Kane kisha alifunga mabao manne kwenye mechi ya mchujo wa mwisho wa msimu huu dhidi ya Leicester City kabla ya kuongeza hat-trick nyingine siku ya mwisho dhidi ya Hull City.

Kwa ujumla, nahodha huyo wa England amefunga mabao 190 katika mechi 290 akiwa na Tottenham Hotspur kwenye Ligi Kuu. Kane ameshinda Kiatu cha Dhahabu cha ligi mara tatu katika maisha yake ya soka hadi sasa na anashika nafasi ya pili katika orodha ya wafungaji wa msimu huu akiwa amefunga mabao nane.

**#1. ALAN SHEARER - HAT-TRICK 5**

Gwiji wa Newcastle United na Blackburn Rovers, Alan Shearer bila shaka ndiye mfungaji bora zaidi katika historia ya Ligi Kuu England.

Miongoni mwa rekodi zake nyingi za kufunga, Shearer alifunga hat-trick nyingi zaidi katika msimu mmoja wa Ligi Kuu England. Mshambuliaji huyo alifunga hat-trick tatu kwa Blackburn katika msimu wa 1995-96.

Shearer alifunga hat-trick yake ya kwanza msimu huo dhidi ya Coventry City kabla ya kufunga bao la pili na la tatu dhidi ya Nottingham Forest na West Ham United. Mwingereza huyo alifunga mabao matatu zaidi kabla ya mwishoni mwa msimu dhidi ya Bolton Wanderers na Tottenham Hotspur.

Kwa ujumla, Shearer alifunga mabao 260 kwenye ligi na kushinda Kiatu cha Dhahabu mara tatu. Alirekodi jumla ya hat-trick 11 katika kipindi chote cha maisha yake ya Ligi Kuu na kushinda taji la ligi hiyo mara moja.

## Nukuu


"Yeye ni mnyama kabisa, ni mzaliwa wa kufunga. Una hisia hiyo, ni nani anayeweza kumzuia mtu huyu? Zaidi ya hayo, huduma anayopata kumzunguka ni ya kipekee, na ndiyo sababu yeye huwa katika hali nzuri kila wakati. Naweza kusema nafasi ya mwili wake daima ni nzuri na iko tayari kufunga," **Kocha wa zamani wa Arsenal, Arsene Wenger akimzungumzia Erling Haaland wa Man City baada ya kufunga hat-trick dhidi ya Manchester United**



"Nadhani kila mtu katika soka anatamani, na hiyo ni kwamba Messi [Lionel], pamoja na kipaji chake chakushangaza na kila kitu alichokifanya katika maisha yake ya soka, kwa jinsi anavyowakilisha soka vizuri, angetamani kushinda Kombe la Dunia kama Diego alivyofanya. Messi anastahili hili zaidi kuliko mtu yeyote. Messi anapaswa kuchukua Kombe la Dunia kutoka Qatar hadi nyumbani kwake," **Kocha wa zamani wa timu ya Taifa ya Marekani na mshindi wa Kombe la Dunia 1990 akiwa na Ujerumani Magharibi, Jürgen Klinsmann**



"Natarajia Salah [Mohamed), ataachwa kikosini hivi karibuni, na simaanishi kuchezeshwa kwa zamu, pia amekuwa mbovu kwa viwango vyake vya juu msimu huu na anajua hilo mwenyewe kushuka kabisa. Jurgen Klopp amebaki naye hadi sasa, lakini nadhani hilo linaweza kubadilika wiki hii," **Mshambuliaji wa zamani wa Leeds United, Noel Whelan**









# SAFU 5 BORA VIUNGO TIMU ZA TAIFA KOMBE LA DUNIA

**LONDON,** England

HATUKO mbali sana na Kombe la Dunia la FIFA la 2022 kwa sasa. Timu za kimataifa ambazo zimefuzu Kombe la Dunia la FIFA la 2022 zote zinajiandaa kikamilifu kwa mashindano hayo.

**Wote wanajaribu michanganyiko tofauti ya vikosi vyao hivi sasa. Wanatumaini kutengeneza mipango itakayowasaidia kucheza kwa uwezo wao wote kwenye Kombe la Dunia.**

Safu ya kiungo ndio uti wa mgongo wa timu yoyote na kadri safu ya kiungo inavyoimarika ndivyo uwezekano wa kutawala mchezo unavyoongezeka. Kabla ya Kombe la Dunia la FIFA la 2022, hebu tuangalie safu bora tano ya viungo kwa timu za taifa.

**#5. ENGLAND**

England wamejiimarisha kama kikosi kinachopewa nafasi kubwa kwenye michuano ya kimataifa katika siku za hivi karibuni. Mbio zao hadi nusu fainali ya Kombe la Dunia la FIFA la 2018 na fainali ya Euro 2020, zinasisitiza jambo hili. 'Simba Watatu' hao wanaonekana kuwa timu ngumu na wana kikosi cha kutisha pia.

Safu yao ya kiungo inaonekana sawia kabisa. Ni safu ya kiungo changa na ikiwa kila kitu kitapangwa, vijana hao wa kocha, Gareth Southgate wanapaswa kuwa na mbio nzuri kwenye Kombe la Dunia.

Wana Kalvin Phillips na Declan Rice katika safu ya kiungo ya ulinzi. Jude Bellingham, Mason Mount, Conor Gallagher na James Ward-Prowse ni viungo wengine waliofanikiwa kwenye kikosi hicho.

Kuna ubunifu na ukakamavu mwingi katika kundi hilo na wanapaswa kuwa na uwezo wa kujizuia dhidi ya baadhi ya timu zilizo bora zaidi kwenye michuano hiyo.


**#4. BRAZIL**

Idara ya ushambuliaji ya Brazil inaonekana kutisha kuelekea Kombe la Dunia. Wana washambuliaji wa kiwango cha kimataifa katika safu zao kama Neymar Jr, Vinicius Jr na Rodrygo. Kuna Antony, Richarlison, Roberto Firmino na Matheus Cunha, wote ni chaguzi za kuaminika pia.

Viungo wao wa kati wamefanya kazi nzuri sana siku za hivi karibuni. Wapo Casemiro na Fabinho, Brazil wana viungo wawili wa ulinzi wa kiwango cha daraja la kwanza. Fred amethibitika kuwa mahiri kama namba sita huku, Lucas Paqueta, Bruno Guimaraes na Everton Ribeiro wakiweza kuongeza ubunifu mkubwa.

**#3. UJERUMANI**

Baada ya kuondolewa hatua ya




makundi katika Kombe la Dunia la 2018, Ujerumani itakuwa ikitafuta kujikomboa wakati huu. Bila shaka wana wachezaji ambao wanaweza kuwafikisha kwenye mstari wa kumaliza na ni mojawapo ya timu inayopewa nafasi kubwa zaidi wakati huu.

Wana viungo wa kiwango cha dunia katika safu zao hivi sasa. Joshua Kimmich anacheza katika kilele cha nguvu zake na mshirika wake wa kiungo wa Bayern Munich, Leon Goretzka huenda akafanya kazi pamoja naye.

Ilkay Gundogan bado ni kiungo mwingine wa ubora wa juu ambaye Hansi Flick anaweza kutegemea kuzalisha jambo zuri kwenye Kombe la Dunia. Zaidi ya hayo, wana kiungo mkabaji kutoka Borussia Monchengladbach, Jonas Hoffman na Jamal Musiala.

**#2. URENO**

Ureno ina wachezaji wengi wa kiwango cha juu katika safu zao kwa sasa na wanapendekezwa kuwa na mbio ndefu kwenye Kombe la Dunia. Ureno imetoa baadhi ya mafundi wakubwa katika historia ya soka na hata sasa hawako tofauti sana.

Ruben Neves, Joao Palhinha, Danilo, Matheus Nunes na William Carvalho wote ni chaguo la kuaminika katika safu ya ulinzi. Pia wana Vitinha na amekuwa katika hali nzuri kwa Paris Saint-Germain katika hatua za mwanzo za msimu mpya.

Zaidi ya hayo, Ureno ina Bruno Fernandes, Bernardo Silva, Renato Sanches na Joao Mario. Kocha Fernando Santos atakuwa na maumivu ya kichwa katika uteuzi, lakini tuna uhakika hatajali hilo.

**#1. HISPANIA**

Hispania ni nyumbani kwa baadhi ya viungo wakubwa wa zama za kisasa. Baada ya kutinga nusu fainali ya Euro 2020, mambo makubwa yanatarajiwa kwa Hispania kwenye Kombe la Dunia. Furaha nyingi katika timu zimejengwa kwa ubora kamili wa safu yao ya kiungo.

Sergio Busquets anaweza kuwa amepita kiwango chake, lakini bado ni mmoja wa viungo bora zaidi wa ulinzi duniani. Rodri ni chaguo jingine la kiwango cha kimataifa katika nafasi sawa. Thiago Alcantara huenda akarejea kikosini na mchezaji huyo wa Liverpool ni mmoja wa wachezaji bora kabisa barani Ulaya kwa sasa.

Pia wana wachezaji wawili wa safu ya kati wenye vipaji vya hali ya juu kama Pedri na Gavi katika safu ya kati. Marcos Llorente ni mchezaji hodari ambaye anaweza kutumwa katika nafasi mbalimbali, lakini kimsingi ni kiungo. Koke, Mikel Merino na Carlos Soler pia ni chaguzi ambazo kocha Luis Enrique anaweza kuzitegemea.

NDANI YA 18



MSHAMBULIAJI wa Arsenal, Gabriel Jesus amekamilisha nafasi nane ndani ya boksi la wapinzani kwa kuzitumia vema kufunga, zikiwa ni nyingi zaidi ya mchezaji mwingine yeyote katika Ligi Kuu ya tano bora Ulaya pamoja na michuano ya Uefa msimu huu.

# SOKA





**MKALI WA WIKI**

**JINA KAMILI:** Robert Lewandowski
**KUZALIWA:** Agosti 21, 1988 (miaka 34)
**ALIPOZALIWA:** Warsaw, Poland
**KIMO:** 1.85 m (6 ft 1 in)
**NAFASI:** Straika
**KLABU:** Barcelona
**NAMBA:** 9
**MABAO:** 9 (Kinara LaLiga)

LIGI Kuu England (EPL), inachukuliwa kuwa ngumu zaidi kucheza kwa sababu ya kiwango cha timu na wachezaji kwenye mashindano hayo.

Uk. 16-17




# SABABU TANO YANGA KUTOSHINDA KWA MKAPA

**Na Adam Fungamwango**

MABINGWA wa Tanzania Bara Yanga, juzi walishindwa kupata ushindi kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa dhidi ya wageni wao, Al Hilal ya Sudan ambao ungeweza kuirahisishia kazi ikienda kucheza ugenini.

**Badala yake ililazimishwa sare ya bao 1-1 nyumbani na kujipa kazi ya ziada itakapokwenda kucheza mechi ya mkondo wa pili ya raundi ya Kwanza Ligi ya Mabingwa Afrika Oktoba 16, mwaka huu jijini Khatoum nchini Sudan.**

Ilikuwa ni mechi ambayo timu ziligawana vipindi, Yanga ikitawala cha kwanza, lakini Al Hilal iligeuka mbogo kipindi cha pili kwa kufanya mashambulizi ya kushtukiza kwa kutumia mipira mirefu ambayo yalikuwa ya hatari sana.

Kipa Djigui Diarra wa Yanga alifanya kazi ya ziada baada ya kudaka mara mbili mipira ikiwa miguuni mwa washambulizji wa Al Hilal kwenye dakika nne za nyongeza na kuiokoa timu yake kuadhirika nyumbani.

Fiston Mayele ambaye alifunga bao la Yanga kwenye mechi hiyo, alikosa mabao mawili ya wazi ambayo yangekuwa yameitanguliza timu hiyo mpaka sasa na kuwapa kibarua wenyeji kwenye mechi ya marudiano.

Katika makala haya tumekuorodheshea sababu tano ambazo ziliifanya Yanga kushindwa kupata matokeo nyumbani, 'kwa Mkapa.'

**#1. NABI KUTOIFAHAMU VEMA AL HILAL**

Kwa kauli yake mwenyewe Kocha wa Yanga, Nasreddine Nabi alisema hakuwafahamu vema wapinzani wake, hivyo alikuwa hajui uzuri zao na mapungufu yao.

Ni kwa sababu hakuwahi kwenda kuitazama timu hiyo hata mechi moja, lakini pia Al Hilal walizuia mechi yao ya nyumbani kuonyeshwa kwenye televisheni dhidi ya St. George ya Ethiopia walipocheza kwenye mechi ya hatua za awali.

Pamoja na kwamba Nabi anaifahamu timu hiyo kutokana na kuwahi kuifundisha msimu wa 2013-2014 na baadaye akawanoa wapinzani wa Al Hilal, Al Merrikh, lakini kwa sasa Al Hilal ina kocha mpya Florent Ibenge na wachezaji wengi wapya waliowasajili msimu huu.

Kutokana na kutoifahamu vema, Nabi alishindwa kupanga mpango mkakati wa kukabiliana na timu hiyo, asijue nani wa kumkaba, nani hatari na wa kuchungwa.

**#2. IBENGE KUWAFAHAMU WACHEZAJI YANGA**

Kinyume chake ni kwamba Kocha wa Al Hilal, Mkongomani Florent Ibenge anawafahamu vizuri wachezaji wa Kikongomani waliokuwa Yanga kwa sababu aliwafundisha akiwa nao AS Vita Club ya Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo pamoja na timu ya taifa ya nchi hiyo.

Aliwafahamu uzuri wao na mapungufu yao. Aliweza kuwatuma kazi vijana wake jinsi ya 'kudili' na wachezaji hao ambao wengi wao ndiyo tegemeo kwenye kikosi hicho.

Wachezaji hao ni Mayele, Djuma Shaaban, Jesus Moloko, Yanick Bangala, Tuisila Kisinda aliyeingia kipindi cha pili na hata Joyce Lomalisa ambaye hakucheza kwenye mechi hiyo.

Straika wa Yanga, Fiston Mayele, akijaribu kumtoka beki wa Al Hilal ya Sudan, Imoro Ibrahim kwenye pambano la raundi ya kwanza ya Ligi ya Mabingwa Afrika iliyochezwa juzi Uwanja wa Benjamin Mkapa, timu hizo zikitoka sare ya bao 1-1.

**#3. KUSHINDWA KUFUNGA KIPINDI CHA KWANZA**

Tangu msimu uanze, Yanga imekuwa ikicheza vema zaidi kipindi cha pili na kupata mabao. Hiyo imeonekana kwenye mechi za Ligi Kuu na mchezo wa awali wa Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Zalan FC ya Sudan Kusini.

Lakini kwenye mechi ya Jumamosi ilimiliki zaidi mpira kipindi cha kwanza ambacho wapinzani wao ni kama vile walicheza kwa kuzuia zaidi na tahadhari sana kiasi cha kutofanya shambulizi lolote lile kwa dakika zote 45.

Ni kipindi ambacho wachezaji wa Yanga walikaa sana na mpira, lakini walionekana kuutembeza zaidi mpira kuliko wao kutembea.

Inawezekana walitembea na historia yao kichwani, hivyo walishindwa kutumia nafasi kadhaa walizozipata 'kuiua' mechi, walitegemea kipindi cha pili, lakini hali ikawa kinyume kidogo, na hasa baada ya kupata bao dakika ya 50.

**#4. 'SUB' YA AL HILAL ILIWAVURUGA**

Baada ya Yanga kupata bao,

Ibenge aliona kama hana cha kupoteza bali kufunguka, ndipo alipowaingiza wachezaji ambao walienda kubadilisha taswira nzima ya mechi hiyo.

Aliwatoa Mwafag Siddi, Abdul Ajagun na John Robia na kuwaingiza wachezaji walioonekana kuwa hatari, Abdei Raouf, Wallieldin Khedr, Mohamed Yousif, halafu akamwingiza 'kiberenge' Yasir Muzamir.

Wachezaji wa Yanga walishindwa kunusa hatari hasusan mabeki kwani walionekana kupanda kusaidia wenzao kutafuta bao la pili, likawa kosa.

Mipira mirefu iliyokuwa ikipigwa kwa Muzamir ilionekana hatari, kwani dakika 17 baada ya Yanga kupata bao, Al Hilal ilisawazisha, baada ya winga huyo wa kulia, kumuacha Kibwana Shomari na kupiga krosi iliyomkuta mchezaji mwenzake aliyeingia naye kipindi cha pili, Yousif, akaukwamisha wavuni.

Kuanzia dakika hiyo hadi mwisho wa mchezo, ni Al Hilal ambao walifanya mashambulizi ya hatari zaidi langoni kwa Yanga, ambayo yalikaribia kuwa mabao kuliko wenyeji.

**#5. MORRISON HATARI, LAKINI HAKABI**

Kibwana alikutana na dhahama kufungashwa tela kila mara kutokana Bernard Morrison kushindwa kushuka kumsaidia kukaba.

Morrison ambaye alikuwa na mchezo bora sana hasa kipindi cha kwanza akimsumbua sana beki Mwafag na kupiga krosi za hatari, alikuwa hashuki chini kumsaidia mwenzake, hivyo kuwa na wakati mgumu wa kukabiliana na mawinga hatari wa wageni, mwanzo akipatishwa tabu na Salah Adil, kabla la Muzamir naye kuja kumalizia kazi.

Wachezaji kama Feisal Salum na Stephane Aziz Ki, hawakuwa kwenye kiwango chao kilichozoeleka, huku Dickson Job aliyefanya kosa lililosababisha bao akiokoa mpira uliokuwa ukitinga wavuni, Djuma, Bangala na Diarra wakiwa kwenye viwango bora kabisa kwenye mechi hiyo.

**JE, WAJUA?**



FOLARIN Balogun amefunga mabao sita akiwa na Reims kwenye Ligue 1 msimu huu wa 2022-23, yakiwa ni mengi zaidi ya mchezaji yeyote aliyezaliwa karne ya 21 kwenye Ligi tano bora Ulaya msimu huu.



## Polisi yatangaza msako kwa wasiosalimisha silaha

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

JESHI la Polisi mkoani Mbeya limetangaza kuanza msako wa kuwakamata watu ambao hawajasalimisha silaha zao katika kipindi ambacho jeshi hilo lilitoa muda wa usalimishaji wa hiari wa silaha.

Oktoba 31, mwaka huu, ndiyo mwisho wa kipindi cha kusalimisha silaha kwa hiari kilichotangazwa na serikali na baada ya hapo, msako utaanza kuwabaini watakaokiuka agizo hilo linalolenga kulinda usalama wa rai na mali zao.

Septemba 5, 2022 Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani na Nchi, Jumanne Sagini, alizindua rasmi kampeni hiyo kwa lengo la kuwahamasisha wananchi kusalimisha silaha zao kwa hiari.

"Alisema kampeni hiyo inamtaka mwananchi yeyote ambaye anamiliki silaha kinyume cha sheria, kusalimisha silaha yake au zake kwa hiari katika ofisi za serikali ngazi ya mtaa au kijiji au kituo chochote cha polisi kilicho karibu naye," alisema Sagini.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mbeya, Benjamin Kuzaga, aliwahamasisha wananchi kushiriki kampeni hiyo kikamilifu kwa kusalimisha silaha zao kwa hiari kabla sheria haijaanza kuchukua mkondo wake.

"Baada ya kampeni hii kumalizika, polisi tutaanza operesheni maalum ya kichwa kwa kichwa, nyumba kwa nyumba na mtaa kwa mtaa ili kuwabaini na kuwachukulia hatua za kisheria wale wote watakaobainika kukaidi kampeni hii na kuendelea kumiliki silaha kinyume cha sheria kupitia kauli mbiu yetu ya 'silaha haramu sasa basi, salimisha kwa hiari,'" alisema Kuzaga.

# Mbaroni kwa tuhuma za kumng'ata masikio mkewe

**Na Grace Mwakalinga,** SONGWE

JESHI la Polisi Mkoa wa Songwe linamshikilia Nadi Said (60), mkazi wa Kijiji cha Namkukwe wilayani Songwe kwa tuhuma za kumng'ata masikio mke wake, Paulina Adam (20) aliyekuwa amemshika sehemu za siri baada ya kutokea ugomvi kati yao.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Songwe, Alex Mkama, jana alithibitisha kutokea kwa tukio hilo na uchunguzi wao umebaini mwanamume alikuwa akimlalamikia mkewe kuuza mahindi (ndoo moja ya plastiki) bila ruhusa ndipo ugomvi ukaanza.

Alisema ugomvi huo ulisababisha Paulina kumshika sehemu za siri mume wake na katika kujinasua, mwanamume akamng'ata masikio ndipo akaachiliwa.

Mkama alisema Paulina alipelekwa kituo cha afya kupata matibabu na baada ya afya yake kuimarika alirejea nyumbani ndipo mumewe alikamatwa na kupelekwa kituo cha polisi kwa ajili ya hatua zaidi za kisheria.

Mwenyekiti wa Kijiji hicho, Geofrey Lyanda, alidai ndoa hiyo imekuwa na mgogoro wa muda mrefu na wamekuwa wakituhumiana kuwa na 'michepuko'.

Mke wa Said, Paulina, alidai kuwa kwa muda mrefu mumewe amekuwa akimtuhumu kuwa na uhusiano na wanaume wengine, akikana tuhuma hizo.

Alisema maneno ya watu yamechangia kwa kiasi kikubwa ndoa yake kuwa na migogoro na ugomvi wa mara kwa mara, akikiri kupata majeraha kutokana na ugomvi huo.

"Mara nyingi mume wangu amekuwa akinituhumu kwamba ninachepuka, jambo ambalo sio kweli, amekuwa akisikiliza maneno ya watu na matokeo yake ndiyo haya amenisababishia majeraha kwenye masikio yangu. Kuhusu suala la mahindi kuwa chanzo cha ugomvi wetu, siyo kweli," Paulina alidai.

Baba wa Paulina, Adam Siame, alidai mwanawe huyo amekuwa akipata mateso kwenye ndoa yake tangu alipoolewa.

Kutokana na tukio hilo aliviomba vyombo vya sheria kutenda haki ili Said na wanaume wengine wajifunze kutonyanyasa wanawake.



Katibu Mkuu wa TAMISEMI, Prof. Riziki Shemdoe (kushoto), akipewa ufafanuzi wa miradi mbalimbali inayojengwa jijini Mbeya na Mbunge wa Jimbo la Mbeya Mjini, Dk. Tulia Akson ambaye ni Spika wa Bunge, mwishoni mwa wiki. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# Mamlaka kuboresha utoaji huduma ya maji

**Na Mwandishi Wetu,** MBEYA

MAMLAKA ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mbeya (MBEYA-WSSA) imesema inaendelea kuboresha na kuongeza wigo wa upatikanaji wa huduma jijini Mbeya na Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mbalizi ili kuwasaidia wakazi wa maeneo hayo kufanya shughuli za uzalishaji mali bila vikwazo. Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka hiyo, Gilbert Kayange, alisema jana kuwa mamlaka hiyo imepewa dhamana ya kuhakikisha huduma ya maji inapatikana wakati wote.

Katika kuhakikisha hilo linafanikiwa, Kayange alisema mamlaka hiyo inaendelea na utekelezaji wa ujenzi wa miradi kama vile wa Ilunga ambao utatoa huduma kwa wakazi wa Mji ya Mbalizi na Iwambi.

Alisema mradi huo wa Ilunga tayari umeanza kutoa huduma, akibainisha kuwa kwa siku huzalisha maji lita milioni 11 na miradi mingine inayoendelea kujengwa ni pamoja na Itagano, Halinji na Mto Simba. "Kwa sasa Mamlaka ya Maji Mbeya inazalisha lita milioni 66.5 kwa siku wakati mahitaji yakiwa ni lita milioni 90, hivyo ili wananchi wapate huduma hiyo, tunaendelea na ujenzi wa miundombinu ya maji maeneo mbalimbali," alisema Kayange.

Diwani wa Mwakibete, Lucas Mwampiki, alisema nyakati za kiangazi upatikanaji wa maji siyo wa uhakika, hali inayosababisha baadhi ya shughuli kukwama.

Alisema licha ya Mkoa wa Mbeya kubarikiwa kuwa na vyanzo vingi vya maji, upatikanaji wa maji siyo wa uhakika, hivyo aliiomba Mamlaka ya Maji kuhakikisha maji, hasa nyakati za kiangazi, hayasumbui kwa kuwa vyanzo vya kutosha vipo.

Kuanzia mwezi wa nane (Agosti) hadi Desemba, huduma ya maji hapa jijini Mbeya husumbua, unashangaa maji yanakatika hata siku nne, watu wanalazimika kutumia maji ya mitaroni ambayo siyo safi wala salama. Tunaomba jambo hili tusaidiwe," alisema Mwampiki.

Baadhi ya wajasiriamali wanawake wanaofanya shughuli zao eneo la Soweto jijini Mbeya, walisema miongoni mwa sababu zinazochangia huduma ya maji kusuasua ni umeme kukatika mara kwa mara.

Bupe Abraham, mmoja wa wajasiriamali hao, alisema licha ya kwamba serikali haijatangaza mgawo wa umeme, kwa sasa huduma hiyo siyo ya uhakika, hali inayochangia upatikanaji wa maji kuwa mgumu na kuathiri shughuli zao.



# Ukosefu wa tiba shufaa unavyowaua mamilioni

**Na Renatha Msungu,**
DODOMA

TAKRIBANI watu milioni 18 hufariki dunia kila mwaka ulimwenguni kote kutokana na maumivu na mateso ya kukosa huduma ya udhibiti wa maumivu hayo.

Vilevile, imebainishwa kuwa hali hiyo iko kwa asilimia 83 kwa watu wazima na asilimia 98 kwa watoto.

Mkurugenzi wa Tiba wa Wizara ya Afya, Prof. Paschal Lugajo, alibainisha hayo juzi kwa niaba ya Mganga Mkuu wa Serikali kwenye kilele cha Siku ya Tiba Shufaa Duniani ambayo huadhimishwa kila mwaka Oktoba 8.

Prof. Lugajo alisema hali hiyo imekuwa inachangiwa na kukosekana kwa vituo vichache vyenye wataalamu wa huduma hizo za tiba shufaa pamoja na uelewa mdogo wa jamii kuhusu huduma hizo.

Hata hivyo, alisema kutokana na kuwapo kwa tatizo hilo, Wizara ya Afya ipo katika mchakato wa kuandaa mitaala ya mafunzo ya tiba shufaa kutokana na watu kupata msongo wa mawazo pale wanapoondokewa na ndugu zao, hasa wenza na hupelekea kujidhuru.


Alisema serikali itaendelea kushirikiana na wadau mbalimbali wakiwamo wataalamu wa huduma za afya, viongozi wa madhehebu ya dini na taasisi za kijamii ili kuponya mioyo na jamii.

Alifafanua zaidi ya kuwa serikali inatambua kifo na huzuni havitenganishwi na kwamba huduma za tiba shufaa zinajumuisha kuwasaidia wale wote wenye huzuni itokanayo na kufiwa na mpendwa wao baada ya kumuuguza kwa muda mrefu bila kujali umri wake.

Mkurugenzi huyo alisema kwa juma la kwanza la mwezi Oktoba 2022, timu za wataalamu wa Huduma za Tiba Shufaa zimekuwa zikitoa huduma hizo katika vituo mbalimbali vya huduma za afya pamoja na kutoa elimu kupitia vyombo vya habari.

"Ninaamini kuwa uhamasishaji uliofanywa katika juma hili umeweza kuongeza ufahamu kwa jamii iliyopata huduma hizi ambazo ni sehemu ya haki ya afya kwa wananchi, falsafa ambayo itaisaidia jamii kupunguza mateso yatokanayo na kuguza," alisema.

Aliongeza kuwa shughuli zilizofanyika katika maadhimisho hayo ni pamoja na uelimishaji jamii juu ya maumivu sugu, kliniki tembezi, uchunguzi wa magonjwa yasiyoambukiza ikiwamo msaada wa kitaalamu kwa watu wenye majonzi na waliopatwa na misiba kwa kuwapa nasaha na ushauri.



Wanafunzi wa Shule ya Msingi El Shadai, waliohitimu darasa la saba wakielezea jinsi walivyojifunza kuhusu mfumo wa moyo unavyofanyakazi kwenye mwili wa binadamu kwenye mahafali yaliyofanyika mwisho wa wiki, Ihumwa, jijini Dodoma. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Waomba kuteta na Samia vikwazo kupata mikopo

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

CHAMA cha Wafanyabiashara Wenye Viwanda na Wakulima Tanzania (TCCIA) Mkoa wa Dodoma kimeomba kukutana na Rais Samia Suluhu Hassan ili kumweleza vikwazo wanavyokabiliana navyo kupata mikopo ya kilimo.

Mwenyekiti wa TCCIA mkoani hapo, Khamis Fungameza, alibainisha hayo jana jijini hapo alipozungumza na wajumbe wa chama hicho.

Alisema kuwa pamoja na jitihada zinazofanywa na serikali kukwamua wakulima kwa kuongeza bajeti katika sekta hiyo, wanakabiliwa na vikwazo vingi kupata mikopo ya kilimo.

Fungameza alisema kila mara wamekuwa wakifanya vikao pamoja na taasisi za kifedha na kuahidiwa kupatiwa mikopo kwa ajili ya kilimo, lakini hakuna hata mmoja wao ambaye amebahatika kupata mkopo.

"Mwaka jana tulikaa hapa na taasisi za kifedha pamoja na aliyekuwa Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Anthony Mtaka na tulihamasisha wakulima wakajitokeza kwa wingi na kuandaa mashamba, lakini hakuna hata mmoja aliyepatiwa fedha," alisema.

Kutokana na hali hiyo, Fungameza alisema umefika wakati sasa wa kukutana na Rais Samia ili kumweleza kero wanayoipata kutoka sekta za kifedha kila wanapohitaji kupata mikopo.

"Umefika wakati sasa kumweleza Rais kuwa ile mikopo ambayo serikali imekuwa ikisema kuwa ni kwa ajili ya wakulima, sisi hatuipati pamoja na uhitaji tulionao. Sasa ni wakati wa kuelekea kilimo lakini hakuna hata mmoja wetu ambaye amepata mkopo wa kilimo.

"Tunamwomba Rais hizi benki ambazo amezikabidhi jukumu la kutupatia mikopo ya kilimo, hazina uwezo, watu wake ni wabinafsi, atuletee benki zingine," alilalamika.

Vilevile, Fungameza alisema wanaiomba serikali kuangalia upya masharti ya taasisi za fedha kwa wakulima kupatiwa mikopo.

"Hivi sasa kwa namna ilivyo wakulima karibu wote hatuna sifa ya kukopesha kutokana na masharti yaliyoko kwenye taasisi za fedha. Kwanini kitambulisho cha taifa kisitumike kama dhamana badala ya hati za nyumba pamoja na mambo mengine magumu yanayotumika sasa kama dhamana?" Alihoji.

Akifungua kikao hicho, Naibu Waziri wa Kilimo, Antony Mavunde, alisema serikali inaendelea na jitihada katika kuboresha sekta ya kilimo.

Alisema kwa sasa wako katika mchakato wa kuboresha miundombinu ya umwagiliaji kwa kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwenye mabonde yote nchini.

"Wakulima sasa lazima wasiwe wanategemea mvua pekee yake kwa ajili ya kilimo, lazima walime hata mara mbili kwa mwaka na hii itawezekana tu kama tutawekeza kwenye kilimo cha umwagiliaji," alisema.

Mavunde alizitaka taasisi za kifedha kutumia mikataba ya wakulima na kampuni zinazonunua mazao ya wakulima kama dhamana ya kuwapatia mikopo ya kilimo badala ya kuweka masharti magumu yanayolalamikiwa na TCCIA Mkoa wa Dodoma.

# Kamati za Bunge zaanza kuchambua ripoti ya CAG

**Na Augusta Njoji,**
DODOMA

KAMATI za Bunge zinazosimamia matumizi ya fedha za umma na uwekezaji wa mitaji ya umma leo zinaanza vikao vyake kwa ajili ya kuchambua taarifa ya ukaguzi wa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwa mwaka 2020/21.

Kamati hizo ni za Hesabu za Serikali (PAC), Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC) na Uwekezaji wa Mitaji ya Umma (PIC).

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Ofisi ya Bunge mwishoni mwa wiki, LAAC na PAC zitashughulikia maeneo yenye matumizi mabaya ya fedha za umma huku PIC ikipokea na kuchambua taarifa za uwekezaji wa mitaji ya umma ili kubaini iwapo uwekezaji huo una ufanisi na kama umezingatia taratibu na miongozo mujarabu ya biashara.

Ratiba ya vikao vya PAC inaonyesha itaanza kwa kupitia taarifa ya ukaguzi wa ufanisi kuhusu usimamizi wa mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu na hesabu za Shirika la Madini la Taifa (STAMICO).

Ratiba hiyo inaonyesha Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI pia itaanza vikao vyake keshokutwa ili kujadili afua za masuala hayo.

Kwa mujibu wa ratiba hiyo, kamati zingine zitaanza kukutana Oktoba 17 hadi 28 mwaka huu ikiwamo Kamati ya Bunge ya Bajeti ambayo imepanga kujadili Mapendekezo ya Mpango wa Taifa unaokusudiwa kutekelezwa na serikali kwa mwaka wa fedha 2023/24.

Shughuli hizo, pamoja na mambo mengine, zinatarajiwa kuwezesha kamati kuandaa taarifa zitakazowasilishwa bungeni wakati wa vikao vya Mkutano wa Tisa wa Bunge la 12 utakaoanza Novemba Mosi mwaka huu.

Pamoja na hayo, miswada minne ya sheria iliyosomwa mara ya kwanza wakati wa mkutano uliopita, inatarajiwa kujadiliwa wakati wa vikao vya mkutano huo wa Bunge.





## Mufti ataja sababu za wimbi la talaka

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MUFTI wa Zanzibar, Shekhe Saleh Kabi, amewataka makadhi wanaofungisha ndoa, kuhakikisha wanafuata misingi na sheria za dini ya Kiislamu ili kuziweka ndoa katika misingi imara na kudumu.

Shekhe Kabi aliagiza hayo jana wakati wa mkutano uliowakutanisha makadhi wanaofungisha ndoa kwa ajili ya majadiliano na kuweka mikakati imara kuhakikisha sheria za ndoa zinafuatwa na kuepukana na wimbi la talaka.

Alisema jukumu la kufungisha ndoa ni kubwa ambalo watu waliopewa kazi hiyo wanatakiwa kuifanya kwa kuzingatia sifa, uwezo na sheria zinazoongoza ndoa.

Alisema jamii inashuhudia kuwapo wimbi kubwa la kuvunjika kwa ndoa ambazo utafiti wake unaonyesha kukosekana kwa misingi ya ndoa hizo katika ngazi za awali.

Aliitaja baadhi ya misingi ya ndoa ni kupatikana kwa idhini ya wazazi wawili, akibainisha kuwa katika siku za karibuni ndoa zimekuwa zikifungwa bila ridhaa hiyo.

"Makadhi ambao wamepewa jukumu la kufungisha ndoa, wanatakiwa kufuata masharti ya ndoa ambayo ni kupatikana kwa idhini kutoka kwa wazazi wote," aliagiza.

Naibu Mufti, Sheikh Mahmoud Mussa aliwataka makadhi wanaofungisha ndoa, kutoa elimu kwa wazee wanaodai mahari ya vifaa (samani za ndani) kutokana na baadhi ya wanaume kudai vifaa vyao baada ya kutalakiana ili wavitumie kama mahari kupata mke mwingine.

"Mahari ni haki ya mwanamke na yule anayepewa vitu huwa ni mali yake, lakini kumejitokeza baadhi ya vijana kudai vitu hivyo na kuvitumiya kuolea wake wengine, jambo ambalo halikubaliki," alionya.

Mkurugenzi wa Idara ya Fatwa, Sheikh Khamis Gharib, aliwataka makadhi hao kufungisha ndoa kwa kuzingatia misingi ya dini ya Kiislamu na kuwataka wanandoa kujenga tabia ya kuvumiliana katika ndoa.

Alisema msingi muhimu wa kuifanya ndoa kudumu kwa muda mrefu ni kujenga tabia ya kuvumiliana kwa wanandoa kwa kuwa watu wawili wanapoishi pamoja hawakosi kukoseana.

Aliwataka wazee kuwa karibu na wanandoa hao na kuwa tayari kuzipatia ufumbuzi kesi za ndoa zinazofikishwa kwao kwa kuhusisha pande mbili bila ya kufanya upendeleo.

# Mradi mpya kuondoa malaria waiva ukigharimu dola mil. 27

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

ZANZIBAR imezindua mradi mpya wa miaka mitano wa kuondoa malaria utakaogharimu dola za Marekani milioni 27 ili kudhibiti ugonjwa huo ambao husababisha vifo.

Akizindua mradi huo jana katika Hoteli ya Golden Tulip mjini Zanzibar, Waziri wa Afya, Nassor Ahmed Mazrui, alisema jitihada za Mfuko wa Rais wa Marekani wa Kupambana na Malaria (PMI) zimechangia kupunguza kasi ya maambukizi ya malaria Zanzibar kutoka zaidi ya asilimia 30 mwaka 2005 hadi kiwango cha sasa cha chini ya asilimia moja.

Alisema mradi huo wa miaka mitano utaondoa kabisa malaria Zanzibar kutoka asilimia moja ya sasa hadi asilimia sifuri na kudhibiti ugonjwa huo na kuwa ukanda huru.

Alisema katika kipindi cha miaka 16, Wizara ya Afya imenufaika na msaada wa PMI katika safari ya kutokomeza malaria nchini.

Mazrui alisema PMI kupitia Shirika la Misaada la Marekani (USAID) wamesaidia hatua zilizothibitishwa za kutokomeza malaria kama vile utambuzi na matibabu ya malaria, udhibiti jumuishi wa vimelea vya malaria na ufuatiliaji na tathmini juu ya ugonjwa huo.

"Katika kipindi cha miaka mitano iliyopita, PMI kupitia Shirika la Okoa Maisha Dhibiti Malaria (OMDM), ilichangia zaidi ya dola milioni 19.3 kwa Serikali ya Tanzania kusaidia juhudi za kutokomeza malaria kwa Tanzania Bara na Zanzibar," alisema Mazrui.

Waziri huyo alisema kuwa kupitia OMDM, kumekuwa na baadhi ya maboresho ya mapambano dhidi ya malaria ikiwamo ufuatiliaji na tathmini ikiwa ni pamoja na kuimarishwa kwa kiwango cha uchunguzi wa kesi, kuweka mikakati ya kuondoa hatari ya malaria Zanzibar, kuunganishwa kwa mfumo wa taarifa za kesi za malaria na DHIS2 na uimarishaji wa ufuatiliaji wa vimelea.

Alielezea matumaini yake mradi mpya wa PMI TMCM ni mwendelezo wa juhudi za kusaidia kutokomeza malaria Zanzibar.

Mkurugenzi Msaidizi Idara ya Afya USAID, Anna Hoffman, alisema kuwa kupitia ushirikiano wa karibu na wananchi, taasisi na Serikali ya Zanzibar na Serikali ya Marekani, wamejitolea kufuata kiwango sawa cha ushirikiano na taasisi ya kudhibiti malaria Zanzibar (ZAMEP) na asasi za kiraia kusonga mbele kuimarisha mifumo ya afya ili kuimarisha na kuongeza juhudi za Tanzania kukabiliana na ugonjwa huo.

Alisema USAID inajivunia kuwa sehemu ya mafanikio hayo aliyoyaita ya ajabu, lengo likiwa kukomesha malaria.

Alisema kuwa kupitia OMDM, viwango vya uchunguzi wa kesi za malaria viliongezeka kutoka chini ya asilimia 50 mwaka 2018 hadi zaidi ya asilimia 95 mwaka 2022, ikiwa na maana kwamba watu wengi zaidi wanapimwa na kutibiwa malaria na kulindwa dhidi ya maambukizi ya baadaye, hatua muhimu zinazowasogeza karibu na kufikia kutokomeza malaria.

Meneja wa Mradi wa Kumaliza Malaria Zanzibar, Mohammed Ali alisema kuwa kupitia mradi mpya, matarajio yao ni kwamba Zanzibar inaweza kufikia lengo la kuwa na asilimia sifuri ya malaria nchini.

Alisema kuwa ingawa kuna vikwazo vingi katika kukabiliana na tatizo hilo, watahakikisha wanapambano navyo na kuondosha malaria Zanzibar.




Waziri wa Afya, Nassor Ahmed Mazrui, akizungumza na waandishi wa habari jana Mjini Zanzibar baada ya kuzindua mradi mpya wa miaka mitano wa kutokomeza malaria. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Mwinyi amulika mapato kushirikiana na India

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amesema serikali inakusudia kuangalia maeneo ya kuingiza vipato kupitia ushirikiano kati ya wafanyabiashara wa India na Zanzibar.

Dk. Mwinyi alibainisha hayo juzi Ikulu mjini Zanzibar alipozungumza na ujumbe wa ngazi za juu kutoka Wizara ya Mambo ya Nje ya India ulioongozwa na Katibu Mkuu wa Idara ya Ushirikiano kati ya India na Bara la Afrika, Dammu Ravi.

Alisema serikali itaangalia kwa kina maeneo yanayoweza kuingiza vipato ambapo wafanyabiashara wa India watashirikiana na kufanya kazi pamoja na wenzao wa Zanzibar ili kuendeleza sekta hiyo na kuleta maslahi kwa wananchi wa nchi zote mbili.

Dk. Mwinyi alisema serikali inafanya kila juhudi kutekeleza dhana ya Uchumi wa Buluu, hivyo akaiomba nchi hiyo kuanzisha kituo cha teknolojia ya mawasiliano kwa kuzingatia kuwapo soko kubwa nchini kwa vile Zanzibar ni nchi ya kutoa huduma, hatua aliyosema itazalisha ajira.

Alisema kuna umuhimu wa kufungua hospitali maalum visiwani hapo kwa ajili ya watalii ambao wanafika kila mwaka kwa idadi kubwa. Alipongeza azma ya India ya kufungua tawi la Hospitali ya Apollo katika eneo la Masaki jijini Dar es Salaam, hatua itakayosaidia kupanua wigo wa upatikanaji wa huduma bora za matibabu.


Dk. Mwinyi pia alitumia fursa hiyo kupongeza uhusiano na ushirikiano wa muda mrefu uliokuwa kati ya India na Zanzibar na Tanzania kwa ujumla pamoja na misaada mbalimbali ya kiuchumi na kijamii ambayo nchi hiyo imekuwa ikiisaidia Zanzibar.

Alisema misaada hiyo inajumuisha miradi ya huduma za majisafi na salama ambayo alikiri kwa kiasi kikubwa itapunguza shida ya upatikanaji wa huduma hiyo.

Katibu Mkuu wa Idara ya Ushirikiano kati ya India na Bara la Afrika, Ravi, alisema Serikali ya India inalenga kuimarisha ushirikiano ulioko kati yake na Zanzibar na Tanzania kwa ujumla kupitia nyanja mbalimbali, ikiwamo biashara.

Alisema India ina wataalamu wa kutosha katika sekta ya Uchumi wa Buluu, hivyo akaiomba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kubainisha maeneo ambayo taifa hilo litaisaidia, akidokeza kuwa nchi yao inalenga kupanua wigo wa ushirikiano kwa kuongeza fursa za masomo.

Alisema wakati akiwa nchini, alipata fursa ya kutembelea miradi mitatu ya maji inayoendelea kutekelezwa katika maeneo mbalimbali kupitia ufadhili wa nchi hiyo na hivyo atahimiza utekelezaji wake.





# NSSF yawafikisha mahakamani waajiri

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

MFUKO wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) wilayani Kahama mkoani Shinyanga umewafikisha mahakamani waajiri 52 kwa kutowasilisha michango ya wafanyakazi wao.

Vilevile, mfuko huo umepanga kuwafungulia mashtaka waajiri 40 kutoka taasisi binafsi ili kuhakikisha michango ya wanachama wao inalipwa kwa kuwa inapochelewa, inasababisha wastaafu kutopata mafao yao mapema. Meneja wa NSSF Halmashauri ya Kahama, Aisha Nyemba alibainisha wakati wa kilele cha Wiki ya Huduma kwa Wateja na kusema kuwa kila mwajiriwa anatakiwa kuwasilisha michango ya watumishi wake kwa wakati.

Alisema kuwa katika kipindi cha miezi sita iliyopita, NSSF imelazimika kuwafungulia kesi za jinai na kuwafikisha mahakamani waajiri 52 kutoka taasisi mbalimbali zilizoko wilayani hapo. Kati yake, kesi 29 zimeamuliwa na michango kutolewa na 23 zinaendelea mahakamani ili kuhakikisha haki inatendeka.

Nyemba alisema waajiri wengi wamekuwa hawawakilishi michango ya wafanyakazi wao kwa wakati licha ya kuwakata fedha kila mwezi, hali ambayo inasababisha malalamiko kuwa mengi kwa watumishi pindi wanapoamua kuacha kazi na ndiyo sababu NSSF inachukua hatua za kisheria.

"Niwaombe waajiri kuacha tabia ya kuchukua fedha za waajiriwa wenu na kuzipangia matumizi mengine kwani kwa kufanya hivyo ni kwenda kinyume cha sheria na unaweza kuchukuliwa hatua kali za kisheria na serikali ikiwamo kufungwa jela," alionya.

Alisema katika kuhakikisha waajiri wanawakilisha michango ya watumishi wao katika mfuko, wameamua kuchukua hatua ya kuwafikisha mahakamani ili watoa fedha hizo na hawataacha kuendelea kuchukua hatua mpaka pale tabia hiyo itakapokoma.

Katika hatua nyingine, Nyemba aliwataka wanachama wa mfuko huo pamoja na waajiri kutumia mifumo ya kielektroniki kuangalia salio la michango yao inayokatwa na kuwasilishwa bila kufika katika ofisi na kuwasihi pale wanapoona michango haiwasilishwi, wafike ofisini kwa hatua zaidi.

Alisema mfumo huo wa kielektroniki ni msaada mkubwa kwa waajiri kwa kuwa watakuwa na uwezo wa kufanya kazi zao hata wakiwa majumbani huku wanachama nao wakifaidika kwa kuangalia salio.



Waziri wa Viwanda na Uwekezaji, Ashatu Kijaji, akimkabidhi mashine ya kuchimbia migodini (Excavator) Mkurugenzi wa Kampuni ya G Unity Square Ltd, Ezekiel Rembo (kushoto), baada ya kuinunua kwa bei ya punguzo wakati wa maonyesho ya madini mkoani Geita. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# TANESCO yaendesha msako wanaoihujumu

**Na Lilian Lugakingira**
BUKOBA

SHIRIKA la Umeme (TANESCO) mkoani Kagera limeanzisha kampeni maalum inayoshirikisha vyombo vya dola na taasisi nyingine za kisheria kuwasaka watu wote wanaohusika na vitendo vya wizi wa nyaya za umeme kwenye transfoma na wanaochoma moto mashamba na misitu na kusababisha nguzo kuungua.

Akizungumza wakati wa kuhitimisha Wiki ya Huduma kwa Wateja, Ofisa Uhusiano wa TANESCO mkoani Kagera, Samwel Mandari alisema tatizo hilo la kuhujumu miundombinu ya shirika hilo ni kikwazo katika kutoa huduma kwa wananchi kwa ufanisi, pia linasababishia hasara shirika hilo.

"Katika kampeni hii italishirikisha Jeshi la Polisi na vyombo vingine vya kisheria na watakaobainika watachukuliwa hatua za kisheria ili kukomesha hujuma hizi kwa shirika na wateja wetu, niwaombe wananchi tutoe ushirikiano kwa hili," alisema Mandari.

Akizungumza na Nipashe kuhusu huduma ya umeme, mkazi wa Manispaa ya Bukoba, George Sebastian aliomba TANESCO kuwapatia umeme wa uhakika kwa siku nzima.

"Umeme usiwe unakatika mara kwa mara, maana wakati mwingine inatokea muda huo una shughuli nyingi zinazohitaji umeme lakini unakatwa. Hili ni tatizo kubwa kwetu maana linatusababishia hasara," alilalamika Sebastian.

Kwa mujibu wa sheria za Tanzania, mtu anayeharibu miundombinu ya TANESCO au kuiba vifaa vya shirika hilo, anatenda kosa linaloangukia kwenye jinai ya uhujumu uchumi.

## RC aonya wafanyabiashara kujipendekeza kwa viongozi

**Alphonce Kabilindo,** GEITA

MKUU wa Mkoa wa Geita, Martine Shigela ameonya wafanyabiashara kujipendekeza kwa viongozi wa serikali ili kupata kinga ya kutolipa kodi ya serikali, huku akiwataka maofisa wa Mamlaka ya Mapato (TRA) kuacha kusumbua wawekezaji.

Shigela alitoa angalizo hilo mwishoni mwa wiki kufuatia kuwapo taarifa za baadhi ya wafanyabiashara kuwa na tabia ya kujipendekeza kwa viongozi wa serikali ili kupata mwanya wa kufanya biashara zao pasi na kulipa kodi.

"Mimi siyo mtu wa hivyo, wewe kama ni mfanyabiashara wa madini, kafanye biashara ya madini kwa kulipa kodi. Nimepata tetesi kuna baadhi ya viongozi wa serikali wanapokuja huwa wanaomba orodha ya wafanyabiashara, nao hujipendekeza. Mimi siyo wa hivyo, twendeni tukafanye kazi," alionya.

Alitoa kauli hiyo wakati akifungua mkutano maalum wa kujadili fursa zinazopatikana katika mkoa wake, zikiwamo za kilimo, ufugaji, uchimbaji madini na utalii.

Alibainisha kuwa tabia hiyo haina manufaa kwa uchumi wa Mkoa wa Geita na kinachotakiwa ni kila kiongozi kuwajibika kwa nafasi yake ili kufanikisha lengo lililokusudiwa la kuinua uchumi wa wananchi na mkoa wake.

Aliwaonya watumishi wa TRA mkoani hapo dhidi ya usumbufu kwa wafanyabiashara wanaojitokeza kuwekeza katika majengo ya biashara, zikiwamo hoteli na majengo ya kisasa kwa ajili ya biashara.

"Nimeambia ipo tabia ya maofisa wa TRA wanawasumbua wawekezaji wanapojitokeza kuanza kujenga au kufanya biashara, huwafuata kuanza kuwachunguza kuhusu walikopata fedha hizo," Shigela alisema.

Alifafanua kuwa baadhi ya wafanyabiashara wakubwa wamekuwa wakivuna fedha nyingi katika mkoa huo, lakini wakitaka kujenga wanakwenda maeneo mengine wakihofia wakijenga Geita wanaanza kufuatiliwa na maofisa wa TRA. "Mfano kuna mtu anaitwa... (alitaja jina la mfanyabiashara) kuna watu waliniambia 'huyu kaamua kujitungua'... sasa hapa kuna shida nyie TRA mnatakiwa mtende haki, mtakimbiza wawekezaji," alisema Shigela.

Katibu Tawala mkoani Geita, Profesa Godius Kahyarara, aliwataka wawekezaji kujitokeza kuwekeza katika sekta mbalimbali zikiwamo za uchimbaji madini, kilimo cha umwagiliaji katika mradi wa Bonde la Ibada na unenepeshaji wa mifugo.

Alisema Mkoa wa Geita ni kinara wa uzalishaji madini, licha ya kutumia zana duni, wakizalisha wastani wa tani 15 kwa mwaka, hivyo wana kazi ya kusaidia kuondokana na matumizi ya zana duni kwenda katika matumizi ya teknolojia ya kisasa.

HABARI KIMATAIFA

# WHO yaitaka Afrika kudhibiti wanaojiua

**WHO,** Afrika

SHIRIKA la Afya Duniani (WHO) limetoa wito kwa nchi za Afrika kuchukua hatua kudhibiti ongezeko kubwa la watu wanaojiua, huku likibainisha kuwa bara hilo linaongoza kwa matukio hayo duniani.

Kwa mujibu wa ripoti iliyotolewa na Mkurugenzi wa WHO Afrika, Matshidisco Moeti (pichani chini), mwishoni mwa wiki iliyopita, nchi sita kati ya 10 zenye idadi kubwa ya watu kujiua duniani ziko Afrika, na kiwango cha kujiua katika bara hilo ni zaidi ya moja ya tano ikilinganishwa na maeneo mengine.

"Takriban watu 11 kati ya 100,000 kila mwaka wanafariki kwa kujiua katika eneo la Afrika, ikiwa kiwango cha juu kuliko wastani wa kimataifa wa tisa kwa kila watu 100,000, vifo vya kujinyonga au kunywa sumu za dawa za kuua wadudu ni vitendo ambavyo vinaongoza katika orodha," alisema Moeti.

Pia inaelezwa kuwa shirika hilo limeanzisha uhamasishaji kwa lengo la kuongeza uwelewa wa tatizo hilo itakayoenda sambamba na Siku ya Kimataifa ya Afya ya Akili inayoadhimishwa kila mwaka Oktoba 10.

"Kujiua ni moja ya tatizo kuu la afya ya umma na kila kifo kutokana na kujiua ni janga. Bahati mbaya njia za kuzuia kujiua ni nadra kupewa kipaumbele katika programu za kitaifa za afya," alisema Moeti.

Aliongeza kuwa unyanyapaa ni tatizo kuu, kama ilivyo ukosefu wa ufadhili.

Pia inaelezwa kuwa Afrika ina wastani wa mtaalamu mmoja wa magonjwa ya akili kwa kila watu 500,000 kiwango ambacho kwa asilimia 100 kiko chini na mapendekezo ya WHO, na kwamba ukosefu wa matabibu ni kitu kinachotisha katika nchi ambazo zimepitia mizozo.

Moeti alibainisha kuwa matumizi katika afya ya akili barani Afrika yako chini ya senti 50 kwa mtu, ikiwa ni chini ya robo ya pendekezo ya UN la robo tatu.



# Maandamano yaendelea Iran kupinga uongozi

**TEHRAN,** Iran

KIKUNDI cha Haki za Binadamu nchini Iran kimesema Wairan wameendelea na maandamano nchini humo kupinga uongozi wa kidini, baada ya kifo cha msichana aliyekuwa chini ya ulinzi wa polisi, ambacho kiliibua hasira kwa wananchi na kusababisha machafuko hayo.

Kwa mujibu wa taarifa ya kikundi hicho iliyotolewa jana, wananchi wameendeleza maandamano dhidi ya watawala wa kidini ambao wanakabiliwa na upinzani mkubwa wa umma.

Vyombo vya habari vya serikali ya Iran mwishoni mwa wiki iliyopita vilisema ripoti ya uchunguzi wa maiti ilikanusha kwamba msichana huyo Mahsa Amini alifariki kutokana na kipigo kichwani na katika viungo vya mwili wakati akiwa anashikiliwa polisi na kukihusisha kifo chake na matatizo ya kiafya aliyokuwa nao.

Ilielezwa kuwa kifo cha Amini (22), ambaye ni Muiran Mkurdi, kilichochea maandamano katika nchi nzima, ikiwa changamoto kubwa sana kwa viongozi wa kidini wa Iran ambao wamekuwapo madarakani kwa miaka kadhaa.

**Akaunti ya Twitter ya Tavsir1500 ambayo inafuatiliwa sana imeripoti ufyatuaji wa risasi kwa waandamanaji katika miji miwili ya Kikurdi ya kaskazini magharibi.**

Kwa mujibu wa VOA, wanawake nchini humo walivua mitandio yao wakikaidi amri ya utawala wa kidini, huku umati wenye hasira ukipaza sauti wakiutaka utawala wa Kiongozi Mkuu Ayatollah Ali Khamenei uangushwe.

Kundi hilo la haki za binadamu la Iran lilieleza kuwa baada ya wito wa maandamano makubwa ya umma, majeshi ya usalama yaliwafyatulia risasi waandamanaji na kutumia gesi ya kutoa machozi katika miji ya Kikurdi ya Sanandaj na Saqqez.

"Migomo imesambaa kote katika miji ya Saqqez, Diwandareh, Mahabad na Sanandaj," lilisema.

Kikundi hicho kiliongeza kuwa, moja ya shule zilizoko katika uwanja wa jiji la Saqqez ulikuwa umejaa wasichana wa shule waliokuwa wakipiga kelele zilizosikika zikisema mwanamke, uhai, na uhuru, huku likieleza kwamba majeshi ya usalama ya Iran yalikuwa yameanzisha msako katika miji miwili ya kikurdi.

Kilisema majeshi ya usalama yanafyatua risasi kwa waandamanaji katika miji ya Sanandaj na Saqqez, na kwamba askari wa kutuliza ghasia walikuwa wanatumia mabomu ya kutoa machozi.

Akaunti ya Twitter ya Tavsir1500 ambayo inafuatiliwa sana imeripoti ufyatuaji wa risasi kwa waandamanaji katika miji miwili ya Kikurdi ya kaskazini magharibi.

Makundi ya haki za binadamu yanasema zaidi ya watu 150 wameuawa, mamia wamejeruhiwa na maelfu wamekamatwa na majeshi ya usalama yanayokabiliana na waandamanaji.

Ilielezwa kuwa Amini alikamatwa mjini Tehran Septemba 13 kwa kuvaa vazi lisilokubalika na alifariki siku tatu baadaye.

Serikali nchini humo ilieleza kuwa maandamano hayo ni njama ya maadui wa Iran ikiwamo Marekani, ikiwashutumu waasi wenye silaha kati ya wengine kusababisha uvunjifu wa amani ambapo takriban wanajeshi 20 wa vikosi vya usalama wameripotiwa kuuawa. **VOA**



Askari wa Kikosi cha Zimamoto wakizima moto katika moja ya majengo yaliyoharibiwa baada ya shambulio la bomu la Russia katika mji wa Zaporizhia Ukraine. **PICHA AFP**

# 17 wauawa shambulio la makombora Ukraine

**ZAPORIZHIA,** UKRAINE

WATU 17 wametajwa kuuawa na wengine kujeruhiwa baada ya vikosi vya Jeshi la Russia kufanya shambulizi la mabomu katika mji wa Zaporizhia Ukraine jambo lililosababisha pia uharibifu mkubwa wa makazi ya watu.

Kwa mujibu wa RFI, vikosi vya Russia vilitekeleza shambulio hilo usiku wa kuamkia jana, na kwamba jana saa mbili asubuhi, makombora kumi ya Russia yaliangukia mji wa Zaporijja, na kusababisha uharibifu mkubwa katikati ya eneo la makazi.

Taarifa ilieleza kuwa majengo matano yaliharibiwa kabisa na mengine takriban 40 kuathiriwa vibaya, huku waokoaji wakiwa bado wanatafuta waathiriwa chini ya vifusi.

Aidha, inaelezwa kuwa mamia ya wakazi wa mji wa Zaporizhia wanajaribu kuondoka katika jiji hilo, ambalo sasa linakumbwa na mashambulizi ya mabomu mara kwa mara.

Septemba 30, vikosi vya Russia vilifyatua kombora dhidi ya msafara wa magari, na kuua raia 30, wakati Alhamisi kombora lilianguka katika barabara kuu ya jiji hilo, na kuua jumla ya watu 17.

Wakati Moscow haidhibiti mji mkuu huu wa eneo ambalo imeamua kuunganisha, inaonekana kwamba jeshi la Urusi limeamua kuweka serikali ya ugaidi katika mji wa Zaporizhia. **RFI**

# Shekhe Mkuu ataka wanafunzi wafundishwe dini na ibada

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

SHEKHE Mkuu wa Mkoa wa Pwani, Hamis Mtupa, ameshauri uongozi wa shule za bweni kutoa muda kwa wanafunzi kufanya ibada ili kujifunza mambo ya kiimani.

Mtupa alitoa rai hiyo mwishoni mwa wiki aliposhiriki katika mahafali ya darasa la saba katika Shule ya Msingi Kibaha Independent (KIPS).

Alisema utaratibu huo ukianzia chini unawaandaa vijana kuishi kwenye maadili mazuri.

Kwa mujibu wa kiongozi huyo, watoto walioko katika shule za bweni, muda mwingi wanakuwa shuleni, hivyo utaratibu huo ukiwapo utawasaidia kuwalea na kusimama kwenye imani zao.

Aliwakumbusha wazazi kuthamini elimu kwa kuwekeza fedha zao kuwasomesha, ili baadaye wakidhi vigezo vya kuajiriwa na kujiajiri.

Shekhe Mtupa aliwakumbusha wahitimu kuzingatia maadili ya kidini ambayo yatawaongoza kushikamana na ibada kuwaongezea kupenda kumcha Mungu na kuepuka kujiingiza kwenye makundi ya uhalifu.

Mkurugenzi wa KIPS na KPS, Annex Yusuph Mfinanga aliwataka wazazi kuendelea kuthamini elimu kwa kuwapeleka watoto shuleni.

Alisema wazazi wanatakiwa kuzingatia muda wa kulipa ada kwa shule binafsi na wale ambao hawamudu wawapeleke kwenye shule za serikali, ili nao wapate elimu.

Meneja wa shule hiyo, Nuru Mfinanga aliwashauri wazazi kutowaingiza watoto kwenye migogoro inayochangia kuwarudisha nyuma kitaaluma.




Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya Maendeleo TIB, Lilian Mbassy (katikati), akizungumza wakati wa kukata keki kuadhimisha kilele cha Maadhimisho ya Wiki ya Huduma kwa Wateja kwa mwaka 2022. Wengine ni baadhi ya wawakilishi wa wateja wa benki hiyo, kushoto ni Yvone Mbando (kutoka TUDARCO) na Philemon Msegu ambaye ni Mkurugenzi Mtendaji wa Exomark Investment Limited. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wabuni mfumo wa kuzalisha mboga kwenye eneo dogo

**Na Elizabeth Zaya**

WANAFUNZI wa Shule ya Sekondari Mzimuni iliyoko Magomeni Dar es Salaam, wamebuni mfumo maalum wa kuzalisha mboga za majani unaotumia eneo dogo kwenye nyumba ya kuishi.

Wakizungumza na Nipashe shuleni hapo mwishoni mwa wiki, wanafunzi hao walisema kubuni mfumo huo ni miongoni mwa matokeo ya sayansi wanayoisoma darasani ya kutatua shida kwenye jamii.

"Tumeamua kubuni mfumo huu kwa kuiweka sayansi ya darasani kuwa kwenye vitendo hususani kwa kutatua changamoto zilizoko kwenye jamii, huu ni mfumo ambao kila mtu anaweza kuutumia nyumbani kwake na akapata mboga ya kula na ya kuuza na hauna gharama hata kama una eneo dogo unapoishi," alisema mmoja wa wanafunzi waliobuni mfumo huo, Rahimu Saidi.

Aliongeza: "Tunataka tuitumie sayansi tunayoisoma darasani kwa vitendo katika jamii tunayoishi na kuisaidia taifa kwa ujumla, na itusaidie na sisi kwenye eneo la ajira badala ya kutegemea kuajiriwa tu."

Rahimu alisema miongoni mwa waliochangia wao kuwa wabunifu wa mawazo mbalimbali ya kutatua kero kwenye jamii ni Rotary Club kupitia mradi wao wa Inspire.

"Sisi tumekuwa tukisoma masomo ya sayansi kwa ajili ya kujibia mtihani, lakini hatukujua kwamba yanaweza kutusaidia kwenye maisha yetu wenyewe tukiwa shuleni na baadaye, lakini Rotary Club walikuja shuleni kwetu wakatufundisha namna ya kutumia haya tunayosoma katika fursa zinazotokana na changamoto za kwenye jamii.

"Kwa hiyo wao walikaa na sisi na kutufundisha mbinu mbalimbali, na hivi sasa tuna uwezo wa kubuni vitu mbalimbali na vya kifursa na tukajipatia kipato au tukasaidia jamii zetu," alisema Rahimu.

Rais mstaafu wa Rotary Club, Fredy Laiser alisema walianzisha programu ya kuwawezesha wanafunzi kuitumia elimu wanaoipata shuleni katika fursa mbalimbali za kuwasaidia kimaisha wao na jamii.

"Maana ya programu hii ni kuwasaidia wanafunzi wasiishie tu kusoma kwenye vitabu, bali waichukue taaluma hiyo na kuiweka kwenye matumizi kwenye maisha ya kawaida, iwe ni kwenye familia zao, kuendesha maisha yao wenyewe lakini hata kwenye kusaidia taifa kwenye changamoto mbalimbali.

"Kama Rotary Club, tunaamini kwamba tukiendelea kufanya hivi kwa wanafunzi kutoka kwenye shule mbalimbali, tutalisaidia taifa kuzalisha wataalamu na wabunifu wazuri wa kutambua na kuzitumia fursa, lakini tutapunguza vijana wengi wanaokuwa wategemezi wa kuajiriwa pekee," alisema.

Aliongeza kuwa ni vyema wanafunzi wakapewa elimu ambayo haitaishia kujibu mitihani pekee, bali iwe yenye faida zaidi kwao na kwa taifa lao siku zote kwa kufanya vitu kwa vitendo.

## 'Halmashauri zitunge sheria kupinga ukatili'

**Na Mwandishi Wetu,** SAME

SERIKALI imezitaka mamlaka zote za serikali za mitaa nchini kuandaa sheria ndogo zitakazosimamia kupinga ukatili wowote kwenye maeneo mbalimbali hasa wakati huu wenye ongezeko la matukio hayo.

Pia imeagiza katika kila kikao kuanzia ngazi ya mtaa hadi taifa kuwa na ajenda ya ukatili wa kijinsia na inapotokea haipo waseme ili kuwekewa mikakati katika eneo husika.

Mratibu wa Mpango Kazi wa Kitaifa wa Kutokomeza Ukatili wa Kijinsia, Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Linus Kahendaguza, aliagiza hayo mwishoni mwa wiki wakati wa kufunga Tamasha la Jinsia Kanda ya Kaskazini.

Tamashaka hilo liliandaliwa na Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP) na kuwaleta pamoja wanaharakati zaidi ya 600 kutoka maeneo mbalimbali nchini.

Alisema wizara ilifanya kikao kilichojadili ukatili ulioko nchini na kuazimia kila mamlaka ya serikali za mitaa kuwa na sheria ndogo za kupinga ukatili kwenye maeneo yao.

"Imeelekezwa kwa sasa kila kikao kinachofanyika lazima kigusie masuala ya ukatili kwenye maeneo yao, wananchi mkiona kikao hakijazungumzia lolote kuhusu ukatili lazima waseme, ili iwe ni utaratibu wa lazima kwenye kila kikao," alisema.

Aliongeza kuwa wanaharakati na wananchi wanatakiwa kutambua serikali inaunga mkono kwa kila namna mchakato wa usawa kwa wanaume na wanawake, ndiyo maana Rais Samia Suluhu Hassan amekuwa kinara wa masuala ya jinsia ndani na nje ya nchi.

Kandaguza alisema mikopo ya asilimia nne kwa wanawake, nne vijana na mbili wenye ulemavu inatolewa kwa mfumo wa kidigitali unaowezesha uchakataji kwa haraka.

Mwenyekiti wa Bodi ya TGNP, Gema Akilimali, alisema jitihada za serikali zinatia moyo kwa kuwa zinaunga mkono kazi kubwa inayofanywa na wanaharakati wanaotaka kuleta mabadiliko katika jamii yenye usawa.

"Kilichokuwa kinatukwamisha ni kuwa na viongozi ambao hawatuelewi tunachopigania ila uongozi wa sasa unakwenda bega kwa bega na sisi ndio maana kazi yetu inakuwa rahisi, tunaamini nanyi kazi yenu ni rahisi sana," alisema.

Akifunga tamasha hilo, Mkuu wa Wilaya ya Same, Edward Mpogolo, alisema mila zinatumika kama mwamvuli wa kuendeleza ukatili na watatunga sheria ndogo za kupinga ukatili na kuwataka wananchi kusimamia maazimio ya tamasha hilo.

# Godliver ajivunia tuzo

Na Mwandishi Wetu

MSANII wa kike wa Bongo Muvi, Godliver Gordian, amesema anajivunia kushinda tuzo ya msanii bora wa kike kwa mwaka 2021.

Akizungumza jijini Dar es Salaam, Godliver alisema tuzo hizo za Filamu Tanzania zilizoandaliwa na serikali zilikuwa ni za kwanza, hivyo zimetoa chachu kubwa kwa wasanii.

"Sasa hivi si tu kwamba natambulika kama msanii bali natambulika kama msanii niliyeshinda tuzo," alisema.

"Imeongeza kitu kwenye kazi yangu, watu pia wanapenda kufanya kazi na mtu mwenye 'taito'."

Alipoulizwa kuhusu changamoto za tuzo hizo na nini anashauri kwa waandaaji, Godliver alisema anaamini waandaaji wanafahamu wapi kulikuwa na changamoto na wataboresha kwa mwaka huu.

"Tunajua kwamba kwa kuwa ilikuwa ni mara ya kwanza, waandaaji watakuwa wamejua nini cha kuongeza na changamoto zake na naamini watazifanyia kazi kwa mwaka huu," alisema Godliver.





# DAVIDO KUFUNGA NDOA 2023

**LAGOS,** Nigeria

NYOTA wa muziki wa Nigeria, Davido yupo mbioni kuaga kambi ya ukapera baada ya kuthibitisha rasmi kuwa atafunga ndoa na mpenzi wake, Chioma maarufu kama Chef Chi.

Mpenzi wake huyo wa muda mrefu kwa sasa ameripotiwa kuwa ni mjamzito na Davido anataka kumzawadia ndoa.

Davido amebainisha hayo akiwa na mpenzi wake huyo pamoja na mchungaji wake, Tobi Adegboyega nchini Uingereza, alipoenda kumtambulisha Chioma kwa mchungaji huyo.

"Huyu ni mke wangu na sasa nataka kuhalalisha rasmi," alisema Davido wakati akimtambulisha kwa mchungaji huyo.

"Kwa asilimia mia moja, nakwenda kumuoa na kufunga nae ndoa mwakani 2023."

Ikumbukwe, Davido na Chioma walianza mahusiano yao tangu mwaka 2017, na 2019 Davido alimvisha pete ya uchumba, huku wakiwa wamebahatika kupata mtoto mmoja.

Hata hivyo, wakaja kuachana mwaka 2020, wakabaki kuwa walezi wa mtoto wao tu.

Julai mwaka huu wakawa wanahusishwa kurudiana, kisha baadaye wakathibitisha na sasa wamepanga kufunga pingu za maisha ifikapo mwakani.

# Mke amtaka Roma Mkatoliki arudi Bongo

Na Mwandishi Wetu

MKE wa rapa Roma Mkatoliki, Nancy Mshana, kupitia ukurasa wake wa Instagram amemtaka rapa huyo ambaye yupo nchini Marekani kurudi Tanzania kwani mashabiki wake 'wamemmisi'.

Nancy aliandika hayo wakati akisherehekea kumbumbuku ya miaka yao saba ya ndoa na Roma mwishoni mwa wiki.

"Miaka 13 iliyopita nilikutana na huyu mwamba hapa akawa rafiki yangu sana. Miaka saba iliyopita tukaenda mbele ya kanisa na mbele ya mashahidi kuweka ahadi ya kupendana hadi milele, aanze yeye au nianze mie hatutoachana.

"Natamani ningekuwa mzuri wa kuandika siku moja ningewaelezea historia yetu kidogo, naamini kuna ambayo watu wangejifunza kitu kupitia sisi.

"Miaka saba si mchezo, umejitahidi sana hongera ila sasa imetosha naambiwa nikuambie urudi nyumbani mashabiki wamekumiss."



HABARI MICHEZO

# AZAM YAANIKA SABABU KICHAPO LIBYA, YAPANIA KUPINDUA MEZA

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA Mkuu wa Azam FC, Denis Lavagne na mwenzake wa safu ya ushambuliaji, Kalimangonga Ongalla, wamekiri timu kucheza chini ya kiwango, lakini wamesema watapambana hadi mwisho kwenye mechi ya marudiano ili kuhakikisha wanapata ushindi na kusonga mbele.

**Wakizungumza kutoka nchini Libya timu yao juzi ikichezea kichapo cha mabao 3-0 dhidi ya Al Akhdar ya nchini humo kwenye mechi ya raundi ya Kwanza ya Kombe la Shirikisho Afrika iliyopigwa kwenye Uwanja wa Martyrs of February uliopo Benina, kilometa 19 Mashariki mwa jiji la Benghazi, makocha hao wote wakihojiwa kwa nyakati tofauti walikiri kuwa timu yao haikucheza soka ambalo walitarajia au wanalolifahamu kutoka kwa wachezaji wao.**

"Hatukucheza vizuri sana wala vibaya sana, tulifanya makosa yaliyowawezesha wapinzani kufunga mabao, tukiwa na mpira tulikuwa tunacheza vizuri, lakini tunapokuwa hatuna ndipo udhaifu wetu ulipokuwa, tulikosa nguvu na kujiamini," alisema Kocha Mkuu wa timu hiyo, Lavagne raia wa Ufaransa.

Hata hivyo, alisema bado wana mechi nyingine ya nyumbani na hawajakata tamaa kwa sababu kwenye soka lolote linaweza kutokea.

Kwa upande wa Ongalla, alisema walianza vema kwenye mechi hiyo na kupata nafasi, lakini hawakuzitumia na kadri muda ulivyozidi kusonga mbele walikuwa wakicheza tofauti na matarajio.

"Tulianza vizuri, lakini hatukutumia makosa yao, baadaye timu ikawa iko chini, tukacheza chini ya kiwango sana, imetuumiza sana, sina la kusema tujipange tuangalia mechi ijayo," alisema Ongalla.

Alisema kwenye mechi ya marudiano kinachotakuwa ni kupambana tu na ndiyo njia pekee ambayo inaweza kuwasaidia kuweza kuvuka na si vinginevyo.

"Kwenye mechi ya marudiano kinachotakiwa ni kupambana tu, si kama haiwezekani, inawezekana kuvuka, lakini ni lazima tujitolee zaidi siyo kama tulivyocheza mechi hii," alisema.

Azam ambayo haikucheza mechi ya awali, badala yake ikatinga moja kwa moja raundi ya kwanza, italazimika kushinda mabao 4-0 kwenye mechi ya marudiano ili kuweza kusonga mbele vinginevyo itaaga rasmi michuano ya kimataifa na kusubiri msimu ujao.

Endapo Azam FC itafuzu itasubiri kupangiwa timu moja kutoka zitakazotolewa kwenye raundi ya Kwanza ya Ligi ya Mabingwa Afrika ili kucheza mechi ya mtoano kuwania kufuzu hatua ya makundi ya Kombe la Shirikisho.



Kiungo wa Azam FC, Isah Ndala (kulia), akimtoka mchezaji wa Al Akhdar kwenye mechi ya Kombe la Shirikisho Afrika iliyopigwa Uwanja wa February jijini Benghazi nchini Libya juzi na Azam kuchapwa mabao 3-0. **PICHA: AZAM**

# *Kipanga yaapa kufanya kweli Tunisia*

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

TIMU ya Kipanga imesema licha ya kutoka sare katika mchezo wao wa nyumbani wa Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya Club Africain ya Tunisia, bado inamatumaini ya kusonga mbele katika michuano hiyo.

Kipanga FC juzi, Jumamosi walishindwa kutamba katika dimba la nyumbani baada ya kulazimishwa sare tasa katika mchezo wa kwanza uliopigwa Uwanja wa Amaan.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Msaidizi wa timu hiyo, Khamis Hassan, alisema bado wanamatumaini makubwa kuhakikisha wanasonga mbele kwa kutinga hatua ya katika michuano hiyo.

Alisema anajua utakuwa mchezo mgumu ugenini, lakini wanajipanga kwenda kufanya mapinduzi katika uwanja wa ugenini huko Tunisia.

Hassan alisema anajua mbinu zitakazotumiwa na wapinzani wao mojawapo ni kupata hamasa kuwa ya mashabiki uwanjani kama walivyofanya wao Dimba la Amaan, lakini na wao wanajiandaa kisaikolojia wachezaji wao kukabiliana na mbinu hizo.

"Tunaenda kupambana huko Tunisia ili kuhakikisha malengo yetu ya kusonga mbele yanatimia, uwezo huo tunao japo tunatambua mchezo hautakuwa rahisi, lakini wachezaji wetu na sisi tunawaandaa kimwili na kiakili kukabiliana na vita ya ugenini," alisema.

Aidha, aliwataka mashabiki wa timu hiyo kuendelea kuwapa moyo wachezaji wa timu yao ili kuhakikisha wanaendelea kuwa na hamasa katika mchezo huo wa marudiano.

Kipanga itashuka uwanjani ugenini, Tunisia Jumapili wiki hii katika mchezo huo wa marudiano na kama ikishinda itasubiri kupangiwa timu moja kutoka zitakazotolewa kwenye raundi ya Kwanza ya Ligi ya Mabingwa Afrika ili kucheza mechi ya mtoano kuwania kufuzu hatua ya makundi ya Kombe la Shirikisho.

# Manula, Nahimana vinara 'clean sheets'

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI Ligi Kuu Tanzania Bara ikiwa kwenye raundi ya sita, kipa wa Simba, Aishi Manula na Jonathan Mahimana wa Namungo FC, wanaongoza kwa kukaa golini mechi nyingi bila kuruhusu wavu wao kuguswa.

Manula ambaye ndiye kipa namba moja wa timu ya Taifa, Taifa Stars na Nahimana, kipa wa timu ya Taifa ya Burundi, wamekaa golini mechi nne kila mmoja bila kuruhusu bao na kuongoza kwa 'clean sheets' kwa makipa wote wa Ligi Kuu mpaka sasa.

Kwa mujibu wa takwimu za Ligi Kuu, Manula amesimama kwenye milingoti mitatu katika mechi nne bila kuruhusu bao kwenye mechi ambayo Simba ilicheza dhidi ya Geita Gold ikishinda mabao 3-0, dhidi ya Kagera Sugar ikishinda mabao 2-0, dhidi ya Prisons ikishinda bao 1-0 pia dhidi ya Dodoma Jiji ikishinda 3-0.

Ni mechi moja pekee ambayo aliruhusu wavu wake kugushwa dhidi ya KMC, ambapo Simba ilitoka sare ya mabao 2-2.

Kwa upande wa Nahimana, yeye alikaa langoni kwenye mechi dhidi ya Ihefu FC, Namungo ikishinda bao 1-0, ikaichapa Ruvu Shooting 1-0 na kisha kupata ushindi kama huo dhidi ya Coastal Union kabla ya kutoka suluhu na KMC FC.

Nayo ni mechi moja ambayo aliruhusu mabao mawili kwenye nyavu zake kama Manula, Namungo ilipotoka sare ya 2-2 dhidi ya Mtibwa Sugar.

Mbali na makipa hao, kipa mzawa wa Dodoma Jiji, Aron Kalambo na Mahamoud Mroivili raia wa Comoro anayeidakia Coastal Union wanashika nafasi ya pili kwa 'clean sheets' wakiwa wamekaa langoni mara tatu kila mmoja bila kuruhusu bao.

Makipa wenye 'clean sheets' mbili kila mmoja na ambao wanakamata nafasi ya tatu ni Ali Ahmada, Mcomoro anayeidakia Azam FC, Metacha Mnata wa Singida Big Stars pamoja na Hussein Masalanga wa Ruvu Shooting.



# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### ATAKIWA MAREKANI

KIUNGO wa Ureno, Cristiano Ronaldo mwenye umri wa miaka 37, amepewa ofa ya kuondoka Manchester United na kujiunga na Inter Miami, na mmiliki wa klabu hiyo, David Beckham. ***(Star)***

### SCHMEICHEL KUONDOKA NICE

GOLIKIPA wa Nice, Kasper Schmeichel mwenye umri wa miaka 35, anaweza kuondoka Januari, ikiwa ni miezi sita tangu aondokea Leicester. ***(L'Equipe via Leicester Mercury)***

### BARCA YAMGEUKIA DALOT

BARCELONA inataka kumsajili beki wa kulia wa Manchester United, Diogo Dalot mwenye umri wa miaka 23 raia wa Ureno, ambaye mkataba wake pale Old Trafford unamalizika mwishoni mwa msimu huu. ***(Sport)***

### GAKPO ANUKIA LEEDS

KLABU ya Leeds United imefikia makubaliano binafsi na Cody Gakpo na sasa wanajadiliana kuhusu ada na PSV Eindhoven juu ya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23. ***(Mirror)***

### AWANIWA SOUTHAMPTON

KLABU ya Southampton inamtaka winga wa Celtic na Ureno, Filipe Jota mwenye umri wa miaka 23. ***(Football Insider)***

### BISSOUMA AWINDWA LIVER

LIVERPOOL walikuwa mbioni kumsajili kiungo wa Mali, Yves Bissouma mwenye umri wa miaka 26, katika kipindi cha majira ya joto kabla ya kuamua kujiunga na Tottenham Hotspur kutoka Brighton. ***(The Athletic)***

### RABIOT KURUDI PSG

KLABU ya Paris St-Germain wanaangalia uwezekano wa Adrien Rabiot, 27, kurudi klabuni hapo, huku kiungo huyo wa Ufaransa mkataba wake na Juventus ukitarajiwa kufikia tamati kipindi kijacho cha majira ya joto. ***(Fichajes)***

### LOCATELLI KUBAKI JUVE

ARSENAL wamepata pigo kwenye harakati zao za kutaka kumsajili kiungo wa Juventus, Manuel Locatelli mwenye umri wa miaka 24, baada ya Muitaliano huyo kuamua kubaki Turin. ***(Football London)***

### GARNACHO NA MAN UNITED

KLABU ya Manchester United inapanga kukutana na wakala wa Alejandro Garnacho mwenye umri wa miaka 18. ***(AS via Sport Witness)***

### ABRAHAM KURUDI CHELSEA

STRAIKA wa AS Roma, Tammy Abraham mwenye umri wa miaka 25, amekataa kuondoa uwezekano wa kurudi katika klabu yake ya utotoni ya Chelsea. ***(90 Min)***

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# POTTER ATOA SABABU YA KUBADILI KIKOSI CHELSEA

**LONDON,** England

●●● Ninajua kama tungepoteza watu wangeuliza kwa nini sikumchezesha Aubameyang...

KOCHA wa Chelsea, Graham Potter, amesema ni 'sifa kwa wachezaji' kwamba aliweza kufanya mabadiliko saba kwenye kikosi chake cha kwanza Jumamosi na kuweza kupata ushindi wa mabao 3-0 dhidi ya Wolves.

**Wachezaji Raheem Sterling, Pierre-Emerick Aubameyang, Reece James, Thiago Silva na Mateo Kovacic wote waliachwa kutoka kwenye kikosi kilichoifunga AC Milan katikati ya wiki, na kuwapa nafasi Christian Pulisic, Cesar Azpilicueta, Conor Gallagher, Trevoh Chalobah na wengineo.**

"Kuna kikundi kizuri hapa," alisema Potter akiwaambia waandishi wa habari baada ya mcheo huo.

"Sidhani kama tunaweza kufanikiwa tukiwa na wachezaji 11 pekee. Sidhani kama ni sawa kuendelea na 11 hadi waanguke na kuumia au chochote kisha tuwachezeshe wengine, kwani sidhani kama hiyo ni nzuri kwa nguvu ya kikundi."

Potter alikiri kwamba Chelsea ilistahili kushinda dhidi ya Wolves, pamoja na kufanya mabadiliko makubwa.

"Ninajua kwamba ikiwa tungepoteza mchezo wa leo (juzi) watu wangekuwa wakiniuliza kwa nini sikumchezesha Aubameyang," alisema.

"Ndivyo ilivyo. Lakini mradi tu sababu ipo, mradi ninaelewa kichwani mwangu kwa nini tumechukua uamuzi huo, lazima mtu achukue uamuzi huo."

Aidha, Potter alieleza kwamba ana mpango wa kuchukua kila mchezo kulingana na uteuzi wa timu, ikizingatiwa kwamba Chelsea inaendelea kucheza kila katikati ya wiki na kati ya wikendi.

"Lazima uchukue kila hali peke yake. Ikiwa unacheza mechi tatu kwa wiki katika Ligi Kuu, Ligi ya Mabingwa Ulaya na kisha Ligi Kuu tena, unapaswa kufanya uamuzi kuhusu wachezaji wapya, wachezaji ambao wamedhamiria na wanaotamani kucheza," alisema.

"Tuna kikosi kikubwa chenye ushindani mwingi na unahitaji ushindani, watu wanapigania kila mmoja, kusaidiana. Kutaka kucheza lakini tayari kusaidia na nadhani umeliona hilo."

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 367,
MECHI KALI
NOTTINGHAM
VERSUS
ASTON VILLA
1 | 3.27
X | 3.32
2 | 2.12
PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka
SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# ABRAHAM: NAWEZA KURUDI LONDON




**ROME,** Italia

MSHAMBULIAJI wa AS Roma, Tammy Abraham, amekataa kuondoa uwezekano kwamba anaweza kurejea katika klabu yake ya utotoni ya Chelsea.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25, aliondoka pale Stamford Bridge mwaka 2021 baada ya kupoteza nafasi yake chini ya kocha Thomas Tuchel na kufurahia msimu wake bora wa kwanza Roma, akifunga mabao 27 na kusaidia sita katika michezo 53 kwenye mashindano yote.

Chelsea inasemekana kuwa wamejadiliana kuhusu kipengele cha kumnunua ambacho ni takriban euro milioni 80.

Alipoulizwa kama angependa kurejea Chelsea iwapo watazingatia kipengele hicho, Abraham alisema: "Ninachozingatia ni kufanya kile nilichofanya mwaka jana hapa.

"Nina furaha hapa, timu ni nzuri, kocha mzuri pamoja na jiji na mashabiki ... nina furaha. Lakini huwezi kujua yajayo. Ni Mungu pekee anayejua siku zijazo."

Abraham hajawa na nafasi pale Roma msimu huu baada ya kocha Jose Mourinho kupanga upya safu yake ya ushambuliaji na sasa akimtumia zaidi Paulo Dybala.

Bado haijafahamika kama Chelsea watatumia kipengele chao cha kumnunua, lakini kilicho wazi ni hamu ya 'The Blues' hao ya kutaka kurekebisha safu yao ya ushambuliaji katika miezi ijayo.

## Ancelotti akacha kuizungumzia Clasico

**MADRID,** Hispania

CARLO Ancelotti hakutaka kuzungumzia mchezo wake wa wikendi ijayo dhidi ya Barcelona baada ya Real Madrid kuibuka na ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Getafe kwenye Ligi Kuu Hispania, LaLiga, Jumamosi.

'Los Blancos' hao hawakuwa na kiwango bora zaidi pale kwenye Uwanja wa Coliseum Alfonso Perez, lakini bao la kichwa la Eder Militao dakika ya tatu lilitosha kuwafanya warudi kwenye njia ya ushindi baada ya sare ya 1-1 wikendi iliyopita dhidi ya Osasuna.

Ancelotti hakufurahishwa sana na kiwango cha Madrid kwa maana ya kushambulia kwani walishindwa kuongeza bao lao la mapema.

"Tulikuwa imara sana na Militao na (Antonio) Rudiger walicheza mchezo mzuri," alisema.

"Tungeweza kufunga mabao zaidi, lakini kwa wakati huu wa msimu haijalishi.

"Kufunga bao la mapema hakujatulazimisha kuwa na haraka, na hatukulazimisha uchezaji wetu kiasi hicho, tulitengeneza nafasi nyingi, lakini hatukufunga vya kutosha.

"Timu imecheza vizuri sana na tumeridhika, msimu uliopita hapa tulifungwa, na leo timu imekuwa imara zaidi.

"Niliwaomba wachezaji wasiwe na hatari ya kupita pasi wakiwa wamechelewa na wahakikishe pasi zao ni sahihi kwa sababu matokeo yalikuwa magumu sana."

Madrid itacheza na Shakhtar Donetsk kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya Jumanne, kabla ya mchuano mkali wa Clasico dhidi ya Barcelona wikendi ijayo.

"Nadhani Clasico bado iko mbali," alisema Ancelotti. "Nimewapumzisha Benzema na Mendy, na huenda ikawa Jumanne naweza kuangalia nani wa kuanza."

,741,460

JACKPOT
MECHI WIKI HII
BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 11/10/22 | 22:00 | Dinamo Zagreb vs RB Salzburg | 2.74 | 3.28 | 2.44 |
| 02. 11/10/22 | 22:00 | AC Milan vs Chelsea | 2.93 | 3.33 | 2.28 |
| 03. 12/10/22 | 17:15 | FC Andorra vs Burgos | 2.24 | 3.02 | 3.32 |
| 04. 12/10/22 | 22:00 | Racing Santander vs Zaragoza | 2.85 | 2.95 | 2.65 |
| 05. 13/10/22 | 03:45 | Corinthians vs Flamengo | 2.87 | 3.16 | 2.30 |
| 06. 13/10/22 | 19:45 | Betis vs Roma | 2.28 | 3.41 | 2.95 |
| 07. 13/10/22 | 19:45 | Union Saint Gilloise vs Sporting Braga | 2.34 | 3.35 | 2.90 |
| 08. 13/10/22 | 19:45 | Nantes vs SC Freiburg | 3.06 | 3.41 | 2.22 |
| 09. 13/10/22 | 19:45 | Slovan Bratislava vs FC Basel | 2.90 | 3.30 | 2.37 |
| 10. 13/10/22 | 19:45 | Djurgardens IF vs KAA Gent | 3.05 | 3.39 | 2.24 |
| 11. 13/10/22 | 22:00 | Trabzonspor vs Monaco | 3.14 | 3.39 | 2.24 |
| 12. 13/10/22 | 22:00 | Ferencvaros TC vs Red Star Belgrade | 2.23 | 3.40 | 3.05 |
| 13. 13/10/22 | 22:00 | Steaua Bucuresti vs Silkeborg | 2.70 | 3.25 | 2.55 |

MECHI ZA USHINDI
"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMATATU - 10/10/2022

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 14:00 | 2636 | Alashkert Martuni vs Artsakh | 1.28 | 5.04 | 8.34 |
| 15:00 | 1264 | Oleksandria vs FC Metalist 1925 | 1.84 | 3.49 | 3.69 |
| 17:00 | 3071 | Alta IF vs Valerenga IF 2 | 1.81 | 3.85 | 3.46 |
| 17:00 | 3227 | AL Karmel vs Al Ahli Amman | 6.42 | 4.09 | 1.43 |
| 17:00 | 3282 | Buqaa Amman vs Baalama | 2.27 | 3.16 | 2.91 |
| 17:00 | 5917 | Radnicki Nis vs FK Radnicki 1923 | 2.11 | 3.26 | 3.12 |
| 17:30 | 5739 | U Craiova SA vs Chindia Targoviste | 2.04 | 3.21 | 3.61 |
| 18:00 | 1691 | Atromitos vs PAS Giannina | 1.78 | 3.20 | 5.00 |
| 18:15 | 1293 | Al Raed Club vs AL Tai | 2.09 | 3.26 | 3.51 |
| 18:15 | 4376 | AL Hazm vs Al Qadisiyah | 1.78 | 3.35 | 4.80 |
| 18:15 | 4492 | AL Arabi (SA) vs AL Riyadh | 2.14 | 3.05 | 3.65 |
| 18:15 | 5353 | Hafnarfjordur vs Leiknir | 1.51 | 4.29 | 4.87 |
| 18:30 | 3331 | NK Radomlje vs ND Gorica | 1.95 | 3.31 | 3.50 |
| 19:00 | 1377 | Kfum Oslo vs Stabaek | 2.87 | 3.56 | 2.12 |
| 19:00 | 2445 | Ironi Kiryat Shmona vs FC Ashdod | 2.22 | 3.20 | 2.96 |
| 19:00 | 2618 | Rakow Czestochowa vs Miedz Legnica | 1.23 | 5.46 | 9.75 |
| 19:00 | 2656 | Fredrikstad vs Bryne | 1.88 | 3.75 | 3.31 |
| 19:00 | 2744 | Sandnes Ulf vs Grorud IL | 1.35 | 4.87 | 6.43 |
| 19:00 | 3130 | AEL Limassol vs Omonia Nicosia | 3.09 | 3.24 | 2.28 |
| 19:00 | 3488 | Aasane Fotball vs Raufoss | 2.42 | 3.54 | 2.48 |
| 19:00 | 4066 | Anorthosis Famagusta vs Apollon Limassol | 2.34 | 3.19 | 3.04 |
| 19:00 | 4432 | Ranheim vs Kongsvinger IL | 2.02 | 3.65 | 3.02 |
| 19:00 | 5101 | Zaglebie Sosnowiec vs Nieciecza KS | 2.69 | 3.22 | 2.39 |
| 19:30 | 1007 | Arsenal Tula vs FC Alania Vladikavkaz | 2.13 | 3.12 | 3.22 |
| 20:00 | 1370 | Trabzonspor vs Kasimpasa | 1.44 | 4.57 | 6.16 |
| 20:00 | 2526 | Norrkoping vs Mjallby | 1.94 | 3.36 | 3.50 |
| 20:00 | 2596 | Horsens vs Aalborg | 2.33 | 3.28 | 2.93 |
| 20:00 | 3088 | Basaksehir vs Sivasspor | 1.56 | 3.93 | 5.57 |
| 20:00 | 3644 | Hajer Club vs AL Akhdood | 4.08 | 3.16 | 1.86 |
| 20:00 | 3909 | CD Trofense vs CD Feirense | 2.70 | 3.09 | 2.55 |
| 20:00 | 3917 | Hapoel Beer Sheva vs Hapoel Haifa | 1.59 | 3.76 | 4.88 |
| 20:00 | 4140 | Videoton FC vs Ujpest FC | 1.81 | 3.54 | 3.79 |
| 20:00 | 4298 | Orebro SK vs Dalkurd FF | 1.70 | 3.90 | 4.65 |
| 20:00 | 4767 | Altay vs Caykur Rizespor | 3.51 | 3.26 | 1.97 |
| 20:00 | 5454 | Hallescher vs Borussia Dortmund II | 2.87 | 3.36 | 2.30 |
| 20:10 | 3891 | Hammarby vs Varbergs Bois | 1.22 | 5.65 | 9.75 |
| 20:30 | 2945 | Al Wehda vs AL Baten | 1.92 | 3.26 | 4.11 |
| 20:30 | 4611 | Al Hilal Riyadh vs Al Shabab Riyadh | 1.89 | 3.61 | 3.81 |
| 20:30 | 4845 | UTA Arad vs CFR Cluj | 3.67 | 3.17 | 2.03 |
| 20:30 | 5058 | Maccabi Tel Aviv vs Hapoel Tel Aviv | 1.26 | 5.09 | 9.00 |
| 21:30 | 1265 | AC Siena vs Cesena | 2.27 | 3.05 | 3.30 |
| 21:30 | 5407 | GKS Piast Gliwice vs Widzew Lodz | 1.92 | 3.31 | 3.61 |
| 21:45 | 2539 | Fiorentina vs Lazio | 2.37 | 3.37 | 2.77 |
| 21:45 | 2554 | Sochaux vs St Etienne | 1.98 | 3.32 | 3.66 |
| 22:00 | 3169 | Eibar vs Mirandes | 1.54 | 3.88 | 5.77 |
| 22:00 | 4557 | Elche vs Mallorca | 2.95 | 2.95 | 2.55 |
| 22:00 | 5653 | Nottingham vs Aston Villa | 3.27 | 3.32 | 2.12 |
| 22:15 | 3026 | FC Arouca vs Famalicao | 2.68 | 3.18 | 2.58 |
| 22:15 | 5574 | Stjarnan vs Vikingur Reykjavik | 4.56 | 4.08 | 1.57 |
| 22:30 | 5551 | Rosario Central vs Defensa Justicia | 2.32 | 2.92 | 3.07 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# SERENGETI GIRLS TAYARI KUIVAA JAPAN KOMBE LA DUNIA J'TANO

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Timu ya Taifa ya Wasichana chini ya miaka 17, 'Serengeti Girls', Bakari Shime, amesema kwa maandalizi waliyofanya wachezaji wake, wapo tayari kuikabili Japan katika mchezo wao wa kwanza wa makundi wa Fainali za Kombe la Dunia.

Fainali za Kombe la Dunia zinatarajiwa kuanza kutimua vumbi kesho nchini India huku Tanzania ikicheza mchezo wake wa kwanza keshokutwa, Jumatano dhidi ya Japan.

**Akizungumza na gazeti hili jana, Shime, alisema kundi walilopangwa si jepesi kwa sababu wanakutana na timu nzuri na watapambana kuhakikisha wanafanya vizuri.**

Alisema kila mchezaji anatambua umuhimu wa kufanya vizuri katika mashindano hayo, lakini mbali ya kuiwakilisha nchi yao pia wachezaji watakuwa wanajiuza wenyewe kupitia michuano hiyo ya dunia.

"Kundi tulilopo ni gumu, kila timu iliyofika katika mashindano haya ni bora, kwa upande wa benchi letu la ufundi tumemaliza, kilichobaki ni kukumbushana baadhi ya mbinu tunapokuwa uwanjani," alisema Shime.

Katika mashindano hayo, Serengeti Girls, imepangwa Kundi D pamoja na Canada, Ufaransa na Japan.

## NIMETETEA...



Bingwa mtetezi wa mbio za Baiskeli kwa Wanaume, Omar Ligoneko wa Bohari ya Dawa nchini (MSD), akimalizia mbio za Km. 40 katika Uwanja wa Mkwakwani jana ikiwa ni mwendelezo wa michezo ya Shirikisho la Michezo ya Wizara na Idara za Serikali (SHIMIWI) inayoendelea jijini Tanga. **MPIGAPICHA WETU**

# Simba yanusa CAF

INATOKA UKURASA 32

Straika huyo alipata mpira mrefu ambao uliwapita Henock Inonga na Joash Onyango akapiga kichwa, lakini shukurani kwa Aishi Manula aliyeruka pembeni na kuudaka kwa ustadi.

Ukosefu wa umakini wa Chama uliikosesha Simba bao dakika ya 37 baada ya krosi ya Mwenda, kumpita beki mmoja wa timu hiyo ukamgonga miguuni na kutoka nje lango likiwa tupu.

Onyango aliiokoa Simba dakika chache kabla ya mapumziko alipouondoa mpira wa hatari wa krosi uliokua ukizagaa kwenye lango la Simba na kuwa kona tasa.

Kipindi cha pili kilipoanza Primeiro de Agosto walibadilika na kuanza kutandaza kandanda safi wakimiliki mpira na kufanya mashambulizi ya hatari wakiwatumia mawinga wao Camilo Bito kushoto na Tshibamba kulia, lakini kazi kubwa iliyofanywa na mabeki wa Simba wakiongozwa na Onyango, pamoja na kipa Manula walikaa imara.

Mwenda alifunga bao la pili dakika ya 62 baada ya kazi nzuri iliyofanywa na Chama, aliyemmegea pande, Kibu Denis kabla ya kumtangulizia mfungaji.

Mwenda alipiga shuti la juu lililotinga kwenye engo ya pembeni ya lango.

# Nabi: Subirini dakika 90 Sudan

INATOKA UKURASA 32

ent Ibenge, alisema Yanga ni timu nzuri na walilijua hilo kwamba kikosi chao kinaundwa na wachezaji wazuri, hivyo ungekuwa mchezo mgumu kwa timu zote mbili.

Alisema katika michuano hiyo hakuna mchezo rahisi, hivyo wanapaswa kujipanga ili kupata matokeo katika mechi ya marudiano ambayo watacheza nyumbani.

"Tumecheza mpira mzuri leo (juzi), japokuwa tumepoteza nafasi nyingi za kufunga, unapokuwa ugenini na kupata nafasi ya kushinda unapaswa kuitumia japokuwa sare sio jambo baya, tunaenda nyumbani kujipanga.

# Michezo

Jumatatu Oktoba 10, 2022

Nipashe




**Abraham: Naweza kurudi London** UKURASA 30

**NI MIMI...**



Beki wa Kulia wa Simba, Israel Mwenda (aliyepiga magoti), akishangilia sambamba na wachezaji wenzake, Clatous Chama (kulia), Kibu Denis na Sadio Kanoute, baada ya kuifungia timu yake bao la tatu wakati ikishinda 3-1 ugenini nchini Angola dhidi ya wenyeji, Primeiro de Agosto kwenye mechi ya Raundi ya Kwanza ya Ligi ya Mabingwa Afrika. **PICHA: SIMBA**

# Simba yanusa makundi CAF

**Na Adam Fungamwango**

●●● Yaweka rekodi Angola ikiitungua De Agosto mabao 3-1, huku Chama, Phiri na Mwenda waki...

KWA mara ya kwanza kwenye historia yao ya soka, wawakilishi wa Tanzania Simba jana walipata ushindi nchini Angola, ilipoibabua Primeiro de Agosto ya Luanda mabao 3-1 kwenye mechi ya mkondo wa kwanza katika Raundi ya Kwanza Ligi ya Mabingwa Afrika, ikichezwa Uwanja wa 11 de Novembro.

**Ni ushindi ambao umewaweka kwenye mazingira mazuri kabla ya mechi ya marudiano itakayochezwa nchini kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa Jumapili wiki hii.**

Mara ya kwanza kucheza mechi nchini humo ilikuwa ni 1993, Kombe la Shirikisho Afrika (CAF) hatua ya nusu fainali dhidi ya Atletico Sportive de Aviacao na kufanikiwa kutoka suluhu, ikitinga fainali baada ya kushinda mabao 3-0 kwenye mechi ya kwanza nchini.

Mara ya pili ilikuwa ni Machi 3, 2013, pambano la Ligi ya Mabingwa Afrika, ikipoteza kwa mabao 4-0, huku ikiwa imefungwa bao 1-0 kwenye mechi ya kwanza iliyochezwa Uwanja wa Taifa wakati huo kwa sasa Benjamin Mkapa.

Yalikuwa ni mabao ya Wazambia wawili, Clatous Chama, Moses Phiri na Mtanzania, Israel Mwenda, huku Mkongomani Dago Tshibamba akiwafungia wenyeji bao dakika 78.

Simba ilianza kubisha hodi langoni mwa wenyeji wao dakika ya pili tu, baada ya faulo la Joash Onyango ilioonekana kama inakwenda wavuni, lakini kipa Sebatian Colo akaruka juu na kuupangua mpira huo.

Dakika nne baadaye Chama aliiandikia Simba bao dakika ya tisa, baada ya kupokea pasi kutoka kwa Augustine Okrah.

Okrah alikimbia na mpira kwa umbali mrefu kwenye wingi ya kushoto na kupiga krosi ya nyuma iliyomkuta mfungaji ambaye kabla ya kuukwamisha wavuni, alitisha kama anapiga na kuwapoteza maboya mabeki na kipa wao.

Krosi ya Moses Phiri dakika ya 15 ingeweza kuipatia Simba bao lakini ikakosa muunganishaji na kutoka nje taratibu ukawa wa kurushwa.

Wenyeji walibadilika kuanzia dakika ya 30 kwani walionekana kutulia na kumiliki mpira kiasi cha dakika 32 kukaribia kusawazisha kupitia kwa Melono Dala.

INAENDELEA UK. 31

## Nabi: Subirini dk.90 Sudan

**Na Saada Akida**

BAADA ya kulazimishwa sare ya bao 1-1 dhidi ya Al Hilal ya Sudan kwenye mchezo wa kwanza wa Raundi ya Kwanza wa Ligi ya Mabingwa Afrika, Kocha Mkuu wa Yanga, Nasreddine Nabi, amesema wamebakiza dakika 90 za kwenda kurekebisha makosa yao na kufuzu hatua ya makundi.

Katika mchezo huo uliochezwa juzi kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam, Yanga ilikuwa ya kwanza kupata bao lake dakika ya 51 kupitia kwa Fiston Mayele huku Al Hilal wakisawazisha katika dakika ya 61 mfungaji akiwa Mohamed Yousif.

Akizungumza na gazeti hili baada ya mchezo huo, Kocha Nabi, alisema unapokosa mabao unampa mpinzani nafasi ya kukuadhibu na kwamba walipopata bao walipoteza nafasi mbili za wazi ambazo kama wangezitumia wangekuwa mbele kwa mabao zaidi ya moja.

Alisema wamefanya makosa ambayo wapinzani wao wameyatumia vizuri na kupata bao la kusawazisha na sasa wanarudi uwanjani kufanyia kazi mapungufu yao kabla ya kurudiana mwishoni mwa wiki hii.

"Tulipokuwa tukishambulia wenzetu walifanya shambulizi la kushtukiza na kupata bao na ambalo lilitutoa mchezoni, na tuliporudi kushambulia tulishindwa kupata bao la ushindi, lakini mchezo huu una dakika 180," alisema Nabi.

Alisema dakika 90 za kwanza zimekamilika na sasa wanajiandaa kwa dakika 90 zilizosalia na anaamini watapata matokeo mazuri katika mchezo wa marudiano.

Kocha huyo alisema hakuna madhara yoyote kwa mabadiliko ya mfumo alioingia nao kwa kumtumia Stephane Aziz Ki kama namba tisa badala ya kucheza pembeni kama ilivyozoeleka.

Kocha Mkuu wa Al Hilal, Flor-

INAENDELEA UK. 31

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >